Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI

**Kikao cha Nane – Tarehe 7 Februari, 2008**

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

## D U A

Spika (*Mhe. Samuel J. Sitta*) Alisoma Dua

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida swali la kwanza linaelekezwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na kwa leo linaulizwa na Mbunge wa Mbozi Mashariki Mheshimiwa Godfrey W. Zambi. Basi tutaliuliza baadaye naomba twende kwenye Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na swali linaulizwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya.

Na. 104

**Kuboresha Malipo ya Wastaafu**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inaboresha mishahara kwa sekta binafsi na ya umma.

(a) Je, Serikali inatumia Sheria ipi ya malipo ya *Pension* kwa Watumishi wake waliostaafu?

(b) Je, ni lini itaboresha mapato ya wastaafu walioko kwenye *Pension* ambayo ni njia mojawapo ya kuwaenzi kwa kazi ya kujenga Taifa waliyoifanya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Umma wamegawanyika katika makundi makubwa mawili, walio katika masharti ya kudumu na pensheni ambapo utaratibu wa malipo yao unatawaliwa na Sheria ya Malipo ya Hitimisho la Kazi (*The Public Service Retirement Benefit Act*) Na. 2 ya mwaka 1999. Na wale walio katika masharti ya *Operation* ambao wanapostaafu mafao yao yanatawaliwa na Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*National Social Security Fund)* Na. 28 ya mwaka 1997.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati najibu hoja za Wabunge waliochangia kwenye hotuba yangu ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2007/2008 nililifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha viwango vya malipo ya pensheni kwa watumishi wake. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kuongeza mishahara ya watumishi mara kwa mara kulingana na uwezo wa Serikali kifedha.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya Tume ya Rais ya Mishahara iliyoainisha maslahi ya Watumishi wa Umma ambapo suala la Pensheni kwa watumishi wa Umma ambapo suala la pensheni kwa watumishi wa umma litazingatiwa.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wote kwa ujumla kuwa na subira na waendelee kutekeleza wajibu wao wakati Serikali inaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya Tume hiyo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, mishahara imepanda kwa sasa hivi na maisha kwa ujumla yamepanda na wastaafu hawa bado wanapata malipo yale yale ya zamani. Je , Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuwalipa wastaafu kwa mshahara uliopo sasa hivi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inafahamu kwamba maisha yamepanda na pia imeongeza mishahara ya Watumishi wa Umma. Suala la wastaafu kama nilivyotangulia kusema bado tunalifanyia kazi kuona uwezo wa Serikali na uwezo wa kuweza kuongeza. Mapato ya Serikali yakiongezeka na pensheni kwa watumishi wa umma nayo pia itaongezeka.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa kujua Serikali imefika wapi kwa sababu kwa muda mrefu Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiishauri Serikali kwamba pensheni ingewekwa kwenye kima cha chini ili kima cha chini kinapoongezeka basi na pensheni nayo inakwenda hivyo kulingana na hali ya maisha inavyobadilika. Serikali inasemaje kuhusu hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo kama ifuatavyo:-

Pensheni kwa wastaafu inalipwa kwa mujibu wa Sheria ambazo nimezitaja, kwa kuwa Sheria hazijabadilika bado hatuwezi kuwalipa wastaafu kwa kina kwa sababu Sheria haisemi hivyo. Pensheni za watumishi zinalipwa kwa kulingana na mshahara wake wa mwisho hivyo mapato yakiongezeka tutaangalia kuangalia hawa watumishi walistaafu hizi siku za nyuma kwa sababu waliostaafu sasa hivi pensheni zao ni bora zaidi kuliko za wale waliostaafu zamani.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ninaomba turejee kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, lile swali ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki. Labda urejee kuuliza tena.

Na. 103

**Fedha za Mfuko wa Barabara**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Je, ni vigezo gani vinavyotumika katika kugawa fedha zinazokusanywa na Mfuko wa Barabara nchini kwa ajili ya Barabara zinazohudumiwa na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya Nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi kwa kuchelewa kwa sababu teknolojia ilikuwa imetusumbua kidogo. Naomba radhi sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko wa Barabara kwa ujumla ni kwa matengenezo ya Barabara zilizo katika hali ya kutengenezeka ambazo zimegawanyika katika makundi matatu. Kundi la kwanza la Barabara zenye hali nzuri (*good*) na kundi la pili Barabara zenye hali ya kuridhisha (*fair*). Pia kiasi cha fedha hizo ni kwa ajili ya

matengenezo ya sehemu korofi (*spot improvement*). Kwa Barabara zilizo katika kundi la tatu zenye hali mbaya (*bad*) ili zote ziweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mwaka 1998/1999, na kuongezeka kwa wingi wa fedha za Barabara kulikuwa na vigezo ambavyo vilikuwa vinatumika lakini havikuwa mahususi kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI hawakuwa wanajua urefu wa Barabara na hali zake. Vigezo hivyo vilivyokuwa vinatumika zamani ni kama vifuatavyo:-

(ii) 85% ya fedha zote zilikuwa zinagawiwa sawa kwa Halmashauri zote nchini.

(iii) 7% zilikuwa zinagawiwa kwa Manispaa ya Jiji.

(iv) 5% zilikuwa zinagawiwa kwa Halmshauri za Miji.

(v) 2% kwa miradi ya maendeleo yaani (*Urban Sector Rehabilitation Program (USRP*).

(vi) 1% kwa ufuatiliaji na ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2004 Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI iliona kuna haja ya kujua urefu wa Barabara zote na hali zake ilivyo yaani (*Local Government Road Inventory and Condition Survey*) wakisaidiwa na Benki ya Dunia. Mwaka 2005 walitafuta Mhandisi Mshauri na alianza kazi Novemba, 2005, na kazi hiyo ya upimaji wa Barabara ilimalizikia Aprili, 2007. Zoezi hilo lilileta matokeo ya kujua urefu kamili wa Barabara kwa kila Wilaya ikiwa ni pamoja na hali zake zilizogawanyika katika mafungu matatu:-

(i) Barabara zilizo nzuri (*Good*).
(ii) Barabara zinazoridhisha (*Fair*).
(iii) Barabara mbaya (*Poor*).

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo yaliweza kuonyesha hali halisi za Barabara kwa kila Wilaya, kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008 vigezo vya ugawaji wa fedha kwenye Halmashauri vilibadilika kutoka vile vya mwanzo na kufuata mahitaji halisi (*Maintenance needs*). Katika kila Halmashauri 93% ya barabara zote ambazo ziko katika hali nzuri na kuridhia (*Good*) zilipata fedha za matengenezo ya kawaida, 70% ya Barabara zote ambazo zinaridhisha (*Fair*) zilipata fedha kwa ajili ya matengenezo maalum (*Period Maintenance*), 25% ya Barabara zote ambazo ziko katika hali mbaya (*Poor*) zilipata fedha za matengenezo ya hapa na pale (*Sport Improvement*) au sehemu korofi ili kufanya Barabara yote iweze kupitika. Kwa hiyo, kigezo kikubwa ni mtandao wa Barabara katika Halmashauri husika na hali ya Barabara zake.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka ijayo utaratibu huu utaendelea kutumika na Bajeti za matengenezo ni lazima ziambatane na hali halisi ya Barabara katika Halmashauri yaani *updated Local Government Road Inventory and Condition Survey.*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri lakini pia naomba niipongeze sana Serikali kwa kuongeza pesa zinazokwenda kwenye Halmashauri na hususani kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kuna ucheleweshaji wa kupeleka pesa kwenye Halmashauri hizi, je, Serikali haioni kwa kufanya hivyo kunaathiri utengenezaji wa Barabara katika maeneo hayo?

Pili, ni lini sasa kasoro hizo zitarekebishwa ili Barabara hizo zitengenezwe kwa wakati ule unaokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU**, **TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Godfrey W. Zambi kama ifuatavyo:-

Ni kweli tunakiri kwamba kuna ucheleweshaji kidogo kwenye fedha hizo za Barabara lakini ukilinganisha na miaka ya nyuma mwaka huu angalau zimewahi sana na hiyo siyo tunafanya kwa makusudi ni kutokana na ukusanyaji wa fedha zenyewe. Fedha hizo zinakusanywa, zikisha kusanywa zikiletwa Ofisini kwetu tunazigawa moja kwa moja kwenye Halmashauri husika. Kama mtakumbuka mwaka huu kwenye mwezi wa 10 tulikuwa tumeshatoa angalau *quarter* mbili ya fedha hizo, kwa hiyo tunakiri upungufu lakini kila siku tutakuwa tunajerekebisha.

Swali la pili ni kwamba tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba fedha hizi zinafika kwa wakati ili zitengeneze hizo Barabara kwa wakati. Lakini kikwazo chetu kikubwa ni hicho ambacho nimekisema katika swali la awali kwamba mara nyingi tunategemea ukusanyaji wa fedha zenyewe lakini hata hivyo Serikali itajitahidi ili fedha hizo zifike kwa wakati.

Na. 105

**Barabara ya Ipole – Rungwa**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA** aliuliza: -

Kwa kuwa, Barabara ya Ipole – Rungwa kwa mwaka wa fedha 2006/2007 haikupatiwa fedha kutokana na Barabara hiyo kuwa na hali mbaya, na kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu alifika na kujionea hali ya Barabara hiyo inayounganisha Tabora – Mbeya;

Je, Serikali iko tayari kuiweka Barabara hiyo kwenye mpango wa maendeleo kwa mwaka 2007/2008 ili kuirejesha kwenye hali ya Barabara yenye hadhi ya Barabara ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBUNU (DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa ni Barabara muhimu ya Kitaifa ambayo inaunganisha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Mbeya. Kutokana na umuhimu wake, Serikali imeitengea fedha ili matengenezo ya kuifanya ipitike kwa urahisi. katika mwaka huu wa fedha 2007/2008, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya matengenezo makubwa sehemu ya Ipole – Kitunda ambapo kwa sasa Mkandarasi anaendelea na kazi. Aidha, matenegenezo ya sehemu korofi kati ya Kitunda – Rungwa yanaendelea kwa gharama ya shilingi milioni 160. Sambamba na kazi hizi, daraja la Olua kwenye Mto Olua linajengwa Kalvati kubwa na sehemu ya Kapumpa Makalvati 20 yanajengwa kwa gharama ya shilingi milioni 233.

Lengo la Serikali ni kujenga Barabara kuu zote nchini ikiwemo Barabara hii ya Tabora - Ipole – Rungwa kwa kiwango cha lami. Wakati Serikali bado inakusanya nguvu za kuijenga Barabara hii kwa kiwango cha lami, itaendelea kuiweka katika mipango yake ya maendeleo ili iendelee kufanyiwa matengenezo ya kukidhi mahitaji na hivyo iweze kupitika majira yote ya mwaka.

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, Barabara hii ni moja kati ya Barabara Kuu zenye hali mbaya sana nchini na kila mwaka imekuwa ikitengewa fedha kama alizokuwa anazitaja hapa fedha ambazo kwa kweli hazikidhi haja ya kuitengeneza Barabara hii iweze kupitika katika kipindi chote cha masika. Je, kwa nini Serikali isikubaliane nami ombi langu nililolitoa na kuhakikisha kwamba Barabara zote kuu zile ambazo ziko kwenye hali mbaya zinapata upendeleo wa kupata fedha za kutosha ili ziweze kupitika katika mwaka wote hasa katika vipindi vya masika?

Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri uliahidi kupitika kwa Barabara hii kwa mwaka huu na hali ya Barabara mpaka hivi tunavyosema ni mbaya na wewe mwenyewe unasema kwamba matengenezo yanaendelea wakati hali ya masika inaendelea. Je, unayo maelekezo mengine ya kuwahakikishia wananchi wa Tarafa ya Kiwele ili Barabara hiyo iweze kupitika kwa wale ambao wanashughulikia matengenezo ya Barabara hiyo katika kipindi hiki?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBUNU (DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Juma Nkumba kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Barabara hiyo ni kati ya Barabara kuu ambazo ziko katika hali mbaya na tulisema kama ambavyo yeye mwenyewe amesema kwamba Serikali itaweka umuhimu mkubwa katika Barabara kuu ambazo bado hatupata fedha za kuzijenga kwa kiwango cha lami. Ahadi yetu bado ni kwamba kufikia mwaka 2015 tuwe na Barabara kuu zote tuwe tumezijenga kwa kiwango cha lami. Lakini wakati tukisubiri kukusanya uwezo huo tutaendelea kuweka fedha nyingi.

Kwa upande wa Barabara hii kwa kweli mwaka huu wa fedha tumeweka fedha nyingi kuliko wakato wowote, fedha nilizozitaja hapa zinakaribia bilioni moja, haijawahi kutokea katika Barabara hii na tutaendelea kufanya hivyo ili Barabara hii iweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie tu wananchi wa Tarafa ya Kiwele na wa Sikonge kwa ujumla kwamba Barabara hii kwa mipango ambayo Serikali imeweka sasa itakuwa inapitika wakati wote wa mwaka. (*Makofi*)

Na.106

**Uwanja wa Ndege wa Mtwara**

**MHE. DUSTAN D. MKAPA** aliuliza**:-**

Kwa kuwa uwanja wa Ndege wa Mtwara ambao ni wa tano kwa ukubwa hapa nchini hauna huduma muhimu kwa usalama wa abiria na wafanyakazi:-

(a)Je, ni lini Serikali itaweka uzio kuzunguka Uwanja na mashine za kukaguliwa abiria na mizigo kama ilivyo kwa Viwanja vya Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro na Zanzibar?

(b)Je, ni lini taa za kwenye njia ya ndege zitawekwa ili kuwezesha ndege kutua usiku na wakati wa hali ya hewa si nzuri?

(c)Je, ni lini njia ya ndege kwenye uwanja huo itafanyiwa matengenezo kwani imejaa viraka na vijituta vidogovidogo ambavyo huleta mtikisiko wakati ndege inapotua au kuruka?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** (**DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimwa Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dustan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu umuhimu wa kuimarisha usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA),* imepanga kumalizia ujenzi wa uzio katika maeneo ya viwanja vya ndege ambavyo yanaruhusu ukatizaji wa watu na wanyama na hivyo kutishia usalama wa usafiri wa anga katika viwanja vya Ndege Lake Manyara, Musoma, Mwanza, Kigoma na Tabora. Kiwanja cha Ndege cha Mtwara kipo katika mpango wa kuzungushiwa uzio katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009.

(b)Mheshimiwa Spika, kuhusu mashine za kukagulia abiria, mizigo na wafanyakazi nafurahi kutoa taarifa kuwa machine hizo zimekwishawasili hapa nchini na hivi sasa zinatolewa bandarini. Hivyo mara tu kazi ya kuzitoa bandarini itakapokamilika zitapelekwa na kufungwa katika kiwanja cha ndege cha Mtwara.

(c)Mheshimiwa Spika, kampuni ya kuchimba gesi iitwayo *ARTIMUS* iliyopo *Mnazi Bay,* Mtwara, imetoa taa kwa mamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania *(TAA)* za kuwezesha ndege kutua au kuruka kwa usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara wakati wa usiku au wakati ambao hali ya hewa katika kiwanja ni mbaya. Taa hizo zijulikanazo kama *Portable AGL'* tayari zimethibitishwa na mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA),* kwamba zina ubora unaotakiwa kwa mujibu wa Sheria. Mfumo huu wa taa za kutulia na kuruka ndege ndiyo mbadala kwa mazingira ambayo zile zinazofungwa za kudumu huibiwa au kuharibiwa na wanyama kama walivyofanya kwa taa zilizokuwepo awali katika kiwanja hicho.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutua na kurukia ndege kwenye Kiwanja cha Ndege cha Mtwara itafanyiwa matengenezo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, swali la nyongeza, nilidhani mwenyewe atasimama.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, hizi *screen machines* ni muhimu katika viwanja vyetu vya ndege kwa kukagulia abiria na mizigo, na kwa kuwa *screen machine* iliyopo katika uwanja wa ndege wa Zanzibar mara kwa mara huwa inaharibika na hadi tarehe 13 Januari mwezi uliopita bado haijafanya kazi. Je ni lini Wizara hii itafanya marekebisho ya uhakika au kupeleka chombo hicho kipya katika uwanja wa ndege wa Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, viwanja vya ndege vya Zanzibar vinaendeshwa chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Zanzibar. Tutaendelea kuwashauri wenzetu wa Mawasiliano na Uchukuzi waone umuhimu wa suala hilo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Kwa kuwa, matatizo ya viwanja vya ndege yanafanana na kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kukarabati kiwanja cha ndege cha Singida pamoja na kukipanua na kwa kuwa kiwanja hicho hakina nyumba ya kufikia wageni kwa ajili ya kunawa mikono hata Viongozi wanaposubiri wageni kuwapokea hawana hata pa kukaa husimama muda wote. Je, Serikali ni lini basi itatenga fedha kwa ajili kujenga nyumba ya kufikia wageni katika kiwanja cha Mkoa wa Singida?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** (**DR. MAUA ABEID DAFTARI** ) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, kama ifuatavyo:

Napenda nimfahamishe Mheshimiwa Diana M. Chilolo kwamba ili kiwanja kiweze kufanya kazi zake vizuri kuna mambo mengi ambayo yanahitaji kukamilishwa. Kiwanja cha ndege cha Singida kina mahitaji makubwa kuna masuala ya uzio, kuna masuala ya kuweka *terminal building*, eneo la kuongozea ndege ndiyo baadaye tufanye masuala ya nyumba ya wageni. *Priority* hizo zikimalizika nyumba ya wageni itashughulikiwa.

Na. 107

**Kupeleka Umeme Bukombe**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa Bukombe ni moja ya Wilaya ambazo hazijapata umeme kabisa; na kwa kuwa hali hiyo inachangia kuwepo kwa wawekezaji wachache katika Wilaya hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme Wilaya ya Bukombe?

(b) Je, umeme huo utapitia njia ipi kati ya njia za Ilogi-Segese-Lugunya-Masumbwe-Ushirombo na Uyovu au Ilogi-Mbogwe-Bukombe-Masumbwe-Ushirombo-Uyovu au ile ya Ilogi-Bukoli-Nyarugusu-Katoro-Lulembela-Ushirombo-Uyovu-Masumbwe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kufikisha umeme katika maeneo yote nchini. Utekelezaji wa azma hii unafanyika hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mpango wa kufikisha umeme maeneo mbalimbali, kipaumbele kimewekwa kufikisha umeme makao makuu ya Wilaya ambazo hazijapata umeme pamoja na maneo yenye viwanda vya kusindika mazao (*Agrobased-industries*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maeleo hayo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, mpango wa kupeleka umeme Wilayani bukombe uko katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Benki ya Maendeleo ya Afrika yaani *African Development Bank* (ADB) imekubali kufadhili mradi huu wa kupeleka umeme Wilayani Bukombe chini ya Mardi unaojulikana kama "*Electricity V*". Kwa sasa Serikali inakamilisha taratibu za kusaini mkataba (*on lending agreement*) na tayari ADB imeshatoa tangazo (*general procurement notice*) kwa ajili ya kupata wataalam washauri (*consultant*) na mkandarasi.

(b)Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa umebaini kuwa njia muafaka kiufundi ya kufikisha umeme Ushirombo ni njia ya KV. 33 toka kituo cha Ilogi kilichopo Wilayani Kahama kwenye Jimbo la Msalala la Mheshimiwa Ezekiel M. Maige kupitia Lunguya –Mbogwe-Bukombe-Kagwe hadi Ushirombo. Aidha, kutakuwa na matawi ya KV 33 kutoka Ushirombo hadi Nipha Ginnery, Lubeho hadi Cargill ginnery.Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani Milioni 4.1 ambazo zinajumuisha ujenzi wa njia kuu za KV 33 nilizozitaja, ufungaji wa transfoma na ujenzi wa laini ndogo za kusambaza umeme kwa wateja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Bukombe napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada ambazo zimefanywa kwa ajili ya kupeleka umeme Bukombe.

Lakini pamoja na pongezi hizo ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, wananchi wa Bukombe wamekuwa na hamu sana ya kusubiri umeme na umeme katika Wilaya ya Bukombe ndiyo ilikuwa siasa kubwa na kwa kuwa umeme huo ukifika Bukombe ninaamini wananchi kule watafanya sherehe kwa sababu wataondokana na gharama kubwa wanazotumia katika jenereta.

Je, unaweza ukawahakikishia wananchi wa Bukombe ni lini sasa umeme utafika Bukombe?

Kwa kuwa njia ambazo zimeonyeshwa pale ni njia nzuri za kutoka Ilogi kupita Mbogwe kwenda mpaka Ushirombo na kurudi pia Masumbwe Serikali inawahakikishia kwamba wananchi wa kule watakaohitaji kuvuta umeme kwenye nyumba zao na viwanda

vyao kupitia maeneo uliyoyasema wananchi wale watapewa umeme au unapitishwa tu nguzo pale na bila wao kuutumia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** : Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kwamba tunawahakikishia wananchi wa Jimbo la Bukombe na wananchi wa Bukombe kwa ujumla kwamba umeme huu utafika kama nilivyosema kwenye jibu la msingi na kwamba fedha hizi zimeshapata kibali, Benki ya Maendeleo ya Afrika imesaini mkataba wa maridhiano kwa ajili ya kufadhili huu mradi mwezi Desemba, 2007. Kwa hiyo, tunawahakikisha wananchi kwamba waendelee kujiandaa tu na umeme utafika. Sasa hivi kama tulivyosema kwenye jibu la msingi kwamba tunaendelea na taratibu za kuwapata wakandarasi waanze inatarajiwa kwamba baada kukamilisha hizo taratibu za kuwapata wakandarasi ujenzi wa laini hizi kwa ajili ya kufikisha huduma hii ya umeme unaanza mara moja.

Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo linaweza kutekelezeka ndani ya mwaka huu. Kuhusu swali la pili niwahakikishie wananchi wote ambako hii laini itapita kwa wale ambao watakuwa na sifa za kuhudumiwa na huu umeme watapata.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwaarifu wananchi kwa faida ya Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Bukombe kwa sababu siyo vijiji vingi sana. Baada ya kutoka Ilogi, Lunguya umeme utapitia kijiji cha Ikinda, Ushirika, Shule Mbogwe, Nanda, Ituga hadi Bukombe. Ikishafika Bukombe umeme utapinda kuelekea Lubeho hadi Masumbwe, Mzambarauni na *Cargill ginnery*. Lakini pia kutoka hapo umeme utaelekea Kagwe, Ushirombo, *Nipha Ginnery*, Bitumbili pamoja na *Ushirombo west*, naomba radhi kwa maeneo ambayo majina yao sikuyatamka kwa uhakika lakini kwa jinsi ambavyo taarifa tumezipata. Tunawahakikishia wananchi wa Bukombe kwamba wataendelea kupata hii huduma. (*Makofi*)

**SPIKA:** Huku kuna ambaye hajauliza siku nyingi lakini samahani jina limenitoka kidogo.

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Riziki.

**SPIKA:** Naam, naam swali la nyongeza.

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hitaji la umeme linahitajika kwa wananchi wengi sana kutokana na matumizi muhimu sana. Mheshimiwa Waziri wakati wa kipindi cha Bajeti aliwaahidi wananchi wa Kipumbwi, Wilaya ya Pangani kuwapatia umeme kutokana na kuwapelekea *transfoma*, gharama ambazo zingegharimu Sh. 7m/= kutokana na majibu yake, hadi hii leo hali ile inaendelea na kwamba wananchi wale bado hawajapelekewa ule umeme. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusiana na hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka jana tuliahidi wakati wa Bajeti, pamoja na hilo Mheshimiwa Rished amekuwa akifuatilia kwa makini kuhusu utekelezaji wa mradi huo na tuliahidi kwamba mpango wa utekelezaji wa mradi huo ulikuwa unapitia Shirika letu la *TANESCO* lakini kama ambavyo imekuwa ikijitokeza kwa muda mrefu tulikuwa na matatizo ya kifedha na tulikuwa na tatizo la vifaa, lakini nimeshamwahidi Mheshimiwa Rished Abdallah kwamba jambo hili tunalishughulikia na narudia tena kuliarifu Bunge lako Tukufu na wananchi wa Pangani kwamba hivi karibuni mradi huu utatekelezeka kwa sababu tulishakubaliana na *TANESCO* kwamba huu mradi utatekelezeka, kwa kweli mradi wa gharama ya Sh. 7m/= kuendelea kuachwa kuwa sehemu ya miradi ambayo inasubiri kutekelezwa inatia aibu na sisi wenyewe hatufurahii. Tunamwahidi tena Mbunge kwa mara nyingine kwamba hivi karibuni tutautekeleza kwa sababu vifaa vitawasili ndani ya mwezi huu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kufika umeme vijijini ni moja na wanavijiji kuweza kumudu gharama za umeme ni suala lingine. Je, kwa nini gharama za kuingiza umeme vijijini hasa katika Vijiji vya Lalangulu, Mabama na Usoke ni kubwa na zimewafanya wananchi kushindwa kuingiza umeme? Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama hizo?

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Arfi kwa swali zuri sana kwa sababu Usoke ipo katika Jimbo la Urambo Mashariki. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya uhakika. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la gharama kwa huduma ya umeme linadhibitiwa kwa mujibu wa sheria. Tuna mamlaka yetu ambayo imepewa mamlaka kutokana na sheria ambayo Bunge hili Tukufu liliipitisha, Sheria ya *EWURA*.

Lakini pia napenda kusema kwamba, kwa kipindi ambacho tunacho kwa kweli Shirika letu la *TANESCO* limekuwa likitoa huduma katika sehemu nyingi sana za nchi hii kwa kiwango kama cha ku-*subsidize*, kama rukuzu, kwa sababu kwa muda mrefu zile gharama halisi zimekuwa hazitozwi kwa wananchi waliokuwa wakiomba huduma ya umeme. Lakini hiyo imekuwa ikifanywa kwa nia njema ili kuwawezesha wananchi. Kwa hiyo, nataka kumwondolea hofu Mheshimiwa Mbunge lakini pia na wewe Mheshimiwa Spika kwamba gharama ambazo zinatozwa ni gharama halisi kulingana na utafiti ambao unafanywa na chombo ambacho tumekipa mamlaka kisheria kupitia Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo tunalifanya ni kama ambavyo tumeelezea kama azma ya Serikali kwamba, nia yetu ni kuhakikisha kwamba huduma hii inatolewa kwa uharaka zaidi na mojawapo ya njia ya kuwezesha hilo ni kuweza kufungua wigo kuwezesha pia wawekezaji wengine waweze kufika kusaidiana na *TANESCO* kwa sababu mzigo ambao *TANESCO* inayo kuwahudumia wananchi na mahitaji ya umeme kwa nchi hii kwa sasa ni makubwa sana na tunaamini kwamba kuliachia shirika moja

kwa kweli ni kulibebesha mzigo ambao pengine haitakuwa haki kulihukumu kwamba limeshindwa kutekeleza. Ndiyo maana tunasema tuliongezee nguvu kwa kusaidiana na wengine lakini wakati huo tukiliimarisha kuhakikisha kwamba lenyewe ndiyo linakuwa mtoaji huduma namba moja.

Tunaamini kwa kufanya hivyo, kwa kuzingatia misingi ya ushindani, tutafika mahali ambapo bei zitakuwa zinapungua au kiwango chake cha kuongezeka kitakuwa tofauti na inavyoonekana sasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 108

**Kuanzishwa kwa Bodi ya Mazao**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na hali ya walanguzi kuwahi vijijini na kununua mazao ya wakulima kwa bei ya chini na hivyo kufanya wakulima kupata bei isiyoendana na gharama za uzalishaji, hali ambayo huendeleza umaskini nchini:-

Je, Serikali imefikia wapi katika mpango wake wa kuanzisha Bodi ya Mazao Makavu Mchanganyiko na gharama za uzalishaji wa mazao yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari inaendelea na mchakato wa kuunda Bodi hiyo itakayohusisha mazao mbalimbali yakiwemo ya nafaka na mazao mengine mchanganyiko. Bodi itasimamia na kudhibiti uzalishaji, utafiti, usindikaji na masoko. Mapendekezo ya kuunda Bodi yameandaliwa na kujadiliwa katika ngazi mbalimbali na kupatiwa maoni ambayo yanasaidia kuboresha mchakato wa uundaji wa Bodi hiyo. Mapendekezo hayo yanalenga kuwasaidia wadau hususan wakulima, wakati nguvu za soko zinaposhindwa kuwa na ufanisi na kuweka kipaumbele na msukumo kwenye usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani na kukuza nafasi za ajira.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na Bodi itakayosimamia mazao yanayohusika kikamilifu, Serikali iliamua kwa kuanzia iandaliwe Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo na bidhaa zake ambayo matamko yake ya kisera yatazingatiwa katika kuandaa muundo na majukumu ya bodi inayotarajiwa kuundwa. Hivyo, ukamilishaji wa mchakato wa kuunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko unasubiri kukamilisha na kupitishwa kwa Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ambayo maandalizi yake yapo katika hatua za mwisho. Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko imewasilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri

kuhusu Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo kwenye Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kupangiwa tarehe ya kujadiliwa na kupatiwa idhini ya utekelezaji.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa msimu uliopita wakulima wa Namtumbo ni moja wa walioathirika sana kwa mazao yao kununuliwa kwa bei ya chini sana na walanguzi wao kwenda kuuza kwa bei ya juu katika kituo cha Serikali. Je, Serikali inaweza kuweka utaratibu wa ununuzi wa mazao hayo vijijini kwa muundo wa stakabadhi ya mazao ghalani wakati wakisubiri soko la mazao yao na utaratibu huu wa uanzishaji wa Bodi ya Mazao?

Pili, kwa kuwa gharama za uzalishaji kwa wakulima hawa zimekuwa zikipanda mwaka hadi mwaka hasa kwa sisi tunaolima kwa kutumia mbolea katika baadhi ya Kata zetu za Wilaya ya Namtumbo, mbolea ya Ruzuku mwaka huu imefikia zaidi ya Sh, 26,000/= toka Sh. 19,000/= iliyokuwa mwaka jana. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa walanguzi hao wanaotumia vipimo visivyo halali katika ununuzi ili kumlinda mkulima katika gharama hiyo na aweze kupata faida ya uzalishaji wa mazao yake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu matumizi ya stakabadhi za mazao. Napenda kwanza kumshukuru Mheshimiwa Kawawa kwa sababu binafsi nakubaliana naye kuhusu suala hili na nataka nimhakikishie kwamba tukitoka hapa nitakwenda kutembelea mkoa wake hususan Jimbo lake. Lakini pia niseme kwamba matumizi ya stakabadhi za mazao sasa ni jambo ambalo tumekwishaanza, tumetumia sana utaratibu huu katika Mkoa wa Mtwara hususan kwenye zao la korosho na inaonyesha kwamba kuna mwelekeo kwamba utaratibu huu ni mzuri.

Lengo la Serikali ni kuangalia matumizi haya katika mkoa ule yatakapoonyesha kwamba ni utaratibu mzuri, basi lengo la Serikali ni kuusambaza utaratibu huu katika mikoa mingine. Kwa hiyo, nitakapotembelea pia Mkoa wa Ruvuma tutaangalia na Mheshimiwa Kawawa kama Mkoa wa Ruvuma utakuwa tayari kuanza utaratibu huu.

Lakini pia naomba nitoe tahadhari kwamba matumizi haya ya stakabadhi za mazao ghalani hata na mbolea ghalani yanategemea sana uimara wa vyombo vinavyosimamia hususan ushirika. Kwa hiyo, lazima tuangalie uimara wa ushirika na viongozi waliopo pale kwa sababu wasipokuwa imara hata matumizi haya yanaweza kuwa ya shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Kawawa na Wabunge wengine kwamba Wizara inatarajia kuleta semina hapa kuwaelezea Waheshimiwa Wabunge jinsi tunavyotarajia kusambaza mbolea kwa msimu ujao kwa kutumia utaratibu huu wa stakabadhi za mazao. Nadhani watapata nafasi nzuri ya kuuliza maswali na kuangalia jinsi hii itakavyochangia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vipimo vinavyotumikwa si kwenye mbolea tu na hata kwenye mazao tumeshuhudia matumizi ya kangomba, lumbesa na vitu vingine. Mimi rai

yangu ni kwamba, vyombo vinavyohusika katika Wilaya na katika maeneo mbalimbali lazima visimamie utaratibu huu kwa sababu tayari sheria na taratibu zipo kwa vipimo vya ujazo, uzito na hata vimiminika, kinachobaki ni kusimamia taratibu hizi ili ziweze kutekelezwa vizuri. Lakini mwisho, niwaombe wafanyabiashara kuwa na huruma na wakulima kwa sababu wao ndio wanaoanzisha huo utaratibu na wakulima mara nyingi wanakuwa hawana fedha, sasa unapowanyanyasa wakulima katika kiwango hicho mwaka mwingine utakwenda kununua wapi? Naomba na wafanyabiashara nao washiriki katika kulidhibiti jambo hili.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali fupi sana la nyongeza. Kwa kuwa imekuwa ni utaratibu wa Serikali mara zote kuwatangazia wafanyakazi mafao na ongezeko la mishahara yao kila mwaka siku ya wafanyakazi na kwa kuwa kumekuwa na siku ya wakulima kila mwaka. Je, Serikali kwa nini isiwe sasa inatumia siku hiyo kuwatangazia wakulima bei za mazao yao, pembejeo na mafao mengine ya wakulima yanayotakiwa yapatikane katika mwaka ule? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza hata kwa wafanyakazi Mei Mosi siku hizi hatutangazi mshahara. Mshahara unatangazwa kulingana na kukua kwa uchumi na kwa kufuata sheria zote ambazo zipo. Lakini kwa mazao ya kilimo tumekubaliana kwamba tunafuata mfumo wa soko huria ambalo ndilo linalopanga bei. Lakini kwa mazao mengi tumefanya mashauriano na Bodi zinazosimamia mazao ili yawepo mashauriano kati ya wanunuzi wa uuzaji na Bodi ili kuweka kitu kinaitwa bei dira kama tulivyofanya kwa zao la korosho mwaka huu ambako bei dira imekuwa Sh. 610/=, lakini kupitia Mfuko wa Stakabadhi Ghalani wameweza kuuza kwa awamu na kulipwa katika awamu mbili na mahesabu yakikamilika inawezekana kuwepo na awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kufuata mfumo huo wa bei dira na kwa mashindano ya soko, mkulima anaweza kupata bei nzuri. Tatizo linalojitokeza ni kwamba wanunuzi badala ya kushindana wanashirikiana na kufanya bei za mkulima kuwa chini na hapo ndipo Serikali tunapokuwa na wajibu wa kuingilia kwa sababu soko la ushindani linaposhindwa Serikali inaingilia kati.

Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Peramiho kwamba Serikali haiwaachi tu wakulima bila kusimamia haki zao. Lakini Serikali haiwezi kupanga bei ya kila zao, mazao ya nchi hii ni mengi yanaanzia kwenye choroko mpaka kwenye kahawa, sijui unaweza kupanga bei za kiasi gani na kwa kutumia mfumo wa soko lipi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikijitokeza mara kwa mara kupiga marufuku uuzaji nje wa mazao ya chakula hasa mahindi na mchele na kwa kuwa hata kama bei ndani ya nchi ni ndogo wakulima hao hulazimika wauze mazao yao ndani ya nchi kwa bei hiyo ndogo. Je, Serikali haioni

kwamba inawanyanyasa wananchi hao ambao wamelima na kuzalisha mazao hayo kwa gharama kubwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Serikali haina nia yoyote ya kuwanyanyasa wakulima, tunachofanya tunaangalia uzalishaji wa mazao, tunatazama kwa msimu halafu tunaangalia pia mahitaji ya wananchi wetu ni kiasi gani.

Sasa pale tunapogundua kwamba unyeshaji wa mvua si mzuri, tukiona pia uzalishaji wa mazao unaweza kuwa sio mzuri kiasi cha kuathiri hali ya usalama wa chakula, basi ndipo tunaposema sasa tunasitisha kuuza mazao nje ya nchi.

Hata hivi sasa tumesitisha kuuza mazao hayo kwa sababu bado tunaangalia jinsi mvua zetu zitakavyoendelea. Lakini lengo kubwa ni kwamba mazao yakiwa mazuri, yakiwa yanatosheleza na hayana athari yoyote au tishio lolote kwa usalama wa chakula Serikali inatoa kibali kwa wananchi kuuza mazao hayo.

Na. 109

**Zao la Jatropha**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:

Kwa kuwa zao la *Jatropha* ni jipya na Watanzania wengi bado hawajalijua na kwa kuwa zao hilo linaonekana kuwa linaweza kuwa mkombozi wa Mtanzania mmoja mmoja na vikundi vya Watanzania wakielimishwa vizuri juu ya zao hilo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulitangaza na kuwaelimisha Watanzania juu ya zao hilo ili walilime kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli, katika soko la dunia na changamoto zinazotokana na uchafuzi wa mazingira, dunia imelazimika kutafuta vyanzo vingine vya nishati, ikiwemo mimea inayozalisha mbegu za mafuta, sukari au wanga.

Mazao ya mimea hiyo yanatumika kutengeneza mafuta ya kuendeshea mitambo yanayojulikana kitaalam kama *bio-fuel* ambayo yanazalishwa kutokana na mbegu za mafuta na aina ya *bio-ethanol* ambayo yanazalishwa kutokana na miwa au wanga uliopo katika mbegu za nafaka.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini, mazao yanayoendelea kufanyiwa utafiti kwa ajili ya kuzalisha *biofuel* ni michikichi, *jatropha* (mbono) na mkonge. Utafiti huo

unafanywa kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, sekta binafsi na Mashirika yasiyo ya Serikali kama *Diligent* na KAKUTE (Arusha), AMMA (Lushoto) na PROKON (Mpanda).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zao la *jatropha* bado ni jipya na utafiti wake unaendelea. Wizara inafuatilia kwa karibu maendeleo ya utafiti huo humu nchini na maeneo mengine duniani, ili kupata taarifa sahihi juu ya zao hilo. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na sekta binafsi na mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoa mafunzo juu ya uzalishaji, usindikaji na matumizi ya mafuta ya *jatropha* ili wakulima na Taifa kwa ujumla linufaike kadri iwezekanavyo na mmea huu unaotoa matumaini makubwa ya kulipunguzia Taifa utegemezi wa kuagiza mafuta ya mitambo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kuitikia wito wa wadau wengi wa zao la *Jatropha* nchini, kuanzia mwaka wa 2006/2007, Serikali ikishirikiana na wadau wa sekta ya kilimo imekuwa ikiendesha mafunzo kwa wataalam wa kilimo ili kuwajengea uwezo wa kwenda kuwafundisha wakulima, kilimo bora cha zao la *Jatropha*. Hadi kufikia Juni, 2007 jumla ya wataalam na wakulima 13,894 kutoka Mikoa ya Manyara, Ruvuma, Mara, Kilimanjaro, Dodoma, Arusha, Tanga, Morogoro, Rukwa, Dar es Salaam na Pwani, pamoja na wataalam 15 kutoka Jeshi la Kujenga Taifa wamepatiwa mafunzo hayo. Aidha, kuanzia mwezi wa Aprili, 2006, jumla ya ekari 250 katika makambi ya JKT Ruvu, Oljoro, Mgambo, Chita, Maramba, Mlale, Makutupora, Itende, Bulombora na Buhemba, zimepandwa ili kuzalisha mbegu. Nimeandaa kipeperushi kinachoonyesha kanuni za kilimo bora cha *Jatropha*. Waheshimiwa Wabunge watapata nakala zao katika visanduku vyao.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatumia maonyesho ya Nane Nane kuwafahamisha wakulima na wadau wengine kuhusu zao la *Jatropha*. Mimea ya *jatropha* imepandwa katika Bustani za Nane Nane zilizopo katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Morogoro na Viwanja vya Nzuguni, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutahadharisha pia kuwa kuna hatari ya kupungua kwa uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula kutokana na uhamasishaji wa uzalishaji wa mazao ya nishati. Tayari bei za nafaka duniani zimepanda na akiba imepungua sana katika kipindi cha miaka kumi iliyopita.

Kutokana na hali hii, Serikali inaweka umuhimu wa kwanza katika usalama wa chakula (*National Food Security*) wakati mazao mengine yakiwemo yale ya nishati yanapewa nafasi ya pili. Aidha, sio sera ya Serikali kuhimiza uzalishaji wa mazao ya nishati katika maeneo/mikoa ambayo ndiyo inategemewa kwa usalama wa chakula.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia napenda kumwuliza kama ifuatavyo:-

Ametamka kwamba baada ya semina na mafunzo amepata wataalam mbalimbali wakiwemo wa kiraia na wa jeshi na baada ya hapo ni jeshi peke yake ambalo limeweza kwenda kuanzisha ekari 250 kwa ajili ya mbegu ambalo bila shaka zinategemewa zisambazwe katika mikoa kadhaa kama alivyoitaja hapa ama mingineyo ambayo utaratibu atauona. Lakini sikuona basi hizi ekari 250 wakishatoa mbegu wanategemea zipandwe katika mashamba mangapi na katika mikoa gani?

Nasema hivi kwa sababu huu ni wakati wa viwango na kasi. Lazima mambo yaende pia kwa takwimu, sikusikia hilo, ningependa anisaidie majibu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kukiri kwamba Serikali haitoi kipaumbele cha kwanza katika mazao ya nishati mbadala kwa maana hiyo.

Lakini napenda afahamu kwamba mojawapo ya mikoa inayosumbuliwa na nishati ni pamoja na Mkoa wa Kagera na katika wataalam waliofundishwa Mkoa wa Kagera haumo.

Je, anaona vipi kama zao hili lingeweza kuanzishwa katika Mkoa wa Kagera ili kusaidia katika nishati mbadala ama ya mafuta au kutoa mazao ambayo yanaweza kupata soko kwa ajili ya kutengeneza sabuni kama ambavyo nimeona katika vipeperushi vyake akielezea?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimfahamishe kwamba malengo ya Serikali kwa mwaka huu ni kuandaa ekari 700, hivi sasa tumeweza ekari 250 kulingana tu na uwezo wa fedha zilizopo, lakini pia si kwamba ni Jeshi tu la Kujenga Taifa linalofanya kazi hii.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, hata kampuni ya *KAKUTE* nayo inatoa utaalam huu na hata katika Mkoa kama wa Rukwa ipo kampuni ya *PROCON* na wanaendelea na uzalishaji wa zao hili.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye swali la Mkoa wa Kagera uhusike, kama Mkoa wa Kagera unayo maeneo ambayo wanaweza kupanda zao hili. Kama nilivyosema mwanzoni ni kwamba, hatupendi watu waanze kubadilisha mazao ya kilimo na kuanza kulima zao la nishati kwa sababu lengo letu namba moja ni *food security* kwa sababu ipo hatari kama nilivyotahadharisha na nimesikia katika Mkoa wa Rukwa kwamba baadhi ya wananchi sasa wameanza kufyeka miti na kuharibu kidogo mazingira kwa ajili ya kupanda zao hili. Kwa hiyo, tunatahadharisha kwamba tusibadilishe, tusifanye *substitution* ya zao hili kwa mazao ya chakula. Lakini Mkoa wa Kagera mimi nawakaribisha kabisa na kwa kuwa zao hili ndiyo linaanza si mwanzo na mwisho hata Mkoa wa Kagera tunaweza kuangalia maeneo yanayofaa na tukauhusisha.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa nimwulize swali kama ifuatavyo. Pamoja na Serikali kuhimiza zao la *jatropha* pamoja na mimi pia kugawa mbegu kwenye Jimbo langu kama kilo mia tano tatizo tulilonalo sasa hivi je, ni wapi *jatropha* inauzwa na kwa bei gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema zao hili bado ni jipya na linaendelea kufanyiwa utafiti lakini matokeo ambayo yamekwishajionyesha katika nchi mbalimbali inaonyesha kwamba kuna matumaini makubwa. Sasa kinachotakiwa ni sisi kuwasiliana na wale wanunuzi ili waweze kufanya mikataba ya kibiashara na wakulima wetu. Hivi sasa bei bado si nzuri sana maana yake bei iliyopo kwa wale waliokwishaanza inacheza kati ya Sh. 120/= na Sh. 200/= kwa kilo. Lakini nina hakika hii ni kutokana tu na soko lililopo ambalo bado halijawa kubwa na watu hawajajua matumizi ya zao hili. Zao hili likieleweka nina hakika kwamba wanunuzi watakuwa wengi na bei itakuwa kubwa. Ningemwomba Mheshimiwa Kimaro pia awasiliane na wenzake wa Mkoa wa Rukwa kwa sababu kule kuna kampuni ya *PROCON* ambayo imekwishajiingiza katika biashara hizi na vilevile yale makampuni niliyoyataka kama ya *KAKUTE* na *AMMA*, wote hawa wanazo taarifa za zao hili na bei yake.

Swali la pili ni kwamba tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba fedha hizi zinafika kwa wakati ili zitengeneze hizo Barabara kwa wakati. Lakini kikwazo chetu kikubwa ni hicho ambacho nimekisema katika swali la awali kwamba mara nyingi tunategemea ukusanyaji wa fedha zenyewe lakini hata hivyo Serikali itajitahidi ili fedha hizo zifike kwa wakati.

Na. 110

**Tatizo la Walimu Kuchelewa Kupata Mishahara**

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inajitahidi kufuta kero ya upungufu wa walimu kwa kupeleka mashuleni walimu wapya wengi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufuta kero ya walimu hao wapya kukaa muda mrefu bila mishahara?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, zimeweka mkakati unaosaidia kupunguza kero ya walimu wapya kukaa muda mrefu bila mshahara.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai 2006, Wizara yangu imeunganishwa kwenye mtandao wa moja kwa moja na Hazina kwa lengo la kuharakisha walimu wanaoajiriwa kuingia kwenye orodha ya mishahara ya watumishi wa Serikali (*Payroll*).

Aidha, Wizara imeunda Kikosi Kazi *Task Force* maalum kwa kushughulikia uingizwaji wa walimu wapya kwenye *Payroll* kwa walimu watakaohitimu mafunzo ya ualimu Februari, 2008, Wizara imepanga kuwatuma Maafisa katika Vyuo vya Ualimu kuanzia tarehe 11 Februari, 2008 ili kuhakikisha kuwa fomu zinazohusiana na taratibu za ajira zinakamilishwa kabla hawajaondoka Vyuoni. Lengo walimu wote wawe wameingizwa kwenye *Payroll* katika kipindi kilichozidi miezi miwili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuwaagiza Wakuu wa Shule wakisaidiana na Waratibu wa Elimu ya Sekondari wa Wilaya kuwasilisha haraka taarifa za walimu wapya wanaoripoti katika Vituo vyao bila kusubiri wote wakamilike. Aidha, Wizara inawataka walimu wapya wanapopangwa katika Vituo waende kuripoti haraka badala ya kupoteza muda mwingi wakitafuta kubadilisha Vituo vya kazi bila kuwa na sababu za lazima. Jambo ambalo linasababisha ucheleweshaji wa mishahara. Kwa sasa kila Mkoa umekuwa ukichukua jitihada za makusudi za kurekebisha mazingira ya kazi na kuwaandaa mapokezi kwa walimu wapya. Tunaishukuru Mikoa kwa kuchukua hatua hizo za makusudi.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa imefikia hatua kwamba mpaka walimu wanapanga kugoma kwa sababu ya mishahara; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri juzi wakati alipokuwa anajibu swali hapa alisema kwamba anategemea mpaka mwisho wa mwaka huu watakuwa wameajiri walimu zaidi ya 10,000 nadhani pamoja na wale wa Zanzibar. Je, sasa Wizara ina mkakati gani kuhakikisha wale waliokuwepo wanalipwa na hao watakaokuja watalipwa mara moja kwa sababu hii kule vijijini ni tatizo kubwa sana inabidi Waheshimiwa Wabunge na wananchi wachangie kuishi kwa walimu hao?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niongeze kwa yale majibu mazuri ambayo tayari amekwishayatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mafunzo ya Elimu na Ufundi kuhusu suala la matatizo ya walimu na mishahara yao mipya.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ningechukua nafasi hii kwanza kuweka wazi kwamba hatujafikia uamuzi wa kuchukua walimu toka Zanzibar kama nilivyoeleza awali kwamba

ni jambo ambalo linafanyiwa kazi. Kwa hiyo, ningependa niliweke wazi kwamba uamuzi haujafikiwa bado linajadiliwa.

La pili, kuhusu walimu wapya kama alivyoeleza Naibu Waziri, mipango tumeweka mizuri, tatizo linalokuja ambalo naamini ni mojawapo ya mambo ambayo Chama cha Walimu kimetangaza pengine kuja kufanya mgomo baadaye kama halitapatikana suluhisho si hasa mishahara mipya, sana ni masuala ya malimbikizo ya posho zao za likizo, uhamisho na tuseme kama mwalimu hajalipwa mishahara ya nyuma, kama amefika kwenye Kituo chake cha kazi ile mishahara yake ya nyuma ambayo alikuwa bado hajalipwa ndiyo wanayodai sana. Kwa hiyo, naweza kusema ni malimbikizo ya mishahara na malimbikizo ya madeni mengine ya posho mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ningechukua nafasi hii kuwashukuru Chama cha Walimu kwamba nimeona barua ambayo wamemwandikia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi ya Umma kwamba tukutane nao. Kwa hiyo, tukikutana nao naamini tutazungumza vizuri, na naamini kabisa hata mgomo huo hautafanyika kwa sababu panapokuwa na maelewano kati ya Serikali na Chama cha Wafanyakazi mambo huwa yanaishi vizuri tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningetaka tu nimhakikishie Mheshimiwa Hamza Mwenegoha kwamba kwa utaratibu tuliouweka walimu wengi wapya hawatakosa mishahara, kama alivyosema Naibu Waziri wanaopata matatizo sana ya mishahara mipya ni wale wanaochelewa kuripoti kwenye Vituo vyao vya kazi. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Ingawa karibu anifilisi Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, lakini nitauliza swali dogo. Kama taarifa zangu ni sahihi ni kwamba walimu wanakusudia kugoma wakidai Serikali malimbikizo ya zaidi ya shilingi bilioni tisa (9). *(Makofi)*

Sasa na Serikali inasema kwamba inafikiria Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuajiri walimu kutoka Zanzibar. Sasa je, isingekuwa vizuri zaidi kwanza Serikali ikawalipa malimbikizo walimu hao baada ya kufikiria kuwaajiri walimu wengine huku deni bado lipo kubwa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii pia kurudia kwamba suala la walimu kutoka Zanziba bado linajadiliwa hatujafikia uamuzi kwamba sasa tunawachukua au hatuwachukui. Ni suala ambalo bado linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, halafu nilitaka kusema kwamba suala la malimbikizo kweli ni baya kwa sababu wafanyakazi wanastahili kupata haki zao zote, na sisi tunakubali hivyo kwamba kwa kweli ni muhimu wafanyakazi wapate haki zao wanaostahili kwa wakati. Lakini ilimradi tumekwishakubali naamini kabisa tutakutana nao, tutajadiliana

malimbikizo yatafanyiwa kazi wakati shughuli zingine za kazi zinaendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la malimbikizo ya walimu litafanyiwa kazi ili walimu wapatiwe haki zao kadri fedha zitakavyopatikana, na hasa baada ya majadiliano na sisi na wao. Naomba nimhakikishie Mbunge kwamba hilo litafanyiwa kazi. Walimu tunawaomba waendelee kuchapa kazi wakati suala lao linashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, wanachodai kwa kweli ni kama shilingi bilioni 8 na kidogo tu. Kwa sababu kwenye shule za msingi tunafahamu wanadai kama shilingi bilioni 7 na kwa upande wa waliopo chini ya Katibu Mkuu yaani Secondary na Vyuo ni kama shilingi bilioni 1.6. Kwa hiyo, yatashughulikiwa tu.

**SPIKA:** Suala la mwisho la nyongeza. Karibu sana Mheshimiwa Halima Mdee. Natumaini unaendelea vyema na masomo huko Afrika ya Kusini au sijui umehitimu tayari?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, bado sijahitimu nipo kwenye likizo, nimemaliza *semester* moja.

Mheshimiwa Spika, mimi nina swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna malimbikizo makubwa ya mishahara ya walimu na suala hili la malimbikizo ni la miaka mingi kila siku tunalizungumza tu.

Je, Serikali leo ipo tayari kuji-*commit* kuwalipa walimu fedha zao hasa hasa kwa zile fedha ambazo sasa hivi zinakusanya kwa wale watu ambao walijichotea mabilioni ya *BOT? (Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani umeleta jambo jipya kabisa hilo. Kwa hiyo, tunaendelea. *(Kicheko)*

Na. 111

**Mafunzo Stadi za Kazi –JKT**

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, JKT wanafundisha stadi za kazi kwenye Kambi zao:-

(a) Je, ni aina gani za stadi za kazi zinazofundishwa pale JKT?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti na kuongeza aina za stadi za kazi?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa katika vikosi vyake hufundisha stadi za kazi mbalimbali kama zifuatazo:-

(1) Ushonaji nguo;
(2) Useremala;
(3) Uashi;
(4) Umeme wa majumbani;
(5) Umeme wa magari;
(6) Uungaji vyuma;
(7) Ufundi wa magari;
(8) Ufundi mafriji;
(9) Useketaji na ufungaji ;
(10) Kilimo, mifugo na uvuvi; na
(11) Ujasiriamali.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Ufundi Stadi nchini *(VETA)* hufanya tafiti za stadi za kazi mara kwa mara kutegemeana na ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii ndani ya Wilaya zetu. Tafiti hizo zinaangalia mahitaji ya ufundi stadi kwa Wilaya mbalimbali ili mafunzo yatakapotolewa yaweze kusaidia katika kuwapatia vijana ajira pamoja na kuinua mapato yao. Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekamilisha utafiti, na matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuwa zipo fani nyingi za stadi za kazi zinazohitaji kufundishwa. Kutokana na utafiti huo, utaratibu unaandaliwa wa kuongeza aina ya stadi za kazi ili ziweze kufundishwa katika Vyuo vyetu vya Ufundi pamoja na JKT.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, licha ya kupatia mafunzo hayo ya ufundi vijana wengi hao bado wameshindwa kujiajiri. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia vijana hao kujiajiri na kuweza kuendeleza shughuli zao?

(b) Kwa kuwa, baadhi ya vijana hao ni mafundi wazuri, lakini wachache tu uajiriwa na SUMA JKT. Je, ni vigezo vipi vinavyotumiwa na SUMA JKT katika kuwaajiri vijana hao?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu (a) Serikali imeandaa mpango ambao unawawezesha vijana hao kuweza kujiajiri. Mpango ambao umeandaliwa na Serikali ni kutoa shilingi

bilioni moja kwa kila Mkoa ili waweze kukopa. Ninachowaomba vijana hao ni kujikusanya pamoja ili waweze kuchangamkia fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu (b) vigezo ambavyo SUMA JKT inavitumia katika kuwaajiri vijana hao ni kwamba kwanza wawe ni mafundi wazuri. Lakini la pili, ni nafasi ambazo zitakuwepo katika Shirika hili la SUMA JKT. Kama mnavyoelewa kwamba nafasi walizonazo za uajiri katika Shirika letu la SUMA JKT kila mwaka ni chache. Kwa hiyo, *definitely* hawataweza kuwaajiri vijana hao wote licha kwamba wengine ni mafundi wazuri.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Tanzania ina mbao nyingi na nzuri kwa ajili ya kutengeneza fenicha za hadhi za Kimataifa, lakini bado tunaagiza fenicha.

Je, Wizara kwa nini haipeleki vijana hao wa JKT nje ya nchi kujifunza kutengeneza fenicha nzuri ili waje hapa watengeneze badala ya kusafirisha magogo kupeleka nchi za nje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ningedhani Wizara ya Maliasili na Utalii wangeweza kusaidia. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa nini tusiwafundishe vijana wetu kutengeneza fenicha nzuri na mbao tunazo badala yake tunapeleka magogo nje na mbao na kuagiza fenicha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kuona kwamba ni muhimu Wizara yangu ijibu swali hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba kwanza usafirishaji wa magogo nje ya nchi hauruhusiwi kisheria. Wote wanaosafirisha magogo nje ya nchi wanafanya kinyemela na Serikali inachukua hatua zote kuhakikisha kwamba hiki hakifanyiki.

Pili, hao vijana wanaojifunza stadi za kazi JKT na *VETA* mbalimbali zipo kazi nyingi sana za kufanya katika utengenezaji wa thamani kutokana na mazao ya misitu.

**MHE. HAFIDH A. TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kuniona na pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake yaliyotokana na swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, JKT ni chombo kinachowafundisha vijana sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini JKU kule Zanzibar hali kadhalika inafanya kazi zinazofanana na kitengo hiki cha JKT japokuwa ni sekta mbalimbali na si za Muungano.

Lakini Bunge lako tuliwaomba Wizara washirikiane na vijana hao wa JKU ili kuwapatia mafunzo yanayolingana na ufundi unaohusika katika sehemu hizi mbili. Je,

Wizara imechukua hatua gani na vijana hao hivi sasa wameungana vipi katika kujipatia ufundi katika sehemu hizi mbili za Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza mwenyewe kwamba wametupa ushauri Wizara yetu ishirikiane na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambayo ndiyo inayoongoza JKU kwa upande wa Zanzibar. Nataka nimhakikishie kwamba ushauri huo tuliupokea na tumeanza kushirikiana. Viongozi wa JKT na viongozi wa JKU wamekwishakutana mara mbili toka tumepokea ushauri huo, wamekutana Dar es Salama na wamekutana Zanzibar na wataendelea kukutana ili kuweza kushirikiana.

Na. 112

**Majengo ya Shirika la Nyumba la Taifa – Dar es Salaam**

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam hayana "*Parking*" hali inayosababisha magari kuwekwa maeneo ya wapita kwa miguu ambao pia hulazimika kutumia njia za magari na hivyo kuhatarisha maisha yao; na kwa kuwa, inashangaza kwa Shirika la Nyumba la Taifa kuingia ubia wa kujenga majengo yao hususani katikati ya Jiji hali inayoongeza tatizo hilo:-

(a)Je, Serikali itakubali kuwa, baadhi ya majengo ya Shirika hilo yavunjwe na kujengwa maegesho ya magari ukiwa kama mradi badala ya makazi?

(b)Kwa kuwa, azma ya Serikali ni kuona kila Mtanzania anapata makazi bora na ya heshima; na kwa kuwa kuna wapangaji katika nyumba hizo waliokaa na kulipa kodi kwa kipindi kirefu ambazo zimeshafidia gharama za ujenzi?

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwamilikisha wapangaji hao nyumba hizo na hivyo kuwasaidia kupambana na umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haikubaliani na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuvunja baadhi ya majengo ya Shirika la Nyumba la Taifa na kufanya maegesho ya magari kwa vile ni kinyume na Sheria Na.2 ya mwaka 1990 ambayo ndiyo iliyoanzisha Shirika la Nyumba la Taifa. Aidha, majengo yanayojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa yanazingatia Sheria ya Ardhi na Sheria za Mipangomiji.

Ujenzi hufanyika katika viwanja vilivyopimwa au maeneo ambayo nyumba chakavu zinabomolewa ili kupisha maendelezo mapya. Jukumu la kuandaa maeneo ya maegesho ya magari ni la Manispaa ya Ilala. Aidha, pia ni jukumu la Manispaa ya Ilala kuweka masharti kwa kila nyumba inayojengwa ili iwe na maeneo ya maegesho ya magari, kwani hii si kazi ya Shirika la Nyumba la Taifa.

Hivyo, napenda kutoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri zote nchini ikiwemo Manispaa ya Ilala, kuheshimu maeneo ya wazi na kutoyavamia ili yaweze kutumika katika shughuli za huduma za jamii ikiwemo maegesho ya magari.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Shirika la Nyumba la Taifa halina mpango wa kuwauzia nyumba wapangaji wanaokaa kwenye nyumba za Shirika.

Hata hivyo, Shirika lilianza kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kuuza nyumba ndogo ndogo na za kati kwa wapangaji waliokuwa wakiishi kwenye nyumba hizo mwaka 1993. Nyumba zinazohusika kwenye mpango huu ni 4,992. Nyumba zilizouzwa ni zile zilizojengwa na Shirika na siyo zilizotaifishwa. Hadi Januari, 2008 nyumba 4,948 zilikuwa zimelipiwa kikamilifu na nyumba 44 zinaendelea kulipiwa.

Aidha, kwa sasa Shirika la Nyumba la Taifa linajenga nyumba kwa ajili ya kuuza na kupangisha. Hadi Januari, 2008 Shirika limejenga takriban nyumba 400 kwa ajili ya kuuza katika maeneo kadhaa yafuatayo:-

(i) Nyumba 191 eneo la Boko (DSM);
(ii) Nyumba 47 eneo la *Mbezi Beach* (DSM);
(iii) Nyumba 7 eneo la Kijenge (Arusha);
(iv) Nyumba 69 eneo la Tabata (DSM);
(v) Nyumba 3 Kapripoint (Mwanza;)
(vi) Nyumba 8 Ilala ( DSM); na
(vii) Nyumba 63 eneo la Mbweni JKT (DSM).

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Mussa Zungu, kuuliza swali la nyongeza. Ningeomba tutambue kwa heshima uwepo wa Mheshimiwa Mama Regina Lowassa mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Swali langu lilikuwa la kuishauri Shirika hili liweze kuingia nalo katika biashara ya kufanya maegesho ya magari. Inaelekea Serikali haikubali. Hili jibu la kuwa Halmashauri zetu zizingatie maeneo ya uwazi linatoka wapi?

Pili, Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kwamba sasa inataka kuwa na majengo mapya katika Jiji la Dar es Salaam suala ambalo wote tunalikubali. Lakini Serikali vilevile haioni umuhimu kuwa majengo haya ni Mji Mkongwe wa Dar es Salaam ukabaki kama ulivyo na yakatafutwa maeneo mapya ili waweze kujenga?

Mheshimiwa Spika, lakini baya kabisa na sheria zote ambazo zipo na Sera ya Shirika la Nyumba la Taifa, Mpango huu wa kujenga majengo mapya katika Jiji la Dar es Salaam unashabikia kuwafukuza wakazi wa zamani kuwapeleka nje ya Jiji la Dar es Salaam na kukaribisha wageni ambao wana uwezo mkubwa wa kukaa Mjini?

Serikali haioni kwamba inaleta matabaka ya watu katika Jiji la Dar es Salaam na katika maeneo mengine katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge umekwishauliza maswali mawili hayo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba Shirika la Nyumba lilianzishwa ili kujenga nyumba za makazi na kuwasaidia wananchi wasiojiweza.

Mheshimiwa Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge ni nzuri na yeyote ambaye atapenda kuingia ubia na Shirika la Nyumba la Taifa ili kuweza kujenga eneo la *Parking* katika maeneo mabovu alete mapendekezo katika Shirika la Nyumba.

Mheshimiwa Spika, suala la kujibu maeneo wazi yalindwe limetoka wapi? Bado tutasisitiza kama Sheria za Ardhi zinavyosema kwamba maeneo yote yaliyo wazi lazima yazingatiwe kwa matumizi yaliyowekwa, na natoa wito kwa Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam kuwa maeneo yote yaliyo wazi ambayo yamechukuliwa au kuvamiwa kinyume cha sheria yarudishwe na Mheshimiwa Waziri amekwishaagiza nchi nzima na kufuatilia kwamba maeneo yaliyo wazi yarudishwe kwa matumizi yaliyoandaliwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, majengo mabovu yaliyopo Dar es Salaam ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema yabaki kama kumbukumbu ya Mji Mkongwe wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa maelezo kwamba majengo yanayoingiwa ubia mengi ni yale ambayo yamekuwa *condemned buildings* au ni sehemu ya majengo yaliyochakaa ambayo hayafai.

Vile vile kutokana na kuanzisha Shirika la Nyumba la Taifa mwaka 1990 na pia Sheria iliyorekebisha sheria hiyo ya mwaka 2005 inataka Shirika lijiendeshe kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Shirika limebuni njia ya kuweza kupata fedha zaidi kwa kuingia ubia kukarabati majengo ambayo yapo katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Na. 113

**Kuzuia Uvutaji wa Sigara Kwenye Maeneo ya Hadhara**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni dhahiri kuwa uvutaji wa sigara una matatizo na madhara makubwa kwa wavutaji; na kwa kuwa, ulimwengu mzima unapiga vita uvutaji sigara hadharani:-

(a) Je, ni lini Serikali itapiga marufuku uvutaji wa sigara katika hadhara kama kwenye "*clubs*", mabaa, mahospitalini na sehemu zingine zenye mikusanyiko?

(b) Je, ni hatua gani zitachukuliwa na Serikali kwa wavutaji wa sigara wanaovuta hadharani bila kujali athari zake kwa wengine?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa moshi wa tumbaku una madhara makubwa ya afya, si kwa mvutaji tu, lakini ni pamoja na watu wengine wanaovuta moshi wa mvutaji.

Napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekwishapiga marufuku uvutaji wa sigara katika maeneo ya hadhara kwa sheria ya udhibiti wa bidhaa za tumbaku Na.2 mwaka 2003 ambayo ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 2003. Kifungu cha 12(1) cha Sheria hiyo kinapiga marufuku uvutaji sigara katika maeneo ya umma.

Maeneo hayo yanajumuisha vituo vya kutolea huduma za afya, maktaba, sehemu za kuabudia, majengo yanayotumiwa kwa mikutano ya kijamii na kiutamaduni, sehemu za michezo, sehemu za kulia chakula, maeneo ya mazingira yaliyojengwa kama vile masoko na maduka.

Aidha, inawataka wamiliki wa baa, hoteli, na kadhalika kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wanaotumia sigara na bidhaa nyingine za tumbaku. Maeneo hayo yawekwe onyo la uvutaji sigara na bidhaa nyingine za tumbaku ili kuendelea kuwakumbusha wavutaji. Kwa taarifa, hivi sasa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Kambarage Nyerere ni "*Smoke free zone*."

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria niliyoitaja, mtu yeyote anayevuta hadharani anakiuka sheria na hivyo anakuwa ametenda kosa la jinai. Kulingana na kifungu Na.28(3) cha Sheria ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku, adhabu ya faini isiyozidi Shs.500,000/= au kifungo cha muda usiozidi mwaka mmoja inaweza kutolewa iwapo mtu atatiwa hatiani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kutoa elimu ya afya kwa umma wakiwemo watumiaji wa bidhaa za tumbaku waweze kufahamu madhara ya tumbaku na kuzingatia kuepuka matumizi ya bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa wote na kuwakumbusha wanaotumia bidhaa za tumbaku waache kwani ni hatari kwa afya zao pamoja na afya za wananchi wengine. Ahsante.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba sheria ipo, naomba kuuliza kama Sheria ipo mbona haitekelezwi na Serikali inachukua hatua gani?

La pili, Serikali haioni kuendelea kuwa na kiwanda cha sigara hapa nchini ni sawa na kuhimiza wananchi waendelee kuvuta sigara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce Kimaro, ukumbuke kwamba Urambo tunalima tumbaku. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba Sheria hiyo ipo, na kwamba mtu yeyote yule ambaye anaonekana anafanya hivyo anafanya kosa la jinai.

Sheria inatakiwa itekelezwe, na mtu yeyote anayeonekana anafanya hivyo anatakiwa kuchukuliwa hatua ili apelekwe Mahakamani ili sheria iweze kutekelezeka. Kama huyo mtu hajachukuliwa akapelekwa kule kwa kushtakiwa ina maana basi sheria itaonekana haitumiki lakini sheria ipo.

Kwa hiyo, nawaomba wananchi na sisi tusaidiane ili yule ambaye anakiuka tumpeleke ili akahukumiwe na sheria hii ndiyo itakuwa inatekelezeka. Lakini inaonekana watu hawapelekwi ndiyo maana sheria haishiki mkondo wake, lakini sheria ipo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu kiwanda cha sigara ambacho kipo hapa nchini. Kama tunavyofahamu kuna maeneo mawili hapa ambayo yanaguswa. Kwanza, kuna sehemu ambayo wanachi wanalima tumbaku ambapo inaongeza kipato cha uchumi, na hii inaongeza kipato cha wananchi na kuweza kuendesha maisha yao. Lakini vilevile kwa maana hiyo hatuwezi tukakifunga kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi kwa upande wetu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni wajibu wetu na ni haki yetu kueleza kwamba matumizi ya baadhi ya vitu vingine ambavyo vinahatarisha maisha ya wananchi, ni jukumu letu kutoa elimu hiyo.

Kwa hiyo, sisi kama Serikali hatuwezi tukasema kiwanda kifungwe, lakini wakati huo huo sisi kama Serikali tunatoa pia angalizo kwamba utumiaji wa sigara ni hatari kwa afya ya mtumiaji.

Kwa hiyo, ni wajibu wetu kuendelea kusisitiza kwamba ni hatari, na tunawaomba wasitumie bidhaa hiyo. Lakini wakati huo huo isiathiri upatikanaji kwa wale wanaolima tumbaku na vilevile kupata kipato na kwa sababu ya maisha ya watumiaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa jibu nzuri. Sasa Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho lilikuwa limeondolewa, yamebakia maswali mawili. Nakusudia katika muda huu tuyamalize haya. Kwa hiyo, tunahamia kwenye swali linalofuata linaloulizwa na Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Kusini.

Na. 114

**Ugonjwa wa Ebola**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa Ebola umepamba moto nchi ya jirani ya Uganda; na kwa kuwa inasadikiwa kuwa ugonjwa wa UKIMWI uliingia Tanzania kutoka Uganda; je, Serikali inachukua hatua gani za kudhibiti kuingia kwa ugonjwa hatari wa Ebola nchini Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imekuwa ikifuatilia kwa karibu taarifa za kuzuka kwa ugonjwa hatari wa *Ebola Haemmorhagic Fever* na mwenendo wake katika nchi jirani ya Uganda. Kwa kuzingatia hali halisi ya mwingiliano mkubwa kati ya wananchi wa Tanzania na Uganda waishio mipakani katika shughuli zao za kila siku Wizara imeweka na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na ugonjwa huu ili kuhakikisha kuwa haungii nchini. Baadhi ya mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

(1) Imewaandikia barua Waganga Wakuu wote wa Mikoa na Wilaya nchini kuwatahadharisha juu ya ugonjwa huu.

(2) Kutoa Elimu ya Afya kwa umma na kwa watumishi wa Afya ili kuweza kutambua mapema na kuzuia kuenea kwa ugonjwa huu.

(3) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Afya juu ya jinsi ya kutibu na kuzuia maambukizi ya ugonjwa huu (*Case Management and Infection Prevention and Control).*

(4) Kuhakikisha kwamba vifaa vya kinga (*PersonalProtective Equipments, PPEs*) pamoja na dawa vinapatikana na kukagua mara kwa mara *stock* za vifaa hivi endapo ugonjwa utatokea.

(5) Kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa (*Intensifying Surveillance*) hasa katika maeneo yote yenye uwezekano mkubwa wa ugonjwa kuingia nchini kama maeneo ya mipaka ya nchi kavu na majini pamoja na viwanja vya ndege.

(6) Kuunda timu ya wataalamu ya Kitaifa (*National Task Force*) itakayoratibu masuala yote yanayohusu mwenendo wa ugonjwa huu; na

(7) Utafutaji wa fedha (*Resource mobilization*) ili kuweza kutekeleza mikakati hii.

(8) Imepeleka timu ya wataalamu katika Mikoa ambayo iko katika hatari zaidi ya kupata maambukizo ya ugonjwa huu kutoka nchi za jirani. Wataalamu hawa kukutana na timu za milipuko za Mikoa na Wilaya na kujadiliana zaidi jinsi ya kufuatilia, kuchukua hatua za kitaalamu na kutoa taarifa mapema endapo ugonjwa huu utajitokeza.

(9) Imeandaa mkakati wa muda mrefu (*Long Term Plan*) kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako kwamba hadi sasa hakuna mgonjwa hata mmoja aliyegundulika kuwa na ugonjwa huu wa *ebola*.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

Katika viwanja vya ndege upo utaratibu wa kwamba wageni wanaoingia basi wanaonyesha *vaccination card* kuonyesha kwamba afya zao ziko sawa sawa. Lakini sina hakika kama utaratibu huu unatumika katika mipaka yetu ya nchi kavu pamoja na majini; je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulieleza Bunge hili kwamba utaratibu wa kuhakikisha kwamba wanaoingia ni salama kiafya katika mipaka yetu ya nchi kavu na majini upo?

Pili, je kuna dawa yoyote ya kinga ambayo ipo kwa ajili ya ugonjwa huu? Ahsante Mheshimiwa Spika.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa kwamba wale wanaoingia kwenye mipaka yetu kupitia nchi kavu ni muhimu wawe wanaonekana kwamba ni salama. Ndiyo maana nimesema kwamba katika ile mikakati ambayo nimeitaja katika jibu langu la msingi nimesema wataalamu na wananchi wamewekwa pale na wafanyakazi wamewekwa kufanya *surveillance*. Lakini nachukua ushauri ili tuweze kuangalia ni mkakati gani ambao tutafanya ili kila anayeingia katika mipaka yetu aweze kuonekana kuwa kama ni salama. Tumechukua ushauri wake.

Mheshimiwa Spika, pili, hakuna kinga ya ugonjwa wa *ebola*.

Na. 115

**Uchunguzi wa Kesi Kuchukua Muda Mrefu**

**MHE. BENSON M. MPESYA (K.n.y. MHE. RICHARD S. NYAULAWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na ucheleweshaji wa kesi Mahakamani kutokana na uchunguzi wa kesi kuchukua muda mrefu; na kwa kuwa ucheleweshaji huo husababisha mateso na kuwanyima haki watuhumiwa na kuongeza gharama za utunzaji kwa Serikali:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka kiwango cha juu cha kufanya uchunguzi wa kesi ili kupunguza kero hizo;

(b) Je, Serikali inaweza kuruhusu wachunguzi wa kesi binafsi na kuwapa uwezo wa kuendesha mashtaka Mahakamani sanjari na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua umuhimu wa kuweka ukomo wa muda wa kufanya upelelezi katika kesi za jinai zilizopo Mahakamani. Ukomo huo umeainishwa katika Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai Nchini Na. 9 ya mwaka 1985 (*The Criminal Procedure Act, Cap. 20 R.E. 2002)* ambayo inataka kesi zote ziweze kupelelezwa kwa kipindi kisichozidi siku 60 isipokuwa kesi zinazohusisha makosa ya mauaji, uhujumu uchumi, kughushi hati, uhaini na uchochezi wa kuasi Serikali. Hata hivyo, kipindi hicho cha siku 60 chaweza kuombewa kuongezwa kwa mujibu wa sheria hiyo iwapo kuna sababu za msingi ambazo zimesababisha kuchelewa kukamilika kwa upelelezi wa shauri husika. Mamlaka inayohusika kuomba ongezeko la siku zaidi za upelelezi ni Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa, Wakili wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka uchini.

Endapo mtuhumiwa ama jamaa yake hajaridhika na mwenendo wa uchunguzi, basi anaweza kupeleka malalamiko yake Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ambaye

atatumia mamlaka yake kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai Na. 9 ya mwaka 1985 na *Attorney General Act* Na. 4 ya mwaka 2005 ikiwa ni pamoja na kuondoa shitaka Mahakamani.

(b) Serikali imeunda vyombo vya kushughulikia ukusanyaji wa ushahidi kwa njia ya upelelezi na inayo wataalamu katika fani mbalimbali. Vyombo hivyo ni Jeshi la Polisi, TAKUKURU, *TRA*, UHAMIAJI, Maliasili na kadhalika.

Mpaka sasa hakuna mapungufu yaliyojitokeza na kusababisha haki za wananchi kutoshughulikiwa ipasavyo hivyo kulazimu kuruhusu wachunguzi/wapelelezi binafsi kupewa uwezo wa kuchunguza kesi za jinai.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mkurugenzi wa Mashitaka anaweza kuwapa uwezo wa kuendesha Mashtaka Mawakili wa kujitegemea kwa ajili ya kuendesha kesi maalum kadri atakavyoona inafaa kwa manufaa ya umma. Ni matumaini yangu kwamba Sheria ya Mfumo wa Mashtaka Nchi (*The National Prosecutions Service Act, 2007)* itakapoanza kutumika itaharakisha upelelezi wa kesi na hivyo kuufanya utaratibu wa utoaji haki kuwa wenye ufanisi zaidi.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpaka sasa hivi wapo Watanzania wengi ambao kesi zao hazijakwisha ndani ya siku 60 kama tunavyoelezwa na Mheshimiwa Waziri, Watanzania hawa wamekuwa wakisota, wakipata taabu bila haki yao kupatikana; je, Serikali kwa kutumia sheria hiyo hiyo ya siku 60 ipo tayari kuziangalia kesi zote zilizo katika Magereza ili wale wanaostahili waondolewe haraka?

**NAIBU WAZIRI USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kushughulikia kesi zote ambazo zimechelewa na hatua hiyo imeanza kuchukuliwa kupitia Magereza mbalimbali, kuonana na wahusika ili kujua chanzo cha kesi zao na pale inapoonekana kuwa hawana makosa hatua huchukuliwa kuwatoa watuhumiwa hao.

Na. 116

**Usalama wa Watanzania Wanaoishi Ujerumani**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:**

*(Swali lililotajwa hapo juu lilifutwa na muuliza swali)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Tunayo matangazo. Nitaanza na wageni. Nilikwishamtambulisha Mheshimiwa Mama Regina Lowassa na mkamtambua. Kwa hiyo, nitaendelea na wengine wageni wa Mheshimiwa Yahya Kassim Issa ambao mmoja anatoka jimbo la Chwaka naye ni Suleiman Ame Kibeni naomba asimame. Yule pale! Na wengine ni kutoka Uingereza, Catriona Spiller, Annabel James na China Collins. *Could you please*

*stand up, so that the Members can acknowledge you. Thank you very much for being here, we welcome visitors to Tanzania all the time. Thank you! (Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Anna Lupembe ni kikundi cha Maombi kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Dodoma Mjini. Naomba wasimame pale walipo. Wale pale! Ahsante sana kikundi cha Maombi tunatumaini mnaliombea Bunge na hususan mmwombee sana Spika wenu. Kazi ngumu hii. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Juma Killimbah kutoka jimbo lake la Iramba Magharibi, nitawataja haraka haraka Bwana Mbarak Mpanda. Daudi Napunigwa, Jumanne Mpindi. Naomba wasimame wale pale. Mkisimama mbaki mmesimama, Eliamin Mbaya, Elizabeth Stephano, Richard Kisiwa, Bakar Maharia, na Fadhili Mkenka. Karibuni sana, tunashukuru kuwaona hapa. *(Makofi)*

Wapo pia wageni, iwa Mheshimiwa Aggrey Mwanri ambao ni Ndugu Daniel Andrea Sandewa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha. Mheshimiwa Mwenyekiti upo wapi usimame. Mwenyekiti karibu sana. Ahsante sana na Ndugu Colnel Ngudungi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha. Ahsante sana. Natumaini mnashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kwa kazi za maendeleo za Siha. Kama tunavyotazamia Wenyeviti na Wakurugenzi wengine kuwaunga mkono Wabunge sehemu zao. Ahsante sana. (*Makofi)*

Wapo wanafunzi 18 kutoka *Independent School* Dar es Salaam pamoja na walimu wao. Karibuni sana wajukuu zangu, tunafurahi sana mmesafiri kutoka mbali sana. Natumaini mnafurahia hali ya Dodoma na pia tunawashukuru walimu wa *Independent School* kwa kuwaleta watoto mapema wajue demokrasia ya nchi yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo vijana 21 wa TAYOA wanaendelea na ziara yao ya mafunzo. TAYOA naomba msimam, wale pale! Karibuni sana na mwendelee kuchanganyika na Waheshimiwa Wabunge nje ya ukumbi kwa sababu mtajifunza mengi kwa kuweza kujadiliana nao mambo mbalimbali. Karibuni sana TAYOA! Vilevile wapo wanafunzi kutoka Chuo cha Biashara Dodoma. Wale pale! Karibuni na nyinyi pia ujumbe ni ule ule. Ahsante sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Hassan Ali Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ameniomba nitangaze kwamba Kamati ya Maliasili na Mazingira itakutana leo saa 7.00 mchana ukumbi namba 231.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyochunguza Mchakato wa

**Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura Ulioipa Ushindi**
**"Richmond Development Company LLC" ya Houston,**
**Texas – Marekani Mwaka 2006**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge orodha yangu ya wachangiaji kwa hoja hii ni 44.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Kuhusu utaratibu! Kanuni ya 59 (a).

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako baada ya Kamati Teule kuleta ripoti yake jana ambayo ilikuwa nzuri sana. Baada ya kupitia vitabu vile, nilichokiona mimi ambacho ningependa kupata mwongozo wako, moja, watuhumiwa hawakupata nafasi ya kuhojiwa na Kamati Teule. Naomba mwongozo wako!

**SPIKA:** Sasa ukianza kusema watuhumiwa na sijui nani hakupata nafasi na kadhalika, inatupa shida kwa sababu umelifunga funga jambo lenyewe, wala halieleweki. Ripoti ni ndefu kurasa zaidi ya 160. Unataka uwe wazi zaidi au unaishia hapo tu?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Nataka niwe wazi zaidi. Mheshimiwa Spika, ukiangalia watu wote walioitwa kuhojiwa na mapendekezo yaliyotolewa sikuona popote pale ambapo Waziri Mkuu aliitwa kuhojiwa. Naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Ukiileta hoja kwa namna hiyo…! Mheshimiwa Waziri Mkuu unataka kuongezea labda?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba uniachie jambo hilo, nitatoa katika maelezo yangu.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Umeniondoa katika utata wa kujaribu kujibu swali ambalo kwa kweli kwa maoni yangu lilikuwa linatangulia mjadala wenyewe. Kwa sababu mazingira hayo yalitakiwa yazingatiwe kwenye mjadala na wote tutawapa nafasi. Napenda kukuarifuni kwamba Kamati ya Uongozi imeniruhusu kwamba ikiwa itabidi tutaendelea hadi Jumatatu. Kwa hiyo, mtu asiwe na shaka kwamba amejiorodhesha atakosa nafasi ya kusema. (*Makofi)*

Sasa katika orodha yangu kama ninavyosema nina wasemaji 44, wameongezeka 7 kwa hiyo, 51. Sawa! Mtaona kwamba katika ile orodha sitaifuata ilivyo na ninayo sababu. Sababu kubwa ni kuzingatia kanuni ya 60, Kanuni ndogo ya (5) ambayo inamtaka kuwa Spika aangalie wale waliokwishachangia katika Mkutano huo huo kwenye hoja nyingine wasubiri ili tutangulize wale ambao hawajachangia. Kwa mfano, Mheshimiwa George Simbachewene namba 7 kwenye orodha yangu amekwishachangia hoja mara mbili katika Mkutano huu, Katibu anaweka rekodi. Vilevile Mheshimiwa Mgana Msindai na kadhalika. Nisitoe mifano yote nitapoteza wakati. Kwa hiyo, mkiona naruka sio kwamba nakwepa kitu chochote, hatimaye wote mtasema, hata hivyo, kwa

hiyo sioni tatizo.Kwa hiyo, sasa nitamwita msemaji wangu wa kwanza ambaye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunifanya msemaji wa kwanza katika hoja hii.

Lakini la pili, nimpongeze Dr. Harrison Mwakyembe, Mwenyekiti wa Kamati Teule, kwa kuwasilisha kwa mbwembwe nyingi sana taarifa yake, mbwembwe zilikuwa nzuri kweli. *(Makofi)*

Kwa kazi nzuri kwa maoni yao, wamewasilisha vizuri. Lakini nimesimama kuweka kwenye kumbukumbu kutoridhika kwangu na jinsi kazi hiyo ilivyofanywa. Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe ni mwanasheria, tena Daktari, alikuwa anafundisha wanafunzi Chuo Kikuu. Moja ya vitu alivyokuwa anafundisha ni *"Natural Justice"*.

Mheshimiwa Spika, wewe pia ni mwanasheria, unafahamu suala la *Natural Justice.* Kwamba Kamati Teule imesikiliza watu wengine wote pamoja na wanaoita minong'ono ya mitaani, wamesafiri mpaka Marekani kutafuta mashahidi, lakini mimi ambaye ni mmoja katika watuhumiwa mle hawakunihoji hata siku moja!

Mheshimiwa Spika, nimesimama kueleza masikitiko yangu. Ofisi ya Bunge mpaka ofisini kwangu hata wangeniita ningekwenda kwa miguu kama hamna gari na nilikuwa tayari kufanya hivyo. (*Makofi)*

Hawa ni watu makini sana siwezi kuamini kwamba wanaweza wakafanya *oversight* kama hiyo. Kwa sababu katika kila hoja walizojenga wamesema Waziri Mkuu ilikuwa hivi. Kulikuwa na shida gani kuja kuniuliza Waziri Mkuu wanasema ulitoa dokezo hili ni sawa? Ni kweli? Kulikuwa na shida gani kwa mfano kufuata utaratibu wa *Westminster* kuthibitisha hapo unaposema mwenye *Richmond* ni fulani uka-*lay on the table records* na ushahidi kuwa ni fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taifa letu ni Taifa changa, lakini chombo hiki ndiyo mahali pa demokrasia, pakubwa katika nchi, hapa ndipo penyewe. Kama katika chombo hiki haki haitaonekana kutendeka nchi yetu haitakwenda vizuri. Hapa ndipo tunategemea tuwaonyeshe umakini wetu, umahiri wetu katika mambo ya demokrasia. Kwa hiyo, nilichofanyiwa napenda kuweka kumbukumbu sawa kwamba naona si sahihi, nimefadhaika sana, nimedhalilishwa sana, nimeonewa sana katika hili. Maana zimechukuliwa tuhuma zikaja zikaelezwa hapa kwamba hivi ndivyo ilivyo. Mimi sijaulizwa. Kulikuwa na shida gani ya kuniuliza, kwa nini muamini minong'ono ya mitaani kuliko maelezo yangu? Sisi wote hapa ni wanasiasa, tukianza kuamini minong'ono ya mitaani niambieni mwanasiasa atakayesimama! Hatuwezi! Tume imepewa muda wa kutosha lakini inashindwa kumuona mtu ambaye wanamtuhumu na wanamsema kwa kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini hata pale uliponinong'oneza ukaniuliza una ushahidi wowote nilikupa ushahidi huo wa maandishi. Katika taarifa yao hakuna hata moja ya ushahidi ambao umetoka kwa Waziri Mkuu. Kile kitabu cha majedwali kimejaa majedwali mengi pamoja na magazeti mpaka ya Udaku lakini maelezo ya Waziri Mkuu hakuna hata moja. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini ingekuwa ni heshima wangeiweka halafu wakasema tunakataa kitambulisho hiki kwa sababu hii na hii na hii, hiyo ndiyo imejengwa hoja. Lakini kujenga hoja na kuja hapa Bungeni tunahutubia nchi nzima na kusema Waziri Mkuu amefanya hiki, amefanya hiki bila ya kumsikiliza nachelea kuuliza hivi mtu wa chini itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, lakini nimetafakari kwa makini sana jambo hili, nikajiuliza hivi hasa kulikoni mpaka watu wazima wenye uwezo wao, watu maarufu wenye heshima zao mpaka wafike mahali waache jambo la msingi kama hilo kulikoni? Mimi nadhani *there is a wish which I am going to grant*, ni Uwaziri Mkuu. Nadhani tatizo ni Uwaziri Mkuu. Kwamba ionekane Waziri Mkuu ndio amefanya haya, tumuondolee heshima au tumwajibishe.

Mheshimiwa Spika, nimetafakari sana kwa niaba ya Chama changu, kwa niaba ya Serikali yangu, nimeamua kumwandikia Rais barua ya kumwomba niachie ngazi. Nafanya hivyo kwa moyo mweupe kabisa ili kuonyesha dhana ya uwajibikaji lakini na kutokukubaliana na utaratibu uliotumika kusema uongo ndani ya Bunge wa kumsingizia mtu. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais kwa heshima aliyonipa ya kutumikia nchi hii kwa Uwaziri Mkuu kwa miaka miwili. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi)*

Nakushukuru wewe, nawashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge na wanachama wa CCM tuliosimamia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tamko hilo ni zito sana na wala sikulitegemea. Sasa ningeomba ushauri tuendeje? Tuchangie tu hakuna haja ya kunong'ona na kupiga kelele?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Spika!

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Waziri Mkuu ndio Mkuu wa Shughuli za kila siku za Serikali na ndio Msimamizi wa shughuli za kila siku za Mawaziri wote na kabla Mawaziri hawajateuliwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anashauriana na Waziri Mkuu katika kuteua Mawaziri. Kwa maana hiyo *Executive power* ya Rais anai-*share* na Waziri Mkuu. Kwa tamko hili la Mheshimiwa Waziri Mkuu la kumwomba Mheshimiwa Rais kujiuzulu

kama nimeweka tafsiri sawa sawa, naomba mwongozo wako juu ya tafsiri ya Katiba. Kwa muono wangu ni kwamba Baraza zima la Mawaziri kuanzia hivi sasa limejiuzulu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba ….!

**SPIKA:** *Order! Order please* ! Utulivu, utulivu!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Nimeomba mwongozo wako sasa nashangaa Mawaziri wanapoanza kusema bado Rais hajakubali. Nilikuwa naomba tu mwongozo wako juu ya hili kwa mujibu wa uzoefu wako wa Kikatiba na masuala kama haya ya kiuongozi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu ni kama ifuatavyo:- Hadi sasa sijapata mawasiliano yoyote kutoka kwa Mheshimiwa Rais kunieleza kama amekubali kujiuzulu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa sababu utaratibu ndio huo alichoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ni kwamba amewasilisha kwa Mheshimiwa Rais kama mamlaka ya uteuzi kusudio lake la kujiuzulu. Sasa hatuwezi kulifanyia kazi kusudio, kwa hiyo, tuendelee tutaona mambo kadri yanavyokwenda. Hayo mengine yanayofuata sasa yanaanguka, hayana maana kabisa kwa sababu…!

**MBUNGE FULANI:** Tuahirishe Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Hiyo ndiyo *ruling* yangu. Kama mnataka ku-*challlenge Speaker's ruling* kanuni inahitaji mambo mengine tofauti, mkate rufaa kwa Kamati ya Kanuni.

Mwongozo kuhusu jambo lingine?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Ushauri !

**SPIKA:** Hapana hakuna ushauri. Kwenye kanuni yetu hakuna ushauri, kuna neno taarifa kama unataka. Mwongozo kuhusu jambo lingine?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Ndiyo Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Hayaa!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, uliomba ushauri wewe mwenyewe na nadhani hujafuta kauli hiyo ya namna gani tuendelee. Kwa hiyo, mimi siendelei na hilo lililokuwepo nataka kwenda kwenye kile ulichokiomba wewe.

Mheshimiwa Spika, na mimi nakubaliana na wewe kwamba hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kauli nzito na kwa kuwa ni kauli nzito inahitaji iangaliwe kwa namna yake. Lakini kilichoko mbele yetu ni Kanuni ya 119, Toleo la 2007 na nina rejea hapa Kanuni ndogo ya 3 ambayo inatokana na kanuni ndogo ya 2, "Taarifa ya

Kamati Teule itawasilishwa Bungeni na Mwenyekiti" na ya 3 inasema "Iwapo baada ya hoja kutolewa Bunge litaamua kujadili Taarifa hiyo, hoja itakayotolewa Bungeni itakuwa ni kwa madhumuni ya kuliomba Bunge likubali mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo."

Mheshimiwa Spika, sasa kwa tafsiri yangu ni kweli pamoja na yale aliyoyaeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu, mapendekezo ya Kamati Teule yaligusa maeneo mengi sana. Moja ni eneo la Waziri Mkuu lakini kuna maeneo mengi ambayo yaliguswa na kuna mapendekezo ambayo pia yametolewa yanayohusu namna gani utendaji katika sheria zetu katika taasisi zetu unaweza kuboresha kwa maana ya mapendekezo yale.

Sasa kwa kuwa kanuni ya 3 inataka ile taarifa ijadiliwe; na kwa kuwa taarifa kujadiliwa hata wangejiuzulu wale wote waliotajwa bado kuna mambo mazito ambayo yanatakiwa kuamuliwa, mimi nadhani Bunge bado lina nafasi ya kujadili. Suala sasa ni je, kwa mfano, Waziri Mkuu amejiuzulu na Mawaziri wote, Bunge linaweza kuendelea kujadili wakati Waziri Mkuu hayupo na Mawaziri hawapo? Hilo ni suala ambalo tunahitaji kuliangalia. Lakini hakuna kitakachoondoa nafasi ya Bunge kujadili yale yote ambayo yamekwisha kuwasilishwa yanayotokana na Kamati ambayo imeundwa na Bunge lenyewe.

**SPIKA:** Naomba nieleweke kwamba mimi sijafunga mjadala. Niliomba tu kwamba kwa tukio hili, lazima tukubali kauli ya Spika kwamba tukio hili sasa ni zito sana lililotokea sasa hivi. Sasa nilikuwa nasema tunaendelea tu na mjadala moja kwa moja? Mheshimiwa Masilingi hebu nisaidie!

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza katika hatua hii. Katika orodha ya awali nilikuwa sijaomba hata kuchangia, siko kwenye orodha nilikuwa bado natafakari mambo hayo. Baada ya kusikia kauli ya Waziri Mkuu kama mchangiaji wa kwanza katika mjadala wa hoja iliyopo mbele ya Bunge hili, lazima tukubali mambo mawili ambayo lazima tuyazingatie kabla ya kushauri.

La kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu hajajiuzulu. Bado ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aliposimama kulieleza Bunge hili Tukufu na Taifa ni masononeko yake, kutoridhika kwake na jinsi Kamati Teule ilivyofanya kazi kuhusiana na yeye. Akasema anatafakari binafsi kwa heshima yake kama Waziri Mkuu na ameamua kwa sasa kumwandikia Mheshimiwa Rais. Kama amekwishaandika haijafika au kama imefika haijajibiwa kwa sababu sisi tulivyofahamishwa hapa yeye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, hilo ndio nilikuwa nataka lieleweke.

La pili, baada ya mjadala kuanza kwa mujibu wa kanuni, kanuni ile inataka tuamue mapendekezo ya Kamati Teule. Lakini baada ya mshituko huu tulioupata lazima tukiri mshituko umetokea. Hatukutarajia mchangiaji wa kwanza asimame na kutupigia hoja nzito ya namna hii ambayo hatuwezi kusema Waziri Mkuu tuliyempigia kura sisi hapa tukampa imani kwa kura nyingi sana awe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, atuambie hapa kwamba anakusudia kutoka halalfu tuseme mambo yanaendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wewe kuwa na wewe umeshituka. Si kawaida kuomba mwongozo kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Kwa sababu nimekuwa kwenye Bunge hili tangu mwaka 1995 hili jambo sijawahi kuliona, nimeliona leo. Sasa sisi ni watu wazima, Mheshimiwa Spika ni mzima kuliko mimi, mzoefu kuliko mimi. Tuliambiwa katika ukumbi wa Bunge hili na baba wa Taifa alipokuja kutu-*brief* kuhusu mambo ya suluhisho la Burundi, alitutahadharisha Wabunge. Nikiwa ndani ya ukumbi alisema: "Nyinyi ni viongozi wazito sana, Taifa hili linawategemea sana Wabunge. Jihadharini sana na kauli zenu mnazozisema ndani ya ukumbi huu. Akamalizia kwa kusema: "Mambo mazito huamuliwa na watu wenye subira." Mwisho wa kumnukuu Baba wa Taifa. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, Bunge haliishi leo, dunia haiishi leo. Mambo mazito ya watu wenye subira, na sisi ni watu wazito, tuwe na subira. Napendekeza tuahirishe ili tutafakari na kushauriana nje ya ukumbi. Na sisi tuna chama chetu, huyu ni Mbunge wa CCM, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, twende tutafakari hili na yeye kwenye *party caucaus* tukirudi ku-*debate* sio kwamba nasema tufute mjadala tutafakari tujue tunasongaje mbele. Wengine wameshituka, hapa wanaweza wasichangie sawa sawa au wengine wanaweza wakaanza kulia hapa halafu jasho likawa linavuruga hoja zilizoko mbele yetu. Mapendekezo ya Kamati Teule ni mengi sana kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Slaa na Mheshimiwa Waziri Mkuu hakupendekezwa ajiuzulu mle, mimi nimesoma ingawaje kurasa kadhaa nimemweleza Katibu wa Bunge hazimo kwenye kitabu changu 67 – 74. Nilisema niletewe nakala nyingine, inawezekana labda kwenye nakala hizo ambazo sina labda ndimo humo ziko, siamini ndiyo hivyo.

**SPIKA:** Nadhani nimeuelewa ushauri wako.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Naomba tuahirishe ili baada ya kutafakari tuangalie tunaendeleaje. Naomba kuwasilisha hoja.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Kuhusu utaratibu! Kanuni ya 47 inatupa fursa ya kuweza kuahirisha mjadala. Kwa kutumia kanuni ya 47 na kwa kuzingatia lililotokea sasa ndani ya Bunge, naomba kutoa hoja kwamba tuahirishe kwa muda mjadala huu wa kujadili Taarifa ya Kamati Teule kuhusiana na suala la *Richmond* mpaka hapo utakapotuita baadaye. Naomba kutoa hoja!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mimi niliomba ushauri tu haya yote mnanipeleka kwenye mzunguko wa bure tu. Sasa naamua! Waheshimiwa Wabunge

kutokana na hali hii isiyo ya kawaida; na kutokana na ukweli kwamba lazima Spika apate ushauri mzuri wa kisheria na pia aweze kuwasiliana na mamlaka ambazo hazimo humu Bungeni nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja.

*(Saa 5.11 Asubuhi Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge…!

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu utaratibu!

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Selelii Kanuni ipi?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Bunge, nasimama kuhusu utaratibu chini ya Kanuni ya 59 (d) ili niweze kutoa taarifa inayotokana na Kikao chetu cha dharura cha Kamati Teule leo hii kuhusu mchango uliotolewa na Waziri Mkuu leo asubuhi ambao bila ufafanuzi kutoka kwenye Kamati Teule unaweza ukalipotosha Bunge lako na kuathiri mwenendo wa mjadala.

**SPIKA:** Hujawa wazi, unajaribu kusema kwamba alipochangia Mheshimiwa Waziri Mkuu kunahitajika ufafanuzi?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ndiyo na ndiyo maana nimetumia Kanuni ya 59 (d).

**SPIKA:** Sawa, endelea.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Bunge lako Tukufu ambayo tulifanya Kikao cha dharura mchana huu baada ya kusitisha shughuli za Bunge mchana.

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Waziri Mkuu ameituhumu Kamati Teule kwamba imesema uongo ndani ya Bunge na kumsingizia. Katika taarifa yetu yenye kurasa 165 hakuna sehemu hata moja tuliyosema uongo au kumsingizia, hivyo tunadai uthibitisho wa kauli yake au ifute kauli hiyo, vinginevyo Kamati teule itachukuwa hatua chini ya Kanuni ya 63(8) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu amedai kuwa kitabu cha viambatisho cha Kamati teule kimejaa majedwali pamoja na magazeti mengi mpaka ya udaku lakini kwenye maelezo ya Waziri Mkuu hakuna hata moja. Tunamtaka Waziri Mkuu aseme hayo magazeti ya udaku ni yapi katika taarifa yetu. Vilevile kitabu cha Kamati Teule cha viambatisho kina jumla ya nyaraka 104, hiki hapa chenye uthibitisho wa hoja zetu zote za msingi. Ili kuwapunguzia kazi Wabunge kuzitafuta nyaraka hizo zinazomhusu Waziri

Mkuu kwenye kitabu hiki nimezitenga chache na naomba kibali chako ili nyaraka hizo zigawiwe kwa Waheshimiwa Wabunge sasa hivi. Zote zinatoka, viambatisho vyote tumeviweka katika taarifa yetu.

**SPIKA:** Itabidi nivione mezani kujiridhisha.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, sawa. Aidha, Waziri Mkuu amedai alikupa wewe ushahidi wa maandishi ambao Kamati Tuele haikuujumuisha kwenye taarifa yake ya mwisho. Naomba tuwe wakweli, ushahidi huo wa maandishi anaouongelea Waziri Mkuu ni barua yenye Kumbukumbu Namba PM/P/567/2/40 ya tarehe 21/09/2006 yenye kurasa mbili ambayo Waziri Mkuu alimwandikia Waziri wa Nishati na Madini wakati huo Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mbunge, akimshauri awe mwangilifu na Kampuni ya Richmond, kampuni ambayo yeye mwenyewe aliiteua tarehe 21/06/2006.

Mheshimiwa Spika, barua hii tuliipata tarehe 28/01/2008 kupitia kwako tukiwa hapa hapa Dodoma. Kamati Teule isingeweza kuitumia barua hiyo kwenye taarifa yake kwa sababu mbili kubwa. Kwanza, Taarifa ya Kamati Teule ilikuwa imekwishawasilishwa kwako Mheshimiwa Spika tarehe 31/12/2007. Hivyo isingekuwa rahisi kwa Kamati Teule kuichomeka barua hiyo kwenye Taarifa iliyokwisha wasilishwa kwa Spika.

Mheshimiwa Spika, kama mchezo huo unafanyika sehemu nyingine, kwa Kamati Teule hii ikiongozwa na Mwanasheria aliyebobea, Wajumbe makini wenye nia njema kwa taifa hili na Sekretarieti yenye usiri mkubwa na uaminifu mkubwa mchezo huo usingewezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, hata kama tungeitapata hiyo barua kabla hatujawasilisha taarifa kwa Mheshimiwa Spika, isingemwondoa kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye lawama. Ni barua hiyo hiyo ambayo ilinukuliwa na Gazeti la Rai la tarehe 12/04/2007, inatamka nanukuu: "Kama unavyofahamu yapo maneno mengi sana yanayosemwa kuhusu uwezo wa kampuni tajwa kuagiza *Gas turbines* kama alivyopewa Mkataba wa TANESCO baada ya kushinda zabuni." Yameandikwa pia katika Gazeti la *This Day* la jana. Barua hiyo ambayo aliisaini yeye mwenyewe kuthibitisha kwamba alifahamu kuwa Richmond haikuwa na uwezo wa kifedha wa kuagiza *gas turbines*, ajabu ni kwa nini aliendelea kukaa kimya kwa kuachia maamuzi ya kuahirisha Mkataba huo baada ya kuuvunja ili kulisaidia Taifa kuokoa fedha za walipa kodi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu amedai hakutendewa haki kwa kutoitwa na Kamati Tuele. Hii si Kamati ya kwanza kumhusisha Waziri Mkuu. Mara ya kwanza ilikuwa kwenye suala la Mheshimiwa Malima na Ndugu Mengi ambapo Waziri Mkuu alidaiwa kuwatuhumu Wabunge kwa kupokea rushwa. Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilipotaka Waziri Mkuu aitwe kwenye Kamati hiyo ya Bunge ulitumia busara zako na kuishauri Kamati hiyo kutomwita kutokana na nafasi nyeti aliyonayo Waziri Mkuu katika uongozi wa taifa, Waziri Mkuu hakulalamika. Kwa busara hiyo hiyo Kamati Teule haikutaka kumwita kwa kuwa ilikuwa na ushahidi

unaojitosheleza. Naomba Waziri Mkuu na Wabunge wengine waisome taarifa ya Kamati Teule na viambatisho vyake kwa makini kuanzia mwanzo mpaka mwisho na Kamati tuele tumegundua kuwa Waziri Mkuu hajasoma taarifa hiyo kwa makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la nne. Katika sura ya sita ya Taarifa uk. 125 – 144, Kamati imeeleza bayana kuwa wamiliki na Richmond ni akina nani. Hakuna hata sehemu mmoja tuliyemtaja Waziri Mkuu anamiliki Richmond. Richmond ni Kampuni ambayo sisi wajumbe ambao ulituteua kwenye Kamati hii na ningependa kulisema kwa faida ya Watanzania wote waelewe na watazamaji wanaotuangalia sasa hivi kwamba ni kampuni inayohusika na *Printing*. Ni *Printer*, kwa Tanzania hii unaweza kuifananisha na *Masumin*. Sisi hatujasema *Richmond* inamhusu Waziri Mkuu wala hatujasema *Richmond* inahusu viongozi wengine. Kwa hiyo, tunaomba Wabunge wote na viongozi wote someni taarifa hiyo, inajitosheleza kwa maelezo yote mtaelewa. Ningeomba Idara yako ya Hansard isambaze viambatisho vyote ili Wabunge wote waweze kuelewa ukweli ambao tumeupata kwa kuchunguza jambo hili ambalo tumemtanguliza Mwenyezi Mungu. Narudia kumtaka Waziri Mkuu kufuta kauli yake ya asubuhi au athibitishe, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Selelii umesema maneno mengi sana lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika mchango wake nae pia alisema mengi tu. Sasa tunapodai kwa mujibu wa Kanuni kauli ifutwe ni lazima tuwe mahususi kwamba ni ipi. Ama sivyo itakuwa sasa hatuelewi na ingekuwa vizuri tu ukatamka hilo ambalo unaona kwamba si sahihi ili tuendelee baada ya hapo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Subiri kwanza msiwe na haraka.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kufafanua. Kauli ya kwanza ambayo tunapenda Mheshimiwa Waziri Mkuu aifute ni ile ya kusema tumesema uongo na kumsingizia. Ukichukua hata *hansard* ambayo amezungumza leo asubuhi, maeneo hayo amesema uongo na taarifa yetu hii ni ya uongo na ni jambo la kumsingizia. Jambo la pili ambalo tunataka Waziri Mkuu athibitishe ni yale magazeti ya Udaku ambayo tumeyatumia kwenye taarifa yetu ambayo alisema kwamba taarifa yetu imejaa magazeti mengi ya Udaku. Kwa hiyo, na hilo tunapenda athibitishe kuweza kutuambia kwamba ni magazeti gani ambayo ya Udaku. Jambo la tatu ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu athibitishe ni lile ambalo amesema hatukumtendea haki kwa sababu hatakuunganisha ushahidi wake aliokupa wewe kwenye taarifa yetu, wakati sisi tumekupa taarifa yetu tarehe 31/12/2007 na wewe umetupa barua aliyotoa ushahidi tarehe 28/01/2008. Ni hayo tu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani hapa naliondoa hili suala la magazeti ya Udaku kwa sababu haliihusu Kamati moja kwa moja. Maneno haya si ya msingi sana na kuhusu barua pia ni suala la *fact.* Nadhani la msingi ni kwamba matamshi ya Waziri Mkuu kwamba Kamati Teule imesema uongo na kumsingizia. Hilo ndilo la kutaka ufafanuzi. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nijibu hoja ya Mheshimiwa Selelii. Mimi nilifikiri nimeanza mjadala, mambo haya kwa kweli ni sehemu ya mjadala. Suala lile la uongo na kunisingizia, kusingizia nadhani libaki, uongo niliokuwa namsumbua Mheshimiwa Selelii ambalo amelisema sasa hivi, kuna mstari kwenye Kitabu chenu mnasema, "Kampuni ya Richmond ni ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na swahiba wake Rostam Aziz." Hiyo ndiyo sentensi ambayo nimeiona na kwa maoni yangu siyo sahihi. Kama hiyo sentensi haipo na ina maana nyingine basi naweza kuiondoa lakini maana yangu ilikuwa hiyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ufafanuzi huo, nadhani wametupa mwanya hapo. Tusitangulize huo mjadala kwa maana ya kutafuta utaratibu, nadhani cha msingi hapa tuendelee na utaratibu tuliopanga kama ni uongo utajulikana tu. Nyinyi ni wengi hapa, mmeomba watu 44 kuongea, kama kuna la ukweli na uongo yatagundulika humo humo na haizuii wakati wowote Mbunge yeyote akibaini kati ya haya kuweza kusimama kuhusu utaratibu. Nitamruhusu na tutaendelea kwenda mbele. Naona tusigande hapa tukibishania jambo moja ambapo tuna michango ambayo naitazamia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge 44.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika! Naomba unipe mwongozo wako kutokana na tafsiri za kikatiba na vilevile kutona na yaliyojiri leo asubuhi.

Leo Mheshimiwa Waziri Mkuu alijiuzulu kwa kuomba kujiuzulu; na kwa kuwa Bunge letu tukufu pamoja na mambo mengine linaongozwa na Katiba na Katiba inapozungumzia suala la Waziri Mkuu haizungumzii kuomba kujiuzuru bali inazungumzia *state* ya Waziri Mkuu kujiuzuru. Naomba kusoma hiki kipengele...!

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, kaa tu. Bado hujaitazama Katiba vizuri! Katiba haisemi Waziri Mkuu akitangaza kusudio la kujiuzuru mambo fulani yanaendelea, lazima ajiuzuru na kujiuzuru ni pamoja na Mheshimiwa Rais kukubali kujiuzuru kwake ndiyo kunakuwa kumekamilika. Hadi dakika hii Waheshimiwa Wabunge ninapozungumza nanyi Mheshimiwa Rais hajaniambia kama amekubali au amekataa kujiuzuru kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tunaendelea kumtambua Mheshimiwa Waziri Mkuu hadi hapo nitakapopata taarifa vinginevyo. (*Makofi*)

Naomba Waheshimiwa tuendelee na wachangiaji wangu ni wengi sana nawataja ili mjiandae wanne kwanza. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Abdurkarim Ismail Shah, amejiondoa sasa hamjanipa. Kwa hiyo Mheshimiwa Shah ameondoka nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ndiyo atafuatia na baada ya hapo atafuatia Mheshimiwa Maulida Komu na Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka. Namwita sasa Mheshimiwa Anne Ndessamburo.

**MHE. ANNE. K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kuwa msemaji wa kwanza lakini mtaniwia radhi kidogo nitakohoa. Naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kutoka kwenye moyo wangu kwa Kamati Teule tuliyoiomba sisi wenyewe

na ukaiunda wewe kwa kufuata taratibu na Kanuni za Bunge hili kwa kutuletea taarifa ambayo naomba niiunge mkono asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mbunge ni mchaguliwa au ni mwakilishi wa wananchi, sisi wote tulikaa hapa ndani ni Tanzania ikijumlisha Tanzania Visiwani na Bara. Wananchi wa Tanzania wanatutegemea kuliko tunavyofikiri sisi wenyewe na wanategemea tuwatendee haki lakini naomba nizungumze ukweli kabisa hata kama ukweli huo uta-*cost* ndiyo kazi ya siasa. Wenzetu watendaji wa Serikali wametutia aibu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimetumia muda wangu mwingi sana kusoma hivi vitabu, yote waliyozungumza kwenye taarifa ya Kamati Teule yana vithibitisho. Kuanzia Waziri Karamagi, Waziri Msabaha, Waziri Mkuu pamoja na Mwanasheria Mkuu, hakuna kitu ambacho hakina kithibitisho. Nitavitoa vichache hapa, kwa sababu nina wasiwasi kuna wengine hawajakipitia kitabu hiki. Mimi nimekwenda *Hansard* kwa sababu nipo *serious*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumnukuu Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alipokuwa Pemba juzi tarehe 3 mwezi huu. Alikiri mwenyewe kwamba kuna viongozi wasio waadilifu, wametuponza. Naomba kwa ruhusa yako ninukuu maneno machache aliyosema. Alisema hivi: “*Imani ya wananchi kwa viongozi inaanza kupungua kutokana na ukosefu wa uadilifu na uaminifu hali ambayo inahitaji kushughulikiwa haraka kabla haijawa mbaya.*” Mwisho wa kunukuu. Hili ni gazeto la Habari Leo na ni gazeti la Serikali si gazeti la Udaku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rais alikwishaona matatizo haya tuliyonayo hapa, mimi nilisimama siku moja hapa nikauliza swali la Richmond kwa sababu nilikuwa ninajua hiki kitu kipo. Saa hiyo hiyo niliandikiwa barua na kuitwa, ”njoo, usiseme hili neno hapa ndani”. Kwa nini? Mtoto ukimwambia acha unamtuma, basi mimi ndiyo nilianza kazi, nilienda *TANESCO* nikachukua *documents* zangu, nilihangaika kila kitu nikachukua. Mimi niligundua mapema kwamba si mchezo msafi; na yule aliyeniandikia barua naomba nimsihi asirudie kuwaandikia barua Wabunge. (*Makofi*)

Wabunge tunapozungumza mambo ya nchi, taifa, yanayogusa wananchi tuachwe tuseme. Mimi ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, kazi yangu ni kuishauri Serikali na kuisimamia. Hivi mnataka nimwachie Zitto Kabwe? *No!* Mimi mwenyewe nitaisimamia Serikali yangu ili iendelee kutawala. Inapokosea niikosoe ili iendelee kuwa madarakani, siwezi kumwachia Zitto Kabwe hata siku moja! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme ukweli kitabu hiki wapewe Wabunge wote. Ukiangalia barua zilizokuwa zinatoka kwa Waziri Msabaha, zinakwenda kwa Waziri Mkuu nyingine sijui kwa Waziri Karamagi, utagundua kuwa wenzetu walikuwa wanatuchezea. Wakati mwingine Mawaziri wanakaidi hata amri au matamko yanayotoka kwenye Baraza la Mawaziri linaloongozwa na Mheshimiwa Rais. Baraza la Mawaziri linasema *Songas*, kesho yake Waziri anaandika hapana ni *Richmond*. Sasa hapo mtu anasema ameonewa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siwezi kupitia vilelezo vyote, vyote viko hapa. Mimi sikulala jana si kwamba nakohoa, sijalala! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwenye hiki kitabu kuna barua pia za Waziri Mkuu, kuna barua zinatoka kwa Mheshimiwa Msabaha anasema; "Jamani kama nilivyoagizwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu..." Zipo hapa na tena nimeziwekea alama. "Kwa Katibu wa Waziri, Nishati na Madini Bungeni Dodoma". "Ununuzi wa mitambo mipya" sijui nini! "Tafadhali rejea Dokezo Sabili la tarehe 10/06/2006 la Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Ibrahim Msabaha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu ununuzi wa mitambo mipya wa Megawati 100 Ubungo. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameagiza ...." Mambo yapo hapa! Sasa Waheshimiwa Wabunge hamjasoma kwamba Mheshimiwa Karamagi anahusika, ni kweli na Mheshimiwa Msabaha anahusika, ni kweli, na wote ni marafiki zangu hawa! Lakini linapofika jambo la nchi sina urafiki na mtu hata angekuwa ni John Malecela! *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa unaweza ukakosa pa kulala leo! (*Kicheko*)

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, tukubaliane kabisa wananchi wameanza kupoteza imani na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kama alivyosema Rais. Wananchi wameanza kupoteza imani na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, tunazomewa kwamba hatufanyi kazi tuliyotumwa. Tunaomba tuwahakikishie wananchi kuanzia leo kazi ni moja tu, tukimaliza hili tutaleta la *TICS.* Yote tutaondoa na kusafisha Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi lakini kwamba tukiache Chama cha Mapinduzi kife au Serikali ya CCM iharibike kwa sababu ya kumpendelea mtu hilo sitafanya. Mkono wangu wa kulia utakibeba Chama cha Mapinduzi na Serikali ya CCM, mkono wa kushoto marafiki zangu nitawakosoa ili Serikali iendelee kuwa safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni rafiki yangu, Mheshimiwa Msabaha ni rafiki yangu, Mheshimiwa Karamagi tuligombana kwa sababu ya *Richmond* hii hii, kwa hiyo, hatuna urafiki kabisa! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndugu zangu naomba niseme kwamba tusipoteze muda, viongozi tunawakosea wananchi wetu. Sasa hivi Mtanzania amebebeshwa mzigo mkubwa sana wa bei ya umeme na *Richmond* na huu mkataba mbovu kuliko yote wa *Richmond*. Mkataba huu kwanza Baraza la Mawaziri lilisema uwe wa mwaka mmoja ukapindishwa ukawa wa miaka miwili. Miezi sita baada ya kuingia Mkataba mabwawa yakajaa na Mtera ikajaa kufurika, kwa hiyo, sasa ikawa hakuna haja ya hii mikataba tena kuendelea na wa *Richmond* ambaye dada yake ni *Dowans*. Sasa wako wamekwishafunga mitambo yao wanatudai sasa kila siku! Naomba ninukuu kitabu hiki: "kwa mujibu wa mkataba Richmond Development Company inalipwa dola za kimarekani 121,811 sawa na shilingi za Tanzania 152,264,000 kwa siku kama gharama za kudumu za uwezo wa mitambo yao (capacity charge). Fedha hizi zinalipwa kila siku bila kujali kama *Richmond* imezalisha umeme au la". Anayelipa ni *TANESCO* na *TANESCO* anapolipa lazima hizi fedha azipeleke kwa nani kwa mlaji ambaye ni mwananchi maskini halafu nyie

mnatuambia *TANESCO* ndiye ambaye anapandisha umeme. Sio *TANESCO* ni wenzetu hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika watu ambao walikataa kata kata Muswada wa Karamagi, nilisimama mimi. Nikamwambia Karamagi, hata utuweke siku nne, huo Muswada hatuutaki. Nilitaka nione kwanza, nani ameifikisha *TANESCO ICU*, ni wenzetu! Sasa kama *TANESCO* inalipa kwa siku fedha kiasi hiki, kwa siku lazima amlipe Dowans hizi fedha maana yake ni biashara hii! Yeye atazipeleka wapi? Lazima ampelekee mtumiaji wa umeme akachukue kwake. Kwa hiyo, mliowaumiza ndugu zetu ni nyinyi mliouchezea huu mkataba. Ni nyinyi mmewaumiza wananchi. Hatuwezi Serikali ya CCM kukubali! Hatuwezi Serikali ya CCM kukubali! Kwa hiyo, naomba niunge mkono mapema maamuzi na mapendekezo yote ambayo wenzetu walitoa. Yale mapendekezo waliyotoa ni mapendekezo sahihi. Mtu akiona ameshindwa kutumikia wananchi; akiona ameshindwa kabisa kuwa mwaminifu, akae kando, tuendelee na waadilifu kama Rais alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati namalizia, naomba nikwambie kitu kimoja. Huku duniani kuna viongozi wa aina mbili: Kuna viongozi ambao wakifa, wamekufa! Kuna viongozi wakifa, wanaendelea kuishi daima! Sijui mnanielewa? Hebu tuwe viongozi ambao tukifa tutaendelea kuishi daima kwa mazuri ambayo tumewatendea wananchi. Tutaendelea kuishi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niipokee hii taarifa vizuri na niseme kwamba hii taarifa ni nzuri kwa sababu moja kubwa, ina vithibitisho. Na naomba Waheshimiwa Wabunge wapatiwe hivi vitabu. Mimi nimevifuata mwenyewe kwa sababu nilitaka kufanya kazi yenye uhakika. Nawasihi Wabunge wapewe, wapitie ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho. Hakuna gazeti la Udaku, kuna vithibitisho vya mkataba mbovu na wenzetu wameiingiza nchi kwenye hasara kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii na niwapongeze tena na niwatie moyo na niwaambie wenzangu *aluta continua*, tuisafishe Serikali ya CCM. Asante sana! *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu na kwa sababu ya muda, nitachangia kwa yale ambayo yananigusa mimi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza Bunge lako Tukufu na wananchi wote Tanzania watambue kwamba nilihamishiwa Wizara ya Nishati na Madini mwezi Oktoba, 2006 wakati mkataba wa *Richmond* ulikuwa na uhai wa miezi sita tayari. Mimi sikuhusika katik…. *(Makofi/Kelele/Miguno)*

Mheshimiwa Spika, naomba unilinde!

**SPIKA:** Utulivu jamani! Waheshimiwa utulivu, utulivu! Tumpe nafasi yake ya kujieleza.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mimi sikuhusika. Kama kuna vielelezo ndani ya kabrasha ambalo lilikuwa linaelezwa ambapo kuna barua yangu ama kuandaa mkataba ama kuongoza mkataba kwa njia yoyote, vingetoka. Lakini hilo haliniondolei wajibu kwamba nilikuwa Waziri katika Serikali hii katika *collective responsibility* wakati maamuzi haya yanatokea.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nataka niwarudishe nyuma mwezi wa Oktoba. Nilipoingia Wizara hii hali ya umeme ilikuwaje katika nchi yetu? Umeme wetu ambao kiasi kikubwa unatokana na mabwawa *(hydro)* ulikuwa umeshuka kutoka *megawatt* 560 mpaka *megawatt* 120. Hiyo ndiyo hali tuliyokuwa nayo. Gridi ya Taifa ingeweza kukatika wakati wowote na nchi ikawa gizani. Hayo ndiyo mazingira ambayo wanaohusika wote katika kufanya maamuzi walikuwa wanafanya kazi nayo. Katika nchi nyingine hiyo ungeiita kama *state of emergency* ku-*declare state of emergency*! Mimi mwenyewe nilipoingia pale kila siku ilikuwa nnapokea ripoti ya mabwawa yote Tanzania na wakati mwingine kuweza kusema hapa zima na hapa washa ili kuinusuru nchi yetu katika giza. Sasa hapa suala la kwanza linalonigusa, wanasema kwamba mimi nilishiriki kukataa ama kushinikiza *TANESCO* isifute mkataba wa Richmond Oktoba, 2006.

Mheshimiwa Spika, mimi nilipoingia Wizarani pale pamoja na Katibu Mkuu, kazi yetu kubwa ya kwanza ilikuwa kuona namna gani ya kufuta huu mkataba. Lakini si kufuta mkataba kwamba tusiongezewe gharama, ni kufuta mkataba ili tuweze kumpata mwingine kwa sababu wakati ule umeme ulikuwa haupo, tulikuwa tunahitaji umeme. Ilikuwa ni namna gani ya kufuta mkataba na kumpata mwingine…… *(Miguno)*

Mheshimiwa Spika, naomba unilinde!

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Kwa hiyo, tukaanza tarehe 5 – haya mambo ya Dowans yamekuja baadaye. Tarehe 5 Oktoba, Katibu Mkuu kamwandikia Mwanasheria Mkuu ili kutupa vigezo ambavyo tunaweza kutumia katika kuvunja huo mkataba na ili kutomwezesha *Richmond* kwenda mahakamani kwa sababu ya kuvunja mkataba. Tulipewa ushauri ambao tuliwaagiza *TANESCO* waangalie vipengele gani wanaweza kutumia katika kufanikisha huo mchakato ambao ulikuwa umeanzishwa na Katibu Mkuu.

Barua ambayo imeambatanishwa ya tarehe 27 Oktoba, 2006, ilikuwa ni jibu la hiyo barua na ukiisoma vizuri, iliandikwa na Meneja Mkuu wa *TANESCO* wakati ule alikuwa ni…. Jina lake silikumbuki, wale wa *Net Group Solution*. Pamoja na mengine alitaja katika kifungu kwamba mkataba huu tuondokane nao kwa sababu Richmond hajaweza kutoa umeme unaotakikana ambao ingebidi upatikane *on commercial operating date*, haijaandikwa ndani ya mkataba, imeachwa *blank*. Akaomba, na mwenyewe ameweka kwenye barua ambayo iko bayana kwamba pengine tunaweza kutumia zile *minutes* ambazo tulikuwa tunakaa tunazungumza, labda ziwe ndiyo vithibitisho vya kuweza kusema ameshindwa.

Lakini hapa Waheshimiwa Wabunge, tunao wanasheria na Kamati Teule ilikuwa na Mwansheria tena aliyebobea, kama *minutes* za vikao hazikuandikwa ndani ya mkataba kwamba zitakuwa viambatanisho kwenye mkataba, ukizitumia mahakamani, hazitakubalika. Palikuwepo na vipengele vingine ambavyo tungeweza kuvitumia, kampuni haijaorodheshwa hapa, haiko Marekani. Lakini, mkisoma vizuri hiyo ripoti na mimi nimeisoma vizuri, utaona kwamba kufuatilia hivyo vipengele, *Richmond* angeweza kwenda mahakamani, akatucheleweshа hata kama tungempata mkandarasi mwingine ambaye tulikuwa tunamhitaji sana wakati anazalisha *megawatts* 120 za nchi nzima, siyo kitu kidogo. Angeweza kuweka *Court Injunction* za kutukataza, tungeweza kupoteza muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichukua njia mbili: Moja, tuache mkataba ufe wenyewe ukifika mwezi wa pili na kwa kutumia njia hiyo, wengine ambao tunaweza kuwapata ambao wanaweza kutunusuru kwenye hili tunaweza tukawa-*engage* bila kupata *Court Injunction* ya *Richmond.* Na kwa njia hiyo ndiyo sababu tuliweza kumpata *Alstom*, kuweza kumchukua Mwanza ku-*stabilize* gridi ya taifa bila kuwa na matatizo na *Richmond* kwa sababu hatukuwagusa. Tulijua tukiwagusa, atatuchukua kortini. Tukivunja mkataba, anaweza kudai fidia ama akaweka *injunction* ya kutucheleweshа, na sisi wakati ule hatukuwa Mungu, tusingeweza kujua kwamba Januari mvua itanyesha. Tulikuwa tunajitayarisha kwa muda mrefu na wataalamu walikuwa wanasema inaweza ikachukua takriban miaka mitatu hivi ili mabwawa yetu yaweze kurejea hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili Kamati Teule kutenda haki kwa maamuzi waliyosema, kwanza, wangeonyesha wapi Karamagi nimeshinikiza? Maana yake wote huko katika vielelezo wameeleza: “Wakati Waziri anashinikiza ama anaandika barua au anaita Menejimenti kuiagiza au Bodi, kwa hili sikuona mahala popote zaidi ya ile kwa Kiingereza wanaita *circumstantial* na nafikiri kuhukumu mtu kwa hili wakati hujajirudisha kwenye mazingira wakati ule tulipokuwa tunafanya maamuzi, mimi kwangu naona kwamba haikuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sina muda mrefu, kuna hoja nyingine ambayo ilikuwa inaelekeza kwamba mimi mwenyewe kama Waziri niliwekea shinikizo *TANESCO* ili i-*assign* (kuhuisha) huo mkataba wa *Richmond* kwa *Dowans*.

Tunachokizungumzia hapa kama nilivyokwisha sema, ni mwezi wa Novemba na mwezi wa Desemba na sijui kama kwenye viambatanisho wameonyesha *level* ya maji ilivyokuwa Mtera ambayo tayari ilikuwa chini kabisa. Ilikuwa ama mashine zile karibu zlikuwa zinavuta upepo. Kwa hiyo, tulikuwa tumeanza kuzima mashine Mtera na Kidatu kusudi tuzitumie tu gridi ya taifa ambayo ilikuwa inakatika katika mara kwa mara inapozima, kwa sababu bila ya Mtera na Kidatu, gridi ya taifa ingezimika, nchi nzima ingekuwa kwenye giza na hata ukiwa na hizi za *Songas*, *IPTL*, *Aggreko*, haziwezi kuwasha gridi ya taifa. Kwa hiyo, ilibidi hayo maji yaende chini, ilikuwa hatari kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa safarini Canada. Nilipopata kwenye *E-Mail* yangu kwamba *Richmond* wana mpango wa ku-*assign* ile *contract* kwa *Dowans*,

kwanza nilifurahi kwamba sasa tuna *opportunity* labda ya kuweza kumpata mtu anayeweza. Lakini nikaona tusije tukaingia kwenye tatizo kama la *Richmond* kwa sababu tulikuwa tumekwishagundua kuwa *Richmond* ni kama tapeli. Hivyo mpaka nafika pale, tulikuwa tumekwishagundua kwamba *Richmond* ni tapeli. Kwa hiyo, ili tusiingie tatizo kama la *Richmond*, mimi kama Waziri wa Nishati na Madini nikaona nisingoje hiyo ziara ambayo sijui ilikuwa inachukua muda gani, nikaona nimpigie simu Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO*, Mheshimiwa Kazaura, nikamwambia: "chonde chonde nimesikia taarifa hizi, chonde chonde msi-*assign* huo mkataba bila kufanya yafuatayo:-….." Yameorodheshwa kwenye *pag*e 90 na kweli Kamati imenifanyia haki kwa sababu imeeleza vilevile kama nilivyotahadharisha. Lakini pamoja na tahadhari hizo, hawakunipongeza kwamba angalau na mimi nilianza kuchukua *due diligence*. Wakanituhumu kwamba hiyo tahadhari ni kama shinikizo kwa *TANESCO*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Baniani mbaya, kiatu chake dawa! Akifanya jambo zuri, jamani mpongezeni! Najua inaweza kuwa ni jambo jema siku hizi *style* nzuri unapotaja jina la Karamagi, inaonekana vizuri. Labda ilionekana kama hii ripoti kama haikutaja Karamagi, haitanoga. Lakini kwa hili…! *(Kicheko/Miguno)*

**SPIKA:** Lakini Mheshimiwa Waziri, kama tapeli anapendekeza mkataba wake uende kwa mwingine, hushituki?! *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wewe ni Mwanasheria, kama tapeli, amekuingiza katika mkataba ambao uko halali, ukiukatisha kinyume na mkataba huo, unampa uwezekano wa yeye kunufaika, akakuchukua mahakamani, ukamlipa pesa ya bure!

**SPIKA:** Aah! Endelea tu Mheshimiwa!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Labda ile isingenoga, kwa hiyo, ikaonekana niunganishwe kwenye hiyo ripoti. Lakini kweli nilichokuwa nafanya kwa moyo wangu, nikatumia *profession* yangu ya *Finance* kwamba wafanye *due diligence physically*. Mheshimiwa Spika, naomba zile *minutes* nilizotumia uniongezee kidogo. Wafanye *physical due deligence*, amezitaja. Nikizitaja, ziko ukurasa wa 90, utazisoma, *physical*.

Lakini wakati ule *management* ya *TANESCO* na yenyewe ikatoa kwamba zaidi ya *physical*, watafanya *financial due diligence* ambayo ni sawa! Sasa jamani, naomba kwa hili mtupongeze kwamba angalau kwa mara ya kwanza tulifanya mambo ambayo yako sahihi.

Mheshimiwa Spika, sasa nimalizie, kwa sababu kengele ya pili karibu ilie, niku-*quote* tu wakati unaomba msamaha ambapo ulisema kwamba, "tafsiri ya mambo ukiyatumia vibaya ama kwa ubinafsi, yana matatizo". Na mimi naona hapa mtiririko wa mambo yalivyokuwa ni sawa, lakini inapokuja *conclusion,* inakuja tafsiri nyingine. Kwa hiyo, naona hiyo hainifanyii haki.

La pili, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge walio wengi, wamenitumia *messages* mbalimbali za kunipa faraja. Lakini wa mwisho ambaye amenifurahisha, ambalo niliseme, amesema, “Yesu hakutenda dhambi, lakini alitolewa kafara”, ukienda kwenye vitabu vya dini, ili kusudi atusaidie sisi wengine duniani tusiwe na dhambi. Kwa hiyo, kwa kuzingatia hilo na kwa kuzingatia dhana ya uwajibikaji na maslahi ya taifa na heshima ya Chama changu, leo asubuhi, nimemwandikia Mheshimiwa Rais barua ya kujiuzulu wadhifa wangu, bado nangoja maamuzi yake kwa sababu ndiye aliyeniteua. Lakini hiyo barua nimekwishamtumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naona tujadili hii ripoti lakini tujadili siyo kwa ushabiki. Aliyekosea azungumzwe, lakini yale mengine ambayo yananifaa, tuyaweke pembeni. Naomba kuwasilisha! *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Spika anaruhusu ushabiki kwa nchi ya Tanzania. Ushabiki uwepo tu lakini tushabikie maslahi ya nchi yetu! *(Makofi)*

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii jioni hii nichangie kuhusu hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba uniruhusu kunukuu Katiba ya Nchi yetu, Ibara ya 8(1). Katiba ya nchi inasema: “Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii.” Kisha inasema: “wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii”. Hapo hapo inasema; “lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi”. Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri au mbaya sote tuliomo kwenye ukumbi huu tumeletwa kwa ridhaa ya wananchi. Tumekuja hapa, wananchi waliopo ndani ya nchi hii wakiwa na imani kubwa na sisi na wakiwa na mapenzi makubwa na sisi kwamba tunakuja hapa tutetee maslahi yao ya maisha yao ndani ya nchi yao. Na uzuri, utaratibu wa nchi yetu, hata Mawaziri wanaounda Serikali, wanatoka miongoni mwa Wabunge - wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mwananchi anayepanga foleni ya kupiga kura kuanzia saa kumi na moja asubuhi, akaingia pale akakamata karatasi kwa imani kubwa, akaweka tiki akasema Maulidah Anna Komu ananifaa, halafu nikaja hapa nikamgeuza kachumbari, nikamtafuna, nikamweka hoi, ninasikitika sana! Kuna Waziri mmoja aliulizwa hapa juzi au jana alisema kinachopandisha bei vitu ni mazao ya chakula!

Umeme, mafuta ya dizeli au petroli ndiyo vitu vinavyochangia kupandisha bei ya vitu katika nchi hii kila siku asubuhi. Nilisimama siku moja nikasema hivi kweli tumeshindwa? Kupandisha bei kila siku, kupandisha mafuta ni kuwawekea mzigo wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila ya umeme hakuna afya! Bila ya umeme ni kuongeza umaskini. Na hivyo vyote viko mgongoni mwa Mtanzania. Bila ya umeme watoto wetu

hawana maabara. Tutapata wapi madaktari ? Bila ya umeme nikiumwa leo nikisema nakwenda hospitali, vitu vya kunichunguza afya yangu, nikitolewa damu, nikiambiwa nipimwe hiki, kile, lazima kuwe na umeme. Nikienda kujifungua, nikishindwa kujifungua mwenyewe, nipasuliwe tumbo, mtoto atolewe ili nchi hii tuzaliane, basi lazima kutumike umeme!

Mheshimiwa Spika, leo kweli watoke watu ambao wananchi wa Tanzania wamewaamini, wakawaleta kwenye Ukumbi mtakatifu kama huu, Rais wa nchi hii akawaamini, akawateua wakawa Mawaziri waunde Serikali wamsaidie, halafu wasimsaidie? Mheshimiwa Rais alikuja hapa kwenye ukumbi ule mwingine akatuambia kwamba tushikane tuunde Serikali iliyo nzuri, tuwatumikie wananchi. Leo hao ndio wanaochukua kitabu chekundu – na walivyoweza kuki-*cover* wenzetu, nawapa hongera kwa *cover* nyekundu kuonyesha kwamba hapa kuna hatari. *(Makofi)*

**SPIKA:** Si lazima *cover* nyekundu ionyeshe hatari! *(Kicheko)*

**MHE. MAULIDAH ANNAH KOMU:** Ni damu! Mheshimiwa Spika, samahani! Tulipitisha bajeti hapa Juni na ilikuwa Bajeti ya 2006/2007. Wakati tunapitisha bajeti hapa, kumbe wenzetu wanacheza ngoma yao wanayoijua wenyewe. Bajeti hii tulipoweka kwenye vikao vya Kamati, tukapitisha, tulirudishwa tena kuambiwa tena tupunguze kwamba fungu lililopo kwa ajili ya bajeti halitoshi. Tukakaa pamoja na Wizara husika na Kamati tukachekecha vichwa, tupunguze fungu lipi kwa sababu kila fungu tunaloliona tupunguze, tunaona lina umuhimu. Lakini hakuna budi, lazima tupunguze!

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ya Maendeleo ya Jamii, kioo cha kumletea Mtanzania maisha bora, tulipewa shilingi bilioni saba na vitu kidogo huko juu. Tukaja hapa tukasikitika sana, lakini hakuna budi. Leo kweli, kweli, kweli kuna thamani ya kitu kinaingia kwenye mkataba cha karibu shilingi bilioni 200 mbali na alizokuwa anazizungumza Mama Malecela hapa! Ukichanganya bajeti ya Wizara ya Elimu, ukachukua na bajeti ya Maendeleo ya Jamii, basi bado kuna marupurupu yanabaki.

Halafu tunakuja hapa, tunazungumza vitu vya ajabu, tunaacha kuwapa mkono wenzetu waliokesha wakafanya kazi tuliyowatuma sisi wenyewe hapa Bungeni waende wakaifanye watuletee ukweli? Hakuna kitu kizuri kama kukubali kwa aliyetumwa kwamba mimi kweli ni mkosa. Mimi nampa hongera kubwa sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nasema hongera! Ndio mwanamme anatakiwa awe hivyo! Kakubali na kasikitishwa kwa sababu yeye anaamini kwamba wananchi wa kwake ndio waliomchagua kwa kura zote, kwa imani kubwa wakamleta hapa. Kwa hiyo, kama anahusika, kama hahusiki, lakini kama yale aliyoyafanya wakati ule aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Bwana Ali Hassan Mwinyi, akawajibika, na yeye akasema na mimi leo basi nawajibika.

Mheshimiwa Spika, akatimiza kifungu kile kile cha *Public Procurement Act* cha 44(5) ambacho pia naomba uniruhusu nikisome lakini kimeandikwa kwa Kiingereza, kinasema:-

*Where an Accounting Officer or Chief Executive Officer satisfies the authority that he is under the provision of any written law subject to the control or direction of any person, board, committee or other board and that it was such control or direction of such other person, board, committee or other board which cause the failure to comply with the provision of sub-section (1),* (hiyo ilipita huko nyuma) *then such other person or every member of such board, committee or other board shall also be accountable for such failure to comply".* Katimiza wajibu wake! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nasema hivi, Mheshimiwa Waziri Mkuu katimiza wajibu, tunamsubiri Rais aseme. Iwe mifano kwa wengine wote ambao Rais atawaona kwamba wanafaa miongoni mwetu kuwaambia nyinyi njooni sasa tuunde Serikali, kama alivyosema Mama Malecela, hatutaki masihara hapa ndani sasa. Mimi ndio maana wakati wote nanyamaza.

Ninanyamaza kwa sababu naona kulikuwa na mchezo wa pata potea hapa! Kama kweli tunasema wakati umefika wa kufanya kazi tumwondolee mzigo Mtanzania aliyetuleta hapa, sasa wakati umefika, jogoo anawika, tufanye kazi! Na kama wewe unajiona kwamba huwezi kufanya kazi, tafadhali muone Mungu, msikilize Mungu, mwamini Mungu, rudi kwa Mungu, angalia vitabu vya Mungu vinasemaje na mtu mbadhirifu, mnafiki, mwongo, mwizi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dini zote zinazungumza kitu hicho hicho kimoja. Hakuna dini ambayo inakwambia nenda kawadhulumu watu, haipo! Dini zote zinasema wafanyie watu kilicho kizuri, fungu lako liko kwangu. Sasa tunapokuja hapa tunapofanya vizuri, siyo fungu liko kwa Mungu tu, liko na kwa wananchi waliokuleta hapa. Tangu juzi Watanzania wamekaa masikio wazi. Wameona ya Zitto yamepita, wanasikia tena kuna *Richmond*, wanasikia tena sijui kuna *T…*, sijui wanasikia kuna nini…Hivi ni nini? Kwa nini hatusemi na mioyo yetu? Unapokamata Msahafu au Biblia ukala yamini, kwa nini hutaki kuwa mkweli kwa wanandamu na kwa Mungu? Sasa ndugu zangu wakati umefika kuwa *rubber stamp,* basi! *(Makofi)*

Tunajadili jambo hapa ndani kwa sababu ya kumuonea huruma Mtanzania aliyetuleta hapa, wote tuwe na kauli moja. Hakuna Mwana-Chadema wala Mwana-CCM, Mwana-*CUF* wala mwana-nani kwenye ukumbi huu! Wote sisi tumeletwa na wao tuwatetee! Na tunapofika kwenye ukumbi huu, hawa si wenzetu. Hawa tuwaambie lazima wananchi wapate haki yao! Siyo kusema, "aah, maana yake mimi Mwana-CCM, kama nikisema hivyo, kwa hiyo, itakuwaje sasa!" Itakuwaje?

Umeambiwa uje hapa kwa sababu uwe fulani au uwe fulani? Uje hapa kwa ajili ya mzigo wa maisha ya Mtanzania anayehangaika asubuhi na jioni! Leo mabibi zetu wanauawa kwa sababu ya macho mekundu, wanaitwa wachawi! Kama wangepelekewa umeme kule na wao wakatumia umeme, wasingeuawa! Wale wasingekuwa na macho mekundu kwa sababu ya kutumia kuni na mavi ya ng'ombe.

Tunakuja hapa, maana yake mbona wanauawa wengi, wameuliwa wangapi basi, basi tufanyeje? Tufanyeje? Tuwapatie maisha mazuri, kama watauawa tena! Tufanye

kazi iliyotuleta hapa, kama watauana tena wale! Umaskini na shida ndiyo inawafikisha watu pahala kama pale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia na kumi na ishirini na thelathini! Na namwambia Mwenyekiti na Kamati yake, *aluta continua!* Mungu yupo pamoja na wao kwa sababu wao wamekwenda kukaa usiku na mchana kutetea haki ya mwananchi na kumwambia Mtanzania hii ndiyo hali ilivyo kwenye nchi yako, uamuzi wako, twendeni 2010! Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Maulidah, namwita sasa Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Masuala ya Afrika Mashariki na baada ya hapo ajiandae Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, aah, ni Mheshimiwa Dr. Slaa, karatasi imekaa vibaya, Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa kwanza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya leo iliyopo mbele yetu. Nianze kwa kulipongeza Bunge lako Tukufu kwa kutimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, kikao kilichopita cha Bunge lako Tukufu, Bunge hili liliamua kuunda Kamati Teule ya kuchunguza suala hili la *RICHMOND* na wewe ulituongoza kwa utaratibu mzuri na hatimaye kutuundia Kamati nzuri na kwa maana hiyo kwa niaba ya wananchi wa Simanjiro, naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza Kamati hiyo Teule kwa kazi nzuri waliyoifanya *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaimani sana na Kamati hiyo tangu ulipoitamka. Kwanza kwa sababu wengi wao ni wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara ya Bunge ambayo mimi ni mmoja wa Wajumbe katika Kamati hiyo na nilikuwa naujua msimamo wao tangu mwanzo katika kusimamia mambo ya msingi yenye maslahi kwa Taifa letu lakini zaidi inaongozwa na Mwanasheria aliyebobea na mtu ambaye ana nchi yake ndani ya moyo wake na mzalendo wa kuigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku ya leo ni siku ya historia kubwa kwa Bunge letu na nchi yetu. Kwa nini nasema hivi? Ni kwa sababu kwa mara ya kwanza baada ya hoja kuwasilishwa ndani ya Bunge lako, sasa wamefika Mawaziri Wawili kabla sijazungumza waliokwishaeleza nia yao ya kuheshimu dhamana za umma walizopewa wakiwajibika kutokana na utendaji mbovu uliokuwepo na ambao umetokea kipindi ambacho wao wako kwenye Ofisi hizo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza kipekee Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Edward Lowassa, Kaka yangu, kwa mambo makubwa mawili, Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mheshimiwa Edward N. Lowassa katika miaka miwili aliyokuwa Waziri Mkuu wa nchi hii, kuna mambo ya msingi uliyoyasimamia ambayo hakuna yeyote mwenye akili timamu atakayekataa kwamba kasi yako ya kusimamia mambo hayo haikuwa ya kiwango stahiki. Huu ni ukweli Kaka yangu na utaendelea kubaki na utaandikwa katika historia. Umeweka tofali lako na sasa unawajibika kwa nafasi uliyokuwa nayo kutokana na

yaliyotokea katika kipindi cha uongozi wako na mimi nakuunga mkono kwa uamuzi huo wa kijasiri ulioufanya.

Mheshimiwa Spika, katika mwongozo wa Chama cha Mapinduzi, tulifundishwa na Baba wa Taifa kwamba kujikosoa na kukosoana ni silaha ya mapinduzi na ukiendelea mbele anasema kukiri upungufu si dalili ya kushindwa bali ni ishara ya kujiimarisha. Ninapenda Bunge lako Tukufu lichukue mistari hiyo ya mwongozo wa Chama cha Mapinduzi kama changamoto na kuchukua jambo lililotokea sasa kama changamoto ya kuanza kutoka hapa katika suala zima la kujitakasa na kuijengea imani Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa umma.

Mheshimiwa Spika, ukweli unabaki hivi, katika Ilani ya Uchaguzi, Kifungu cha 135 kinasema, lakini kuongoza ni kuonesha njia, kwa ruhusa yako naomba kunukuu, kinasema hivi:-

*"Lakini kuongoza ni kuonyesha njia, ni kuwa mfano bora, ni kuwafanya wananchi waridhike kuona uko mbele na wao wanafuata, wanakufuata si kwa sababu wanakuogopa kwa sababu wanakuamini, na imani ya kweli haipatikani kwa kauli tu bali kwa vitendo vyako, mwelekeo wako na kwa kuwajali wananchi"*

Mheshimiwa Spika, imani ya kiongozi kwa umma inapotiliwa mashaka, kama una busara, unachukua uamuzi kama aliouchukua Mheshimiwa Lowassa leo *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Kifungu cha 110(f), kinabainisha wazi kwamba au kinaelekeza wazi kwamba tuwapuuze na kuwadharau viongozi wanaotoa na kupokea rushwa. Hakuna mashaka kwamba unapokuwa na Kampuni hewa kama ya *Richmond* ambapo Serikali inakubali kuingia mkataba na Kampuni hewa na wakati huohuo Serikali yetu ikiwa na Wanasheria waliobobea, wanaotoka katika Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo kinachoheshimika Duniani, hakuna mashaka kwamba walifanya hivyo kwa bahati mbaya, waliingiza nchi kwenye mikataba ya aina hiyo kwa sababu ya kuwepo kwa dalili zote za kupokea rushwa na kunufaika kwa maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama kada wa Chama cha Mapinduzi, niliyekula kiapo, ninataka kuliomba Bunge lako lisiishie kwa Mawaziri tu, Waziri Mkuu amekubali kuachia ngazi, Waziri Karamagi amekubali kuachia ngazi, Mheshimiwa Msabaha aachie ngazi na Mwanasheria Mkuu awajibike.

Mheshimiwa Spika, Wakurugenzi wa *PCCB,* narudia *PCCB*, kwa sababu hivi karibuni katika kashfa iliyolikumba Taifa letu ya fedha za *BOT,* Rais wetu mpendwa ambaye kwa dhati anaipenda nchi hii, kwa dhati amedhamiria kupambana na wabadhilifu na wezi wa mali ya umma, aliamua kumwondoa aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu, Ndugu Balali na akaelekeza vyombo vya Ulinzi na Usalama vifanye kazi ya kuwashughulikia wale wote wenye makosa ya jinai, lakini miongoni mwa hao ni pamoja

na taasisi ya *PCCB*, taasisi ambayo ilichukua nafasi ya kui-*clear Richmond* na *Dowans* mbele ya Watanzania wakati inajua wazi hii ni Kampuni hewa, iwajibike.

Wenzetu wa *PPRA* waliiambia Serikali taratibu za Sheria za Manunuzi zifuatwe lakini hazikufuatwa, ushindani haukuwepo lakini *PCCB* walisema ushindani wa zabuni ulikuwepo. Taratibu za manunuzi hazikuzingatia Kanuni kwa sababu Kanuni zinasema ni siku 45 kutangaza *tender* ya aina hiyo, wao walitangaza kwa siku kumi (10), hiyo peke yake ilitosha kutilia mashaka maamuzi hayo. Baraza la Mawaziri linapofanya maamuzi mchana na kuielekeza Wizara kwamba ifuate utaratibu huu, Wizara inageuka tena na kufanya mambo mengine tofauti na hayo, mimi nasema *PCCB* haikutenda haki, ilipaswa kubainisha kishawishi kilichowafanya wale waweze kufikia kwenye hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba wale wote waliotajwa katika ripoti ya Kamati Teule wawajibike. Kimsingi Watanzania wana matarajio machache sana, wanatarajio moja tu kwa Bunge lako kwamba tunatakiwa tuchukue hatua kwa wale ambao wameonyesha kutokuwa na uzalendo katika mikataba ambayo nchi yetu imeingia.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wangu kwamba, mikataba yoyote itakayokuwa na harufu ya rushwa, ikivunjwa hata ikiwa ya Kimataifa, Dunia itatuheshimu sana. Kama unaingia kwenye mkataba ambao hauna manufaa kwa nchi unakuwa na manufaa kwa watu wachache, kwanza inabainisha wazi kwamba kuna jambo lililokuwepo hapo katikati. Ninapenda kulishauri Bunge lako na Serikali yetu kwamba iendelee kuchunguza mikataba ya makampuni kama hayo ya *Richmond* na *Dowans* ili kujua kwanza ni akina nani wenye makampuni hayo maana lipo tatizo hapa.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa kwamba *RICHMOND* ni Kampuni ya Marekani, wenzetu wamekwenda Marekani kwenye usajili wameambiwa hakuna kampuni inayoitwa *RICHMOND.* Tumeangalia kwenye kumbukumbu zetu hakuna, sasa hapa lazima kuna watu wamejificha.

Mheshimwa Spika, juzi kwenye ripoti ya *BOT*, katika fedha za *EPA*, kuna makampuni 22 hewa, iko hatari sana kama Serikali inaweza kuingia mikataba na makampuni hewa kana kwamba sisi hatuna wataalamu!

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana ichunguzwe fedha hizi tunazowalipa hawa watu zinapoingia kwenye akaunti zao hizo zinahamia akaunti zipi tena? Maana upo uwezekano tukakuta baadaye makampuni haya kama *Richmond* au *Dowans* na wenzake ni makampuni yetu sisi viongozi wakubwa au watendaji Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ninapenda sana kulishauri Bunge lako Tukufu liishauri Serikali iendelee kuchunguza ili kujua wamiliki wa makampuni hayo ni akina nani kwa sababu bado ni kitendawili.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge waliotangulia, katika suala hili ambalo lina sura ya ufisadi, Wabunge wote tunapaswa kuungana bila

kuangalia umevaa shati la kijani au umevaa shati la bluu, unatoka chama kipi, katika hili wote lazima tuungane pamoja kuwataka wale wanaohusika wawajibike.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha jambo moja kwamba wakati mwingine, wakati wananchi wanaandamana kuunga mkono Ripoti ya Dr. Mwakyembe na Kamati yake, hapa ndani watu wanaweza wakafanya kama mzaha mzaha. Jamani shilingi bilioni 200/- zinatosha kukomboa Majimbo yetu kwa kujenga Shule za Sekondari na Zahanati. Nchi inapoingia katika *crisis* hiyo siyo suala la kuchekacheka wakati unaeleza mambo haya, huu ni ufisadi na mimi inanisikitisha sana Mheshimiwa Spika, haitatosha kuwawajibisha tu, twende mbele zaidi, tuwafilisi, tuwafilisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ukiniachisha Ubunge au Uwaziri au Ukatibu Mkuu lakini ukakuta nina hisa na makampuni kama hayo ambayo nitapata bilioni 150/- kama *capacity charge* kwa siku, hivi huo Ubunge na huo Uwaziri una maana gani zaidi kwangu kama mimi ni mbinafsi? Ni vizuri tukaangalia na akaunti za hawa wahusika ili nchi yetu iweze kuwa salama huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema mimi binafsi namuunga mkono Mheshimiwa Rais katika harakati alizozianzisha na kuelekeza kwamba ni vizuri kutenganisha kofia hizi, kama umeamua kwenda kwenye biashara nenda kwenye biashara, kama umeamua kuja kwenye siasa, karibu watumikie wananchi, maana hapa kuna *conflict of interest!*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema tuwachunguze, hebu twendeni *IPTL*, hebu tuwachunguze *SONGAS*, *AGGREKO*, tuwachunguze na wale wengine ambao tumewapa majenereta haya, ni akina nani? Utaona kwamba waliomo humo ndani hutashangaa ama ni ndugu wa baadhi ya wakubwa au wakubwa wenyewe wamo humo humo. Unaambiwa kampuni ni ya Ujerumani, Marekani lakini wamiliki wa kampuni hizo ni weusi kuliko Ole-Sendeka, ni wa hapa hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba tufanye hivyo na wakibainika kama ni wa CCM na wakiwa na kadi za CCM, ninashauri Chama cha Mapinduzi kisimamie ilani yake na Katiba yake, iwanyang'anye uanachama wa CCM, waende kuendelea na ulanguzi wao huko waliko vinginevyo tutakuwa tunajidaganya hapa, tutakuwa tunajidanganya kuendelea kuwalea watu ambao ni mafisadi na huku wanapeperusha bendera ya Taifa, wanapeperusha bendera yenye hadhi kama *CCM* na bendera yetu kama mnavyojua inasema wanyonge njooni kwangu ufalme wa duniani ni wenu lakini wenyewe wanaendelea kupata utakaso huo na saluti za majeshi yetu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tulikula kiapo na wewe ulikula kiapo ulipoingia CCM kwamba rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa lakini hatupokei rushwa wala hatutoi rushwa? Nilipoomba mkataba wa *Richmond* na *Dowans* uletwe kwenye Kamati ya Uwekezaji, niliahidiwa mara tatu na Mheshimiwa Karamagi lakini hakuuleta. Kwenye Bunge lililopita akasema alitoa ushirikiano kwa Kamati ya Bunge, kwa kiwango cha kutosha, nilimheshimu tu kama Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, nilitaka

kumpiga Kanuni ile ya 50 kabla haijabadilika hii ya 63 kutaka aliombe Bunge lako radhi kwa sababu tulimtaka alete mkataba huo kwenye Kamati hakutaka.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kushauri Bunge lipitishe Azimio kabisa, kwamba mikataba hii isiwe siri ya Mawaziri na Makatibu Wakuu wao, iletwe kwenye Bunge hili, tusipofanya hivyo na sisi tutakuwa ni sehemu ya ufisadi huo. Leteni mikataba hii tuione kama mmejiongezea muda kama ile ya *TICS* ambayo ilipewa miaka 10 baadaye ikaongezewa tena miaka mingine 15 kabla mkataba wa mwanzo haujaisha, tuitazame halafu tujue na hiyo *TICS* ni ya akina nani na baada ya hapo tuwawajibishe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, wakati huo ajiandae Mheshimiwa George Simbachawene.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia.

*(Hapa kulikuwa na minong'ono mingi ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Utulivu.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hadi leo nikiwa hai na pia kumshukuru kwa yote.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nitoe pongezi za dhati kwa Kamati, Wanakamati, Mwenyekiti wa Kamati na Bunge lako Tukufu. Napenda hasa nimpongeze, Ndugu yangu, Mheshimiwa Harrison Mwakyembe kwa sababu yeye na mimi tunafahamiana kutokana na huko tulikotoka kihistoria kwenye mambo ya taaluma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Napenda nimpongeze kwa jinsi alivyowasilisha kwa staili yake na alipomaliza baada ya saa moja na nusu akamfanya kila mtu aamini yote, nampongeza sana. Nampongeza pia kwa kuonyesha kwamba yeye pamoja na Kamati walikuwa na dhamira ya kufanya kazi hii na kufanikisha dhamira nzuri waliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue nafasi hii kwa namna ya pekee kabisa, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Amekuwa Waziri Mkuu wangu kwa miaka yote hii miwili na hasa kwa kitendo chake cha leo cha kutangaza kwamba anakusudia kujiuzulu.

Mheshimiwa Spika, kule nyumbani kwetu sisi, wewe Mnyamwezi sisi Wazaramo, mtu kama huyu tunamwita Kilongola yaani anayeonyesha njia. Kwa hiyo, nampongeza

sana Mheshimiwa Lowassa kwa kuwa Kilongola, kaonyesha njia na sisi wengine tutafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikusidii kujibu hoja kwa hoja, hakuna haja, hapa lipo jambo muhimu sana linajadiliwa na kama yapo mambo au upungufu katika taarifa ile, hayo ni mambo ya kushauriana namna ya kuyaboresha ili iwe nzuri zaidi kwa ajili ya kumbukumbu za Bunge na kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isipokuwa nataka nitoe mfano mmoja tu. Kwa mfano, jana wakati Mheshimiwa Mwakyembe, anawasilisha hoja yake, alinishtua kidogo alipotaja kwamba *Richmond* walilipwa dola milioni 10/-. Kama ni kweli basi kulikuwa na tatizo kwa sababu nakumbuka suala hili lilizuiwa wakati mimi nikiwa Waziri wa Nisahati na Madini mpaka naondoka. Sasa kama walilipwa wakati ule, itakuwa ni suala la kutafuta ilikuwaje kwa sababu najua lilizuiwa na Waziri wa Fedha alilizuia na mpaka viongozi wa juu walilizuia. Natoa mfano wa vitu ambavyo vinaweza pengine vikaboreshwa pengine wakati wa kupitia upya.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni kama ile hali yenyewe ya dharura na ufanyaji maamuzi nyakati za dharura, huko mbele ya safari tunafanyaje, mfumo wa mawasiliano unakuwaje, kwa sababu mambo mengine ni mambo ya kimfumo unayakuta katika Serikali!

Mheshimiwa Spika, wewe ni mzoefu wa mambo haya na jinsi yanavyokwenda ni hivyo hivyo, dokezo linatoka kwa Waziri linakwenda kwa Waziri Mkuu, linatoka kwa Waziri Mkuu linakwenda kwa Rais, tuchukue mfano, au pengine ni mambo yanayokwenda kwenye Kamati Maalumu au *Cabinet*, yakitoka kule yanakwenda kupata idhini na kadhalika. Sasa haya ni mambo ambayo nadhani yanaweza yakatizamwa ni namna gani tunaweza kuboresha mfumo wetu kwa kuzingatia Sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo linaweza kuboreshwa hata katika *presentation* hii, ukurasa 147 mpaka 148. Hii naitoa kwa ajili ya Kamati, ukiisoma unaweza ukadhani ndiyo mambo yale niliyokuwa ninasema mimi Bangusilo, kuna maneno ambayo yanazungumzia habari ya uwajibikaji wa Waziri na Katibu Mkuu, ilivyoandikwa inakuwa kama vile hawa wanawajibika kama kafara na mimi nadhani pengine maana yenyewe siyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, nipo tayari kushirikiana na Kamati katika maeneo ambayo nadhani yakipitiwa tena yanaweza yakaboreshwa vizuri zaidi kwa ajili ya kumbukumbu sahihi na kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia katika mtiririko huu yapo mambo ambayo nayaita kama ni ya kiufundi. Nadhani Mheshimiwa Dr. Mwakyembe kwa *background* ambayo nimeisema kwamba wote tumetokea huko, atakubaliana nami kwamba wakati mwingine unapofanya uchunguzi ama utafiti ukiondoka na dhana fulani …

**MBUNGE FULANI:** *Hypothesis!*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Siyo *hypothesis,* nasema ukiondoka na kwa mfano uamuzi…

**MBUNGE FULANI:** *A pre-inquest.*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Ndiyo, *a pre-inquest of idea* siyo *hypothesis,* unaweza ukaenda nayo ukajikuta wewe tayari umeshapata jibu sasa unatafuta njia ya kuhalalisha. Ninachosema ni kitu ambacho unapaswa uwe kidogo mwangalifu na ukiipitia taarifa hii wakati mwingine inatoa sura hiyo ambayo pengine siyo sahihi kabisa, hiyo ni moja.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, pale mahali ambapo alikuwa anatoa nadhani kwenye maagizo sijui kama iko humu kwenye taarifa maana sikupitia neno kwa neno, jana wakati anatoa taarifa hapa alimpa pole ndugu yetu yule Kubenea lakini jinsi alivyosema ikaonekana kama vile kuna *connection* baina ya *RICHMOND* na matatizo aliyopata ndugu yetu Kubenea, ndiyo!

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuulizwa mahali kwamba wewe umewahi kuhojiwa juu ya ndugu yetu Kubenea? Nikawaambia hili ni jambo la kushangaza lakini ninachosema yote hii inatokana na jinsi ule mtiririko ulivyo unaweza ukatoa taswira ambayo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, unapokuwa unafanya utafiti kama huu wenye mambo ya kisiasa, ni rahisi sana kuweza kuteleza namna hiyo na mimi nadhani ni vizuri tukashauriana namna ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kama ni suala la kwenda hoja kwa hoja, tutapata muda huo baadaye wa kuweza kushauriana kwa maana ya maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Lakini mimi kwa kweli nia yangu ya kusimama hapa, kwanza, ni kusema kwamba mimi si mwoga, ni muadilifu, sipendi rushwa na ni mchapa kazi na nashirikiana na watu. Katika Bunge hili nadhani ni mashahidi, Wasukuma na Wanyamwezi humu ndani wanaweza wakakubali kwamba mimi ndiye Babu yao humu ndani, sina tatizo na ushirikiano na watu. Kwa hiyo, nilitaka hili niliseme tu kwa sababu wakati mwingine inawezekana ni tabia imejionyesha…

**SPIKA:** Kwa umbile lako Mheshimiwa Waziri, inaonyesha kabisa wewe ni Mnyamwezi au Msukuma. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu wakati mwingine yanaposemwa haya maneno kama alivyosema ndugu yangu Mwakyembe jana, ya ubabe na kiburi, sasa kiburi naogopa sana. Sisi Waislamu tunasema kiburi ni sifa ya Mwenyezi Mungu siyo ya binadamu, naogopa. Sasa inawezekana wameyapata haya huko chini huko kwa watendaji, ni bahati

mbaya lakini nataka niseme kwamba kwa kweli si sifa nzuri kwa binadamu ya ubabe, kiburi, jeuri na kadhalika, Mwenyezi Mungu atupishilie mbali.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba nimesimama kusema yale ambayo yameonekana. Kwanza, nakubali kuchukua *collective responsibility* pia *responsibility* ya wale ambao wako chini yangu kwa yale ambayo wameyafanya ambavyo siyo sawasawa kama Kamati ilivyoona. Kwa maana hiyo, siogopi kuwajibika na najua kuwajibika katika *context* yetu sisi labda katika suala kama hili lakini katika mambo mengine inaweza kuwa kidogo kila siku Waziri mmoja yupo katika matata kwa sababu ya hali yetu ya maisha ilivyokuwa duni. Lakini kimsingi mimi ni mtu ninayeamini katika uwajibikaji, katika utawala bora na katika mambo yale ambayo yanadumisha na kuendeleza wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, niliona niseme kutokana na hali jinsi ilivyo kwa sababu siasa ni suala la imani ya watu. Kuwa kiongozi wa kisiasa ni imani ya watu na jinsi watu wanavyoona ni lazima kiongozi wa kisiasa uwe na imani ya wale unaowaongoza na *perception* yao ni jinsi wanavyokutazama na lazima pia iwe ni sawasawa. Sasa inawezekana kabisa hata wakikutazama kwamba uko hivyo lakini hauko hivyo inatosha kwako kusema kwamba kwa kweli ni vizuri mtu ukae kando ili shughuli za Kitaifa ziendelee na wewe uweze kuchangia kwa njia nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimesimama hapa kwa kweli kwa heshima ya nchi yangu, Chama changu, Jimbo langu na kwa heshima kwa kweli ya Bunge langu, ni muhimu sana hii taasisi, kusema hivi, ndiyo maana nikamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye ni Kilongola kwamba alionyesha njia, asubuhi ya leo nimekwenda kumwona Mheshimiwa Rais na kumweleza dhamira yangu ya kujiuzulu na kama ilivyo kawaida kama ambavyo wewe mwenyewe ulivyosema wote sisi tunangojea amri yake.

Mheshimiwa Spika, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa heshima kubwa aliyonipa, namshukuru mke wangu na familia yangu kwa ujumla kwa msaada wote ambao wamenipa, nawashukuru wananchi wa Kibaha na hasa Kibaha Vijijini, Jimboni kwangu, wanakijiji wenzagu wa Kijiji cha Soga na wale Wasukuma na Wanyamwezi mnakaribishwa, mfundishwe namna ya kula kwa nazi, nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote. Hapo Mheshimiwa Rais atakapokubali, naamini nitapata fursa tena nyingine ya kukaa pamoja nanyi na kuwashughulikia Wasukuma ipasavyo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, unataka kututoa kafara sisi Wasukuma sasa. Tunaendelea Waheshimiwa, ahsante sana, nimeguswa sana na namna ulivyowasilisha hotuba yako, ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali, nimwombe Mwenyezi Mungu atujalie tunapojadili hoja hii iwe kwa kutimiza mapenzi yake na atupe mwanga ili tuyaseme kwa unyoofu na ukweli.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba nianze kwa kunukuu, Ibara ya 52(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inasema:-

*"Waziri Mkuu atakuwa na madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hadi siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano".*

Ibara ya 53(2) inasema:-

*"Serikali ya Jamhuri ya muungano chini ya mamlaka ya Rais, ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera ya Serikali kwa ujumla na Mawaziri"*

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo sehemu ambayo nataka iangaliwe kwa makini. Mawaziri chini ya uongozi wa Waziri Mkuu watawajibika kwa pamoja Bungeni kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba niache kwanza itulie. Lakini niseme mambo mawili, la kwanza, naomba sisi Wabunge tutambue kwamba wote tuna maslahi ya Taifa hili na wote tumetoka kwenye Majimbo kwa kuchaguliwa na wananchi ili kuisimamia Serikali, sio kuilinda na kuishauri kwa mujibu wa Katiba na kama tulivyoapa. Kama hivyo ndiyo, wote tuna nia hiyo moja, yanapokuwepo maslahi ya Taifa, tusimame kidete bila kujali huyu ni wa Chama gani, itikadi yake ni ipi au shati lake ni rangi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba niseme kwamba tangu tumeanza kupata taarifa za ufisadi, nchi yetu iko kwenye wakati mgumu sana. Haya yote yanakwenda katika mtiririko ule ule na kama ilivyotajwa kwenye ripoti hii kuna *element* za ufisadi katika taarifa hii. Kama hatutakuwa makini, tukajadili kwa umakini, nchi yetu inakwenda pabaya, wananchi wetu ndiyo wanaumia na sisi wenyewe ndiyo tutakaoumia. Baada ya kusema hayo, naomba nianze mjadala wangu.

Mheshimiwa Spika, nimetaja Ibara hiyo ya Katiba kwa sababu nataka kujenga msingi wa mchango wangu. Baada ya kusoma ripoti hii, Mheshimiwa Waziri Mkuu, rafiki yangu, ndugu yangu na jirani yangu, naomba niseme kwamba nimepitia vifungu vyote hivi, bahati nzuri sijaona mahali ambapo Waziri Mkuu, anatuhumiwa kama yeye kwa maana ya rushwa au yeye amehusika kwa maana ya kupokea chochote. Hili ni suala zito sana kwa sababu kilichotokea hapa na kinachoelezwa hapa na namshukuru amechukua hatua ya kutoa nia ya kujiuzulu, ni uwajibikaji. Baada ya mchakato wote huu kuonyesha Taifa limeingia gharama kubwa sana na kwamba mambo mengi katika mchakato wote wa *Richmond* hayakuenda vizuri na msimamiaji mkuu ni Waziri Mkuu, hakuna wa kuwajibika isipokuwa Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali pamoja na Mawaziri wake kama ilivyo katika Ibara ya 52 na 53.

Mheshimiwa Spika, ninasema haya kwa sababu Baraza la Mawaziri na tuna taarifa zote, kwa wale waliosoma kitabu hicho kwa sababu muda hautoshi siwezi kuyasoma, Waraka Na.2 wa 2006 ambao ulitolewa na Mheshimiwa Waziri akiwasilisha taarifa ya Baraza la Mawaziri, umeeleza kabisa taarifa ya Baraza la Mawaziri au maelekezo ya Baraza la Mawaziri yamevunjwa na hakuna kosa kubwa kama kuvunja

maagizo ya Baraza la Mawaziri. Ndiyo maana katika Katiba yetu tumeambiwa maagizo au maelezo au majadiliano ya Baraza la Mawaziri hayawezi kuhojiwa katika Mahakama yoyote, ni maamuzi mazito kweli kweli, inapofikia yanavunjwa, Waziri Mkuu hasemi kitu, Mawaziri hawasemi kitu, hoja ya *RICHMOND* imejadiliwa ndani ya Bunge hili, hatuwezi kuelewa kwamba Waziri Mkuu na Mawaziri wake leo wanajitetea ndani ya Bunge hili na Taifa limegharamia kwa mabilioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kuendelea kujadili hoja hii nisipoteze muda wangu, naomba nihitimishe, ushahidi ni mwingi mno wa jinsi haya mambo yalivyotokea tangu dakika ya kwanza *Richmond* ilionekana ni kampuni tapeli, imechukua *business card* ambayo inaonyesha tu kwamba kuna makubaliano ya mawasiliano kati yake na *Pratt and Whitney*, hii Mawaziri wanajua, Waziri Mkuu anajua, *TANESCO* wanajua, Mheshimiwa Waziri Karamagi, Mheshimiwa Waziri Msabaha wakati ule wanajua, Makatibu wake wanajua na nina hakika Baraza la Mawaziri linajua.

Mheshimiwa Spika, kampuni imetumia majina yanayobadilika kila wakati kama kinyonga, huwezi kusema Baraza la Mawaziri hawakujua. Haiwezekani uende kule *BRELA* chombo cha Serikali Kampuni hii haikusajiliwa wakati inapewa tenda ya Taifa, tena hata kabla ya 2004 haikusajiliwa wala kwa jina la *Richmond Development Tanzania Limited* wala kwa jina lake la America licha ya kwamba hata kule America haijulikani. Hii Kama kampuni hii haijulikani na Baraza la Mawaziri halikujua basi hawakufanya kazi yao vizuri na ni sababu nzito leo ndani ya Bunge hili kusema basi Waziri Mkuu na Baraza lake lote wanatakiwa kujiuzulu kwa uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokujua, kutofuatilia, kutokuangalia, ni uzembe ambao hauwezi kusamehewa hasa baada ya kuliingizia Taifa mabilioni ya hasara na tunaendelea kulipa kwa sababu mkataba ule unasema hela tunayolipa kwa kampuni ya *Richmond* na leo *Dowans*, tutaendelea kulipa kwa miaka miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani naeleweka na sitaki kuliendeleza jambo hilo niendelee kwenye jambo langu la pili.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu pongezi. Kuna watu katika Taifa hili wanatakiwa wapewe zawadi. Mimi nimesoma kwa umakini sana vielelezo vilivyopo hapa, kazi iliyofanywa na *TANESCO* na hasa yule mama anaitwa Wandiba, ni kazi ya kupongezwa na kwa kuwa ni sisi wanasiasa tumeipeleka *TANESCO ICU*, inatakiwa kupongezwa. Kuna barua nyingi hapa wameionya Serikali, wameandika kwa *Richmond* kwamba mmevunja mkataba na imeelezwa, sina muda wa kuonyesha hapa nikitakiwa nitatoa kila aina ya barua ziko nyingi, wamewaambia kabisa kwamba hapa mmekwenda kinyume. Kwanza walipewa taarifa kwamba jibuni haya hawakujibu. Wakapelekewa taarifa ya pili, tunawapelekea *notice*, hawakujibu, barua zote hizi zinapelekwa kwenye Wizara zote. Kwa taarifa, barua hii wameipeleka kwa Makatibu wa Wizara zile zote husika ikiwemo na Ofisi ya Waziri Mkuu. Ukiniambia kwamba barua hii imepelekwa kwa Katibu Mkuu, Waziri hajui basi

kuna tatizo katika Wizara zetu, uwajibikaji ni Mawaziri na Makatibu Wakuu na wale wote wanaotakiwa kuamua katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inanipa tatizo kidogo, rafiki yangu Karamagi ni rafiki yangu kweli, mimi nadhani rafiki yangu Karamagi, akubali tu na awe mnyofu na mkweli kwa sababu Mheshimiwa Karamagi kwanza barua hizi zote alikuwa anapelekewa na licha ya kupelekewa, anatoa taarifa ndani ya Bunge hili kuonyesha kwamba hatukuweza sisi kama Serikali, kama Taifa kuvunja mkataba wa *Richmond* kwa sababu tunaogopa kupelekwa Mahakamani. Jambo hili si kweli kwa sababu barua za *TANESCO* zimeonyesha vipengele wazi kabisa ni wapi tunaweza kuvunja mkataba kwa sababu wao watu wa *Richmond* ndio wamekiuka mkataba! Cha kushangaza Mheshimiwa Karamagi kama tulivyosikia huko nyuma wakati ule Buzwagi akiwa nje ya nchi Calgary analeta barua, naomba nifanye *reference* kwa sababu ni muhimu. Mheshimiwa Waziri anafanya *reference* ya kupiga simu kwa Balozi siku ya tarehe 28 Novemba, Balozi Kazaura ndiye anasema nimepigiwa simu, sasa Balozi Kazaura anaposema nimepigiwa simu wakati huo Mheshimiwa Waziri katika Wizara yake ameshapata taarifa ya *TANESCO* inayotoa *notice* ya mwisho kwamba hamkutimiza wajibu wenu na kuna *notice of default*, inawezekanaje akiwa Calgary kupiga simu kuelekeza kwamba *Dowans* au *Richmond* wanataka kuhamisha mkataba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa sio tu kuna suala la uzembe nadhani lazima tuwe wanyofu, kuna wingu la rushwa. Haiwezekani kutoka Calgary, maelfu ya kilomita, unapiga simu, wataalam na washauri wako wote wapo Dar es Salaam halafu useme hakuna chochote kilichofanyika pale? Hapa nadhani ni lazima kama walivyosema wenzangu, uchunguzi wa kina unatikiwa kufanyika ili kujua kilichojiri kati ya watu wetu na *Richmond* na *Dowans* na hili hatuwezi kuliachia kwa sababu *document* hizi ziko *very clear*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kitu ambacho kimenishtua sana kwenye kitabu hiki cha ushahidi, kwa bahati mbaya tuna *document* ambayo haina *signature* ya Mtanzania ambaye anasema, naomba ninukuu. Imeandikwa kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchunguzi wa *Richmond* kwa maana hiyo Kamati hii ya kwetu, anasema:-

*“Ninayekuandikia, ni mtumishi wa umma hivyo naomba sana nisitaje jina langu wala ofisi kwa sababu za kiusalama…”*

Mheshimiwa Spika, huko mwanzo sitaki kusoma itanichukulia muda lakini naomba nisome *paragraph* inayohusika.

*“Pili, yupo ofisa mmoja mfanyakazi wa BRELA aliyesaidia kutoa mafaili hayo na kupokea nyaraka mpya za kuficha huo ufisadi. Yeye amepewa nyumba ya Serikali eneo la Chang’ombe na imekarabatiwa kwa gharama za Serikali na kuwekewa fenicha za kisasa”*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili, ni lazima Bunge hili lione ni muhimu kwa sababu watu wetu wanaogopa. Kuna Sheria inayosema kuna siri kwamba ndani ya Serikali

mtumishi atakayetoa siri atachukuliwa hatua na watu wetu kwa sababu hii wamekuwa waoga, hawatoi siri.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa ajili ya yale mambo mengine ya *BOT* nimepokea barua nyingi na watu hawataki kujionyesha, wale wengine wanaweza kunyofoa lakini ina *signature*, sasa huyu anasema yamefichwa. Katika rekodi hii, unaona kabisa kwamba kampuni ya *Richmond* ilipoandikishwa mara ya mwanzo inawezekana walioandikisha wala sio hawa tunaoambiwa ndiyo hawa na katika *Hansard* ndivyo pia inavyoelekea kuonekana. Kama hivyo ndivyo, kuna tatizo zito zaidi ambalo linatakiwa uchunguzi wa kina. Tunamuomba Mheshimiwa Rais aelekeza uchunguzi sio wa Kamati, Kamati imeshafanya kazi yake, wa kipolisi wa kuchunguza nani ni *Richmond* kule *BRELA* na ni nani anayehusika kuandikisha na kwa nini hizi *documents* haziko. Kama inawezekana ku-*trace* mahali pengine popote na hawa watu kuhojiwa ili waweze kupatikana, suala la nyumba na nini, nina hakika itaweza kujitokeza katika hatua ya mwisho, suala hili hatuwezi kuliachia.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo juu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nina hakika Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atakubali tu kwa hiari yake na kwa jinsi ninavyomfahamu, ni mtu anayejua kuwajibika na kwa sababu ofisi yake ndiyo iliyokuwa inashauri kila mahali, iko kwenye Kamati, iko kwenye hatua zote, ndiyo inayonakiliwa barua zote anastahili kuwajibika.

Mheshimiwa Spika, licha ya Mheshimiwa Mwanyika, kuna mtu ambaye nimemkuta kwenye barua zote hapa, nadhani Kamati haikumsema kwa sababu sina hakika kama Kamati inajua na yale mengine ambayo mimi nayajua. Kwenye *documents* hizi, anayepelekewa nakala zote hasa hizi za kuisema *Richmond* kwamba imekiuka mkataba, ni mtu mmoja katika Ofisi ya *Attorney General, Ministry of Justices and Constitution Affairs*, anayeitwa Maria N. Kejo. Huyu ni mtu mkubwa katika Wizara, ni kiongozi, ameshiriki kwenye *process* zote kwa sababu ndiye Afisa anayehusika.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruksa yako niitumie *information* niliyopata sehemu nyingine kumhusu Maria Kejo. Kuna *Affidavit* Mahakamani ya Katibu Mkuu wa Serikali ya Tanzania katika kesi ya *IPTL* inayosema Maria ameshiriki kushinikiza kumhonga Katibu Mkuu wa Wizara. *Affidavit* iko Mahakamani, imekuwa *testified* na watu wawili, kama tunashindwa kumwamini Katibu Mkuu anaposema hivi, nadhani kuna tatizo. Nadhani huyu mtu na yeye ni lazima achukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu kwa bahati nzuri imesema kabisa kabisa kwamba kuna watu wamekataa kutoa ushirikiano walipoombwa walete nyaraka husika, naomba hawa wote, maelekezo na maazimio ya Kamati ya Bunge lako yawe kwamba hawa watu wote wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii tete ambayo kwa kweli naamini inataka umakini. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibakwe, ninaomba na mimi nichangie katika kuifanya historia ikae vizuri kwa umri wangu wa kuwepo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nina mambo kadhaa ya kuzungumzia. Leo tunafanya uamuzi wa mambo mengi na wengine ambao wamekuwa *implicated* kwenye hii ripoti wameamua kuonyesha nia yao ya kujiuzulu, ninawapongeza wote walioamua kuchukua uamuzi huo. Huo ndio uungwana na *as a matter of logic, pattern, trend* mambo yakienda namna fulani tu, unaona basi unawajibika kufanya kitu fulani. Kwa hiyo, niwapongeze sana, nianze kumpongeza Waziri Mkuu, Waziri Karamagi na Waziri Msabaha, kwa kuonyesha nia ya kujiuzulu nyadhifa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nichukue nafasi hii, kuipongeza Kamati Teule ya Bunge, iliyotuletea taarifa hii ambayo imeandaliwa kitalaam sana, imeandaliwa kisomi, lakini pia inaleta zama mpya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, juzi tulipokuwa kwenye semina, nilinukuliwa nikisema, niko tayari kufa kuliko kuiona Tanzania ijayo. Nilimaanisha nini? Nilikuwa najaribu kufikiri kwa akili yangu hii ndogo hali itakayokuwepo tutakapokuwa tumebinafsisha na kuuza vinu vya kuzalisha umeme, viwanda na mambo mengine, je, tutaweza ku-*negotiate* na nani katika bei ya bati maana hao hao ndiyo wenye vinu vya umeme, hao hao ndiyo wenye viwanda, una-*negotiate* na nani na uta-*control* vipi *price*? Ni lazima utanunua sementi kwa bei wanayotaka, lazima utanunua bati kwa bei wanayotaka. Nikawa najaribu kupiga picha hiyo ndiyo maana nikafika mahali pa kutoa *statement* ile lakini leo ninaahirisha kufa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, siku ya leo tunajenga msingi wa Tanzania inayokuja. Inaweza ikaonekana mambo yanayofanyika leo kwa kweli yanauma, ni machungu, marafiki zetu wa karibu wanapoamua kujiuzulu unaona ni kitu kama cha ajabu hivi, ndiyo maana asubuhi watu tulikuwa tuko *confused*. Lakini mimi nasema linalofanyika, ni jambo la kiungwana, ni jambo ambalo linaijenga Tanzania inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba hapa tulipofika na yanayotokea sasa, Wazungu wana msemo wanasema "*the end justifies the means*". Tumefika hapa kwa sababu tulikosea mahali fulani. Tumefika hapa kwa sababu yako mambo yaliyokuwa ya msingi huku nyuma tumeyaacha.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Arusha lilianza mimi sijazaliwa. Maana watu wengine mkituona haya maumbile ni kwa ajili Korie tu na nini ndiyo maana tuko hivi. Mimi nimezaliwa mwaka 1968, Azimio la Arusha lilikuwa mwaka 1967. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema bado natamani na kuviona vitu vilivyokuwemo katika Azimio la Arusha kwa sababu vilikuwa ni vitu vya maana sana. Vilikuwa ni vitu vya maana kwa sababu tulipoliacha Azimio la Arusha, ndiyo tumefika hapa tulipo. Hata mawazo ya Mheshimiwa Rais, kwamba sasa tufike mahali tuamue

Ubunge, Ubunge, Uwaziri, Uwaziri, biashara, biashara, hili ni Azimio la Arusha, *the context of it* ni Azimio la Arusha. Kwa hiyo, tunarudi pale tulipopotea na mimi ninashauri tufikirie hayo na turudi pale tulipotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninapenda niliseme kutoka moyoni mwangu, Watanzania tumrudie Mungu wetu, haiwezekani hali ya malalamiko, hali ya manung'uniko ya wananchi wetu tukaiachia hivi hivi. Unajua Mtanzania yule wa zamani siyo sawa na wa sasa hivi ambaye anaona TV kila kijiji. Mtanzania wa sasa ananunua redio ya shilingi 2,500 anaweza akasikiliza leo, kesho akanunua nyingine, kwa hiyo, anapata habari, anajua kinachoendelea. Kwa hiyo, kufungafunga mambo, haitatusaidia, ni bomu tunalolitengeneza wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niwapongeze waliochukua uamuzi huu kwa nia ya kutaka kuanzisha zama mpya kwa huu tu mfano wa *Richmond* lakini ipo mengine mengi, lakini utoshe tu huu na tufanye *a U*-turn twende kwenye *the right track,* tumeshaanza kuona huku hakutusaidii, tugeuke.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nasoma hii ripoti nilikuwa natafuta suala la kwanza walilokuwa wanajaribu kulitafuta hawa waliotengeneza hii ripoti Teule *Richmond* ni nini? Wamekuja na majibu kwamba hakuna kitu kinaitwa *Richmond* kinachofanya shughuli za umeme. Hii nayo unahitaji uwe *Form Four* au *Form Six* kujua? Yaani kampuni hii ipo au haipo nayo inahitaji uwe na elimu kubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia *trend of decisions* zilizofanyika, *dialogue* na mazungumzo yote kwenye makatarasi mpaka unapata *book* kama hili, linazungumzia kitu hicho hicho, unapata lingine linazungumzia kitu hicho hicho, halafu hiyo kampuni hai-*exist,* unapata maana gani? *The end justifies the means* kwamba *the whole process* ilikuwa *wrong* na waliosimamia utaratibu mzima wana makosa na wanapaswa kuwajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya zabuni haikufuatwa *completely*. Nichukue nafasi hii kupongeza uongozi wa Shirika letu la *TANESCO. TANESCO* katika kila kurasa unaofungua ambapo wame-*participate* kutoa wazo lao lilikuwa *excellent* na ni la kizalendo. Lakini lile ni shirika linakutana na viongozi, wanawapa *instruction* na maelekezo, wananyamaza. Lakini hata wanapoibuka tena siku nyingine, wakitoa *comments* zao zinakuwa safi. Kwa hiyo, mimi nasema Shirika la *TANESCO,* kwa kweli tuna kila sababu kuupongeza uongozi wa *TANESCO* kwa maana walijaribu kutetea haki ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme ni kila kitu, usicheze na kitu kinaitwa *power, the one who controls power, land, water* ndiyo anaye-*control* nchi. Kama *power* hii, kwa tunavyokwenda na kwa Muswada wa Umeme uliokuwa unaletwa, nasema ilikuwa ni moja kwa moja kwenda kuwakabidhi wageni vinu vyetu vya umeme. Huwezi ukasema *TANESCO* ita-*exist* wakati imeshachoka, iko *ICU* unamletea mshindani ambaye anakuja kuinunua yaani wangekuja hapa *in a very simple way* wangeweza kuichukua pamoja na kila kitu wangesema ama *you will be in light* ama mnakaa gizani. Ndiyo wangeweza kusema hivyo, siku moja wanaamua mnakaa gizani, siku nyingine wangesema tunawawashia umeme, mtasema nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tulikuwa tunazungumzia sementi imepanda bei kwa ajili ya mikataba hii hii, Mheshimiwa Rais, kasema sementi lazima itashuka bei, nitajitahidi. Mimi nampongeza sana Rais kwa kuwa ni mzalendo na anafanya kazi yake kwa uungwana na ni mtu wa Mungu na ni mcha Mungu. Lakini sementi imeshuka? Haikushuka! Ni kwa sababu ya *contracts* zilizopo na mfanyabiashara hana mazungumzo mengi na hana urafiki. Kwa hiyo, tutajikuta siku ya mwisho sisi nchi nzima hii imeuzwa iko mikononi mwa wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba ninasikitika na kustushwa na *integrity* ya TAKUKURU. Tulipokuwa tunatengeneza Sheria ya TAKUKURU, tuliamini kwamba inakuja kutusahihishia maeneo yenye matatizo kama haya. Lakini TAKUKURU inapokuja na taarifa kuhusu *Richmond* na kusema, naomba kunukuu taarifa, ukurasa wa 156 inasema:-

*"Matokeo ya Uchunguzi wa Kamati Teule kama ulivyoainishwa hapo juu anasema, mkataba huo wa Richmond Development Company na Dowans Holding kinyume na taarifa iliyotolewa na TAKUKURU wakati huo kwamba Taifa halikupata hasara yoyote, taarifa ya TAKUKURU ililenga kuficha ukweli hivyo ikaishia kujikanganya kwa kukiri kuwepo mapungufu lakini yasiyokuwa na athari".*

Mheshimiwa Spika, taasisi nyeti kama hiyo, ambayo kazi yake ni kutumulika sisi viongozi, huwezi kumwambia mkulima yuko kule Kibakwe ukasema unampelekea TAKUKURU badala ya ku-*deal* na mambo haya makubwa wakatuletea hapa *solution* lakini wanakuja hapa wanakisifia kitu ambacho leo kinaonekana ni cha ovyo. TAKUKURU wamepoteza *integrity* na mimi nasema kwa kweli Mkurugenzi wa TAKUKURU awajibishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunazungumzia kuhusu *Richmond* kama sehemu moja tu ambayo imefanyiwa kazi na Bunge kwa mujibu wa Katiba kwamba Bunge ndiyo lenye mamlaka ya kuishauri na kuisimamia Serikali lakini bado kuna haja Bunge likaenda mbele zaidi ya hapo na kuangalia mikataba yote ya umeme. Kwa kuwa somo lililopo mezani hapa ni suala la umeme basi mikataba yote ya umeme iangaliwe upya, ili tuone huu mzigo anaobebeshwa Mtanzania ni wa kiasi gani. Kampuni inayoonekana ni ya mfukoni leo inapokea shilingi milioni 150 kila siku iendayo kwa Mungu, ambao ni mzigo unaobebeshwa Watanzania, haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, mimi Mbunge wa Kibakwe kila siku nikikaa jukwani naulizwa, hivi kwa nini Mheshimiwa bati zinapanda bei? Naanza kujikanyaga pale. Kwa nini sementi inapanda bei? Najichanganyachanganya pale, sina majibu. Sasa naona leo pengine hii ndiyo sababu ya kupanda kwa bei ya bidhaa. Kwa kweli nataka niwahakikishie wananchi wangu wa Jimbo la Kibakwe, kwamba kwa kweli pengine sasa maelezo hayo yaliyoletwa na Kamati, inaweza ikawa ni jibu la kushuka kwa bei ya sementi na mabati ili waweze kujenga nyumba nzuri.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ya msingi ni kwamba kwa kweli mikataba yote iletwe na ifanyiwe kazi na Bunge ili tuweze kujiridhisha kwa niaba ya wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba katika hali hii, kwa kweli niunge mkono hoja kwa asilimia zote, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu.

Kabla sijaanza kuchangia, ninapenda kuwapa pole vijana wetu wa Polisi Moshi, waliounguliwa na nyumba na mpaka sasa familia 27 hawana makazi. Kwa kweli wanahitaji msaada kwa majanga hayo waliyopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nasikiliza kila mmoja anavyochangia, kwanza tumshukuru sana Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na Kamati yake, amefanyakazi nzuri sana, kwa ujasiri na bila uwoga, angekuwa mtu mwingine, ningekuwa na wasiwasi, angekuwa anaumwa lakini ameweka wazi kila kitu hata sijui tunachangia nini maana ile ripoti imemaliza kila kitu na maamuzi ya Kamati ile yakifuatwa kila kitu kiko sawa. Hongereni sana wote mliofanya kazi hii ya Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingine lazima nimpe Waziri Mkuu, kwa kuwajibika. Ameonyesha njia. Tumekuwa tukipiga kelele, jamani mtu anapofanya makosa awajibike, sasa tumejua njia ya kuwajibisha watu, lazima tuwaundie Tume. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ili nami niweze kuchangia kwanza, kwa kufikiria Sheria gani zinazotupa matatizo hasa mikataba ikawa ni siri ya Mawaziri na timu yao, *Principal Secretary* au *Permanent Secretaries;* ni kifungu gani cha Sheria kinachowapa hiyo nguvu, hata Kamati za Bunge zishindwe kuona ni nini kilicho ndani? Sisi Wabunge ambao ndiyo tunawawakilisha Wananchi wa Tanzania, hatujui wanafanya nini. Huu usiri ni lazima sasa tuukomeshe uishe. Tusingefika hapa tulipofika, kama tungekuwa tunajua yanayoendelea. Yote haya, yamekuja kwa sababu ya usiri na penye usiri kuna sababu. Hii ni hujuma kubwa; shauri la *Richmond* labda Wabunge hawajui, mimi ninajua Ofisi yao ni *Internet Cafe,* ipo nyuma ya hosteli yangu ya *Keys.* Ninawajua wote tena vizuri sana ni vijana wadogo tu. Sijui Serikali ilitoka wapi na hawa vijana; uhuni mtupu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwa ninasoma magazeti; nchi za wenzetu kama za China, wahujumu wa namna hii siyo kwamba wanajadiliwa, wananyongwa hadharani. Tunapozungumzia milioni 150 kwa siku ni kimoja tu hicho *Richmond,* tunayo makampuni manne yanayotoa umeme; sasa kila mmoja kama analipwa hivyo na huku wananchi mlo mmoja hawapati, wengine wanalalia uji wa malimao na nchi ina pesa hii jamani, lakini wanachukua wakubwa zinaisha; tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Tuna wasomi, tuna Mawakili, tuna watu waonajua Sheria vizuri sana; lakini sasa ninaanza kumwamini Mheshimiwa Rais, alipokuwa Scandinavian alisema, kule kwetu

hatuna Mawakili, akaomba Wazungu waje watusaidie kazi. Alisema Rais, akasema hawa Mawakili wetu au hawa Wanasheria wetu, hawajui kuitazama mikataba. Leo hivi tunaisifia *TANESCO* kwa kukosoa, *TANESCO* tunayoisifia aliyekuwa anajibu ni Mzungu. *(Makofi)*

Miaka 46 tuna uhuru, hatujasomesha mtu wa kusoma mkataba; kweli hatuna Mtanzania aliyesoma mpaka Rais anakwenda nje kuomba watu wa kuja kutuangalizia mikataba yetu? Hata mtoto aliyezaliwa siku tulipopata uhuru, tayari ana u-dokta. Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, amefanya kazi hii nzuri mnayoiona. Tungekuwa nao watu kumi kama yeye, haya matatizo yangekwisha. *(Makofi)*

Mimi ninakuwa na wasiwasi sana, Mheshimiwa Rais kuzungumzia kutenganisha siasa na biashara. Hata kama yeye ni maskini, akiwa Waziri atampasia ndugu yake ili ajue ninacho kitu, haitatusaidia. Siyo kwamba, ninasema matajiri ndiyo wanafaa, hapana, lakini mtu mwenye njaa mara kwa mara ana matatizo. Mtu mwenye njaa, ana matatizo sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, ameunda Tume ya Kuchunguza mambo ya *EPA*, katika Tume ile yuko *Attorney General* na yuko Mkuu wa TAKUKURU; hawa wawili wako katika kashfa hii; je, wanaweza kutuletea kitu kizuri kweli katika *EPA?* Tungemwomba Mheshimiwa Rais, kwa kuwa hawa wamekwishaonekana wana dosari waondolewe, wawekwe watu wapya, ambao wataweza kutuletea kitu kizuri kama hiki tulicholetewa hapa leo na Tume hii ya Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. Hii ni kwa sababu, tumekwishaona *Attorney General* wetu na Bwana TAKUKURU, ambaye anakuwa ni fisadi mkubwa, anafukia madhambi, anasafisha majina ya watu. Sasa ninachoona; hivi ripoti hii inaishia hapa hapa Bungeni ama tunaipeleka tena mahali pengine ichunguzwe, maana kuna watu lazima wafungwe hapa na wengine wafilisiwe mali walizonazo tufidie hawa Watanzania maskini wa watu? Hili ni dili, mjini tunasema hili ni dili. Siyo hivi hivi ni dili limefanyika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia tukasema pesa nyingi zimetumika kwa *capacity building*. Umeme ni moyo na roho ya Watanzania, leo hivi tunapandishiwa umeme kila siku, tunaambiwa ni *TANESCO* wanapandisha, siyo *TANESCO* wenzangu wamesema, lakini tunarudia kuweka mkazo, madhambi haya ndiyo yanapandisha umeme, kufidia madhambi haya tunarudi kwa Mtanzania maskini kabisa, tunamwambia afidie. Hii haiwezekani kabisa, lazima tubadilishe.

Tunataka kuanza kitu kipya na Tanzania mpya ya kuwajibika. Kiongozi yeyote, ambaye anaona ana madhambi, awajibike. Kiongozi yeyote ambaye anaonekana ana *kiburiga* chake katika makampuni haya, asije hapa ndani jamani. Tafuteni biashara nyingine, biashara za kunyonya Watanzania ni mbaya ndugu zangu, mwisho wake tutakuja kupata laana za Mungu. *(Makofi)*

Ninasema ni laana, kwa sababu tumewanyonya watu wasio na kitu. Halafu na wale wanaonyonya wana vitu vingi; hivi wanazoziweka Tanzania wameziweka wapi, maana yake mnasema *Richmond* haina *account;* haina *registration* Tanzania wala

Amerika; sasa wanafunguaje *Bank Account?* Hizi pesa zimekwenda wapi, hata tukitaka kuzitafuta, inanitia wasi wasi mkubwa kama kampuni haipo Tanzania wala Amerika; tutazitafutia wapi hizi pesa wanazolipwa na kwenye *account* ya nani au zinalipwa mifukoni mwa watu? *(Makofi)*

Hili ni jambo la hatari kabisa, umeme wa Tanzania *Hydro Electrict, hydro power* ni umeme ambao ni rahisi kabisa kuliko umeme wa aina yoyote duniani, lakini sasa umeme wetu umekwisha kuwa ghali kupita kiasi, hata ile *connection* inakuwa ni hatari. Sisi tunawasifu watu wa simu, wanakuletea mpaka pale kwenye nyumba yako, wanaanza kulipa, lakini *TANESCO* wanataka mpaka tuwachangie kufanya *service* yao. Kwa sababu ya madudu haya, inakuwa ni lazima tuingie mfukoni tuwachangie ili waweze kujiendesha na siyo kujiendesha ili wasaidie kulipa hizo *capacity building charge* ili wazidi kulipa na hizo pesa wazalishe umeme au wasizalishe, zinalipwa tu. Jamani, hivi kweli hakuna mtu mwenye akili kidogo, tukatafuta namna ya kujiokoa katika hili. *(Kicheko/Makofi)*

Kama wapo, tuwaombe hili ni janga la hatari. Wananchi wanakufa na nchi yetu ni tajiri, kama nchi hii ingekuwa ni maskini sawa, Tanzania siyo maskini jamani. Mimi sina mengi ya kuongeza, isipokuwa ninasema maamuzi ya Kamati Teule kama walivyo-*recommend,* tuhakikishe yanatimizwa na hatua za ziada za kuwafilisi waliopokea hizi pesa, kuwapeleka Polisi na kuchunguzwa, zichukuliwe ili Watanzania wajue kweli tuna imani na nchi yetu. Watanzania wanachanganyikiwa hasa Serikali inapokuwa leo inasema hili, kesho inasema lile. *Richmond* wanasema kila kitu safi, leo inakuja kuonekana ni chafu; Watanzania watasema hii ni Serikali gani!

Watanzania wanachanganyikiwa ni lazima tufike mahali sasa tuanze upya na tuwe *honest;* kama unataka kufanya kazi fanya, kama unaona huu mshahara hautoshi nenda kafanye biashara, hata kuchimba makaa ni biashara vile vile.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninaomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru sana, kwa kunipa nafasi hii. Ninaomba nianze moja kwa moja, kwa kuipongeza Kamati Teule iliyofanya kazi nzuri sana katika mwaka huu. *(Makofi)*

Ninajua yatasemwa maneno mengi na wengine watajaribu kutafuta mchawi ili kui-*dis-credit report* hii, lakini *by all intents* ripoti ni nzuri, ina vielelezo na yote yale waliyoyazungumza, yana ushahidi, hakuna kitu ambacho hakina ushahidi mle ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni yetu sote na mimi mara nyingi, nimekuwa ninalizungumza hili na huwa ninasema hivyo kisha wanachanganya maneno, ninasema *we all have a stake in the development of this country.* *(Makofi)*

Ndugu zetu wamekabidhiwa madaraka ya nchi hii, tunahitaji kuendelea mbele. Tunahitaji viongozi wawe na *vision* ni namna gani tunatoka *point A* kwenda *point B.* Bahati mbaya sana, Watanzania walio wengi na ambao wanaelewa vitu katika nchi hii, wengine wameanza kukata tamaa, wanasema sioni ni namna gani nchi hii sasa itapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nchi hii tunataka maendeleo. Nchi hii hatujapigana vita, nchi hii hatuna ugomvi na mtu, nchi hii ni sisi wenyewe tunajikanyaga kanyaga hapa. Maendeleo yetu tunayazima sisi wenyewe, kuanzia sasa uchafu basi. Tuwatendee haki waliotuleta humu ndani. Sisi Wabunge ndiyo tunawawakilisha watu maskini sana katika Taifa hili. Kinachofanya watu waibe na hapa ninaomba nitofautiane na kaka yangu, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, siyo umaskini, tamaa ndiyo inafanya watu wafike hapa. *(Makofi)*

Hivi sasa nje ya nchi, kwa sababu tumeshazoea kusaini mikataba bila utaratibu mzuri, mtu anaona anaweza kusaini mkataba mahali popote na akaja akatuambia alisaini mkataba na sisi tukakubali. Kuanzia sasa, mikataba ya namna hiyo basi, hatuihitaji tena. Tunachokihitaji katika Taifa hili sasa, mikataba yote lazima ipite Bungeni, hata ile ya ku-*ratify*, iletwe hapa, Wabunge waione kama wawakilishi wa watu, wakishaiona ndiyo waseme tunaweza tukatekeleza. Kuna kitu kinaitwa ku-*initial an agreement;* unasaini *agreement* ambayo Bunge hili kama wawakilishi wa watu, hawajui kinachoendelea mle ndani, lakini wakati mwingine kwa sababu mikataba hii inakuwa *initialled* huko nje, hata yule anaye-*initial* wakati mwingine ndani ya mikataba hii *clause* mojawapo inasema *although* huu mkataba tunaousaini hivi sasa, *is only an interim agreement* mbele ya safari; *a framework agreement, comperehensive agreement* itakapokuwa *signed*, haitabadilisha *fundamental clauses* ndani ya mkataba, umeshaifunga nchi, huwezi tena kwenda mbele zaidi. Uwezo wa kuwasaidia Watanzania sasa hakuna, unapofanya kazi hiyo. *(Makofi)*

La pili, ninafikiri Watanzania walio wengi ndani ya Serikali, hawajali maslahi ya Taifa hili, kwa sababu hawamjui Mungu. Wanajifanya wanamjua Mungu kwa kuvaa ngozi ya kondoo lakini wanajidai huku wamemsahau, kwa sasa hivi naweza nikamsahau Mungu. Lakini wanavyokwenda kufanya wanafanya vitu tofauti.

Mheshimiwa Spika, ninafikiri watu wetu sasa wanahitaji kubadilika na *our style of management* ya *economy* hii lazima pia ibadilike, tufanye mambo tofauti na tunavyofanya hivi sasa. Ukiangalia ripoti ya Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, kuna ufunguzi wa *Letter of Credit;* kwa mtu yeyote anayeelewa maana ya *Letter of Credit* ni kwamba, sisi tulijitolea kama Serikali, kumsaidia huyu mtu. Huyu mtu amekuja hapa hata senti tano hana, lakini kwa ulafi wetu, tumekubali kumfanyia biashara na kumpa pesa. *Letter of Credit* unamfungulia kila kitu unafanya, huku umeshaingia mkataba, unamwambia sema kilichopungua bwana, mnamwomba; mnamwomba ya kazi gani? Kwenye *merchandize trading,* tumekuwa tunawafanyia wafanyabiashara biashara zao, tunawafungulia mpaka *Letter of Credit, worth a million and billions.* Nina ushahidi, lakini kwenye rushwa hii na usimamizi wa rushwa katika Taifa hili, ninafikiri

tunakwenda vibaya. Ziko tuhuma zinaituhumu hii TAKUKURU, ichunguzwe nayo. *(Makofi)*

Hawatendi haki kwa Watanzania na ndiyo maana mambo mengi yanakwenda ovyo. Waheshimiwa Wabunge, ipo ripoti inasema, TAKUKURU kazi yake ni kuwalinda watu wengine, mimi siyo mbaguzi, lakini ninanukuu ripoti inavyosema: "TAKUKURU wanachofanya ni kushirikiana na wafanyabiashara tofauti na ngozi hii." Sasa wanafanya hivyo, ili waimalize nchi hii. Ipo ripoti ndefu. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, tukimaliza hii sasa tunakwenda vingine, nazo tunataka zichunguzwe na TAKUKURU ni mojawapo ambayo tunataka ichunguzwe na mikataba mingine ya vitu kama MEREMETA na yote iliyoichafua Taifa hili na kuiingiza nchi hii kwenye matatizo makubwa, mashirika yote hayo yachunguzwe. Tutakuta nchi hii imepoteza *billions. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoteza *billions* kila siku, kwa vitu visivyokuwa vya msingi. Hizi za hii *Richmond*, mwaka 2004 nilisimama hapa nikasema, *Richmond* si Kampuni ni matapeli wa hapa hapa, wanaojifanya wanatoka Huston ila *they have connections* kule Huston. 2004 mimi nilikuwa Huston, nililitamka hilo na ninawaombeni hata viongozi humu ndani wawe wanasikiliza ushauri unaotolewa na sisi Wabunge. *(Makofi)*

Si bahati mbaya kwamba, tunakuja humu ndani ya Bunge tunasema sema tu, yapo mengine tunayajua. *Richmond* amekuja hapa, mara ya kwanza tulimpa *pipe line* tukamfukuza Mswahili mwenzetu kama mbwa, bahati mbaya yule Mswahili alikuwa ameshapata pesa *from an Investor in Canada.* Nilikwenda South Africa wakati fulani, nikakutana na watu wanaomfahamu *Richmond* huyo, anayesemwa ni *Richmond,* wakasema ni mtu anayetafuta fedha kama huyo huyo Mtanzania, ambaye alikuwa a-*own* hii *pipe line* na tulikuwa tayari tumejitolea kumsaidia huyu apate mwekezaji halisi wa kujenga hii *pipe line,* lakini mmemfukuza, *Richmond will never do anything.* Nikasema ngoja mwone, 2004 imemalizika 2005, *pipe line* hakuna, Rais wetu wakati ule Rais Mkapa, alikwenda Uganda aka-*sign communique* na Rais Museveni ya ku-*extend pipe line* kutoka Mwanza kwenda Uganda, sisi tumekaa tu, tunasema hapana, tunakwenda bwana tunaendelea, lakini kuendelea kwetu ni kule kwa tumboni. *(Kicheko)*

Wakati ule tumeshasaini walisema, jamani sasa tuanze kujenga *pipe line* nimeshapata mwekezaji; wewe huna hela bwana! Mtu mmoja akaniambia hapana, yule bwana ana mkono wa birika, hawezi kuendesha *pipe line* hapa tutampa mtu mwingine. Mtu aliyepewa *Richmond, account* hana na *experience* ni *zero;* naye anatafuta pesa kama huyo Mswahili wa hapa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mimi ninasema mtu aliyekufa hapigwi mijeledi. Ninarudia, mtu aliyekufa hapigwi mijeledi, hapa tunapiga mijeledi watu waliokufa. Ngojeni nieleze, hoja tunayoizungumzia, mambo yameshakuwa mabaya; *Tanzania is paying billions in a year.* Si kwamba, Watanzania walikuwa hawajui, katika barua zinazo-*circulate* sasa hivi walijua, wakasema hapana, huu ni upinzani wa kibiashara. Mmefanya uchunguzi? Kwa sababu ni uchunguzi ndio uliokuwa unatakiwa; watu

wafanye uchunguzi, wajiridhishe na huyu *Richmond.* Kabla mkataba haujaingiwa, wakasema hapana, huu ni upinzani wa kibiashara tu; kwanza, upinzani wa kibiashara una faida kubwa katika nchi; unajenga *efficiency* ndani ya nchi na unapunguza bei za yale tunayotaka, bei ya umeme ingepungua ndani ya nchi, ndiyo upinzani wa kibiashara unachofanya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nirudie kusema tena; sasa mikataba ya kiholela basi. Mikataba ile tunayotekeleza hivi sasa yote iletwe Bungeni, tunahitaji nayo ichunguzwe. Pili, mikataba yote ambayo itaingiwa na Serikali hii au Serikali nyingine inayokuja, iletwe hapa. *Recommendation* yangu moja kwa maneno mengi yanayozungumzwa hapa, mimi nimekuandikia wewe; nimesema, tusaidie tuanzishe Kamati ya kufuatilia maneno yanayosemwa na Serikali hapa mbele ya Bunge, kwani mengine hayana tija. *(Makofi)*

Hatutaki kuisaidia Serikali tu, tutakisaidia na Chama cha Mapinduzi, ambacho ndicho chenye Serikali, kwa hiyoi, tunaihitaji hiyo Kamati na itafanya mambo mengi. Nilifikiri niyaseme tu haya kwamba, hali iko namna hii: bwana tumejifedhehesha sana au tumefedheheshwa sana na viongozi wote waliohusika na haya mambo. Kila mmoja anasema ameonewa. Mambo haya yote yameifanya nchi inaingia hasara, kila mmoja anasema ameonewa, haiwezakani Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Hii inakwenda *back* kwa Adam wakati ule, alipokutwa na mke wake kule Bustani ya Edeni akaanza kumkimbia Mungu. Alipomkimbia Mungu; Mungu akamwauliza mbona unakimbia, akasema si yule mwanamke uliyenipa. Sasa hawa nao wanasema sijui nani tena, kila mmoja anasema si yule bwana ambaye yuko juu yangu. Waheshimiwa Wabunge, *spirit* hii tuliyoianza ni *spirit* ambayo watu wa nje wameniletea ujumbe wanasema, tunamwomba Mwenyezi Mungu, kila aliyekosea atetemeke na aondoke humu ndani. Hakuna mzaha kwa maendeleo ya Watanzania. *(Kicheko/Makofi)*

Watu wa Mungu hao wanasema. Mungu anasema mwite Mwenyezi Mungu, maana ukimwita atakuonyesha mambo makubwa, magumu na usiyoyajua. Sisi tumejua tusiyoyajua, maana hatukujua haya yote yanatendeka lakini yako mengi. Tutaomba yaletwe hapa, tuyachunguze nayo, tuweze kubaini mabaya yaliyoko, tuyasahihishe. Nchi hii tuna njaa ya maendeleo, hii njaa ya maendeleo lazima tuitekeleze na Bunge hili ndiyo lenye dhamana ya kuhakikisha hayo yanatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, ninaomba Mungu akujaalie, uongoze vikao hivi kwa neema ya Mwenyezi Mungu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi. Ninashawishika kuamini kwamba, unapata semina za Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare, kwa sababu unazungumza kama vile kuna nguvu za Mungu nyuma yako. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya kipekee, kukushukuru sana kwa kupata hii muhimu ya kuchangia hili tatizo ambalo liko mbele

yetu la *Richmond.* Mimi bahati mbaya, siyo msemaji sana, kama wenzangu waliotangulia, lakini nilikuwa ninategemea kwamba, kama ningepewa nafasi ya kuwashughulikia hawa mafisadi kwa kweli ingekuwa nafuu sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yono S. Kevela, hairuhusiwi kuwashughulikia humu ila kwa hotuba tu. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, mpaka sasa hivi wananchi wanaotusikia, hawaelewi tunafanya nini. Kwa mfano, wananiuliza Bwana Yono; hivi huko Bungeni mbona umekuwa mkimya sana; mbona umekuwa bubu, mambo yanavyokwenda mbona hatutegemei kama wewe mwenzetu unaenda kutuwakilisha kama ni sauti ya wananchi?

Ninasema jamani kuna taratibu, lakini leo nimepata nafasi ya kuchangia hili, kwa kweli ninampongeza kipekee ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, pamoja na timu yake, kazi waliyofanya ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, siwezi nikasema ninawapongeza hao bila kukupongeza na wewe Spika, kwa sababu na wewe umekuwa jasiri. Unajua mpaka unawachagua hawa watu, uligundua kwamba wanaweza wakakufanyia kazi vizuri. Kwa hiyo, ninakupongeza sana. Duniani hapa tuna tatizo moja kwamba, hatupendi lawama, kila mmoja sasa hivi akitaka kuchangia anakwepa kwepa. Hata unapotaka kujitokeza, unasema hapa utapoteza na Ubunge, utaonekana mbaya, utafanya nini. Waheshimiwa Wabunge ni vizuri tuondoe uwoga, tuseme kwamba basi, kwa sababu tupo kwa ajili ya maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, pamoja na hizi pongezi, ninafikiria Mheshimiwa Dr. Harrison Mwenyembe, kwa sababu amesaidia mpaka hali inakuwa hivi, analeta Tanzania mpya, walau tungetoa zawadi au sijui bakishishi au sijui tutumie mbinu gani, lakini tungemtengenezea Taasisi ambayo itashughulikia uozo sehemu mbalimbali na kwenye maeneo mbalimbali. Kwa sababu siyo haya tu, yapo mengi; kuna mikataba mingi mibovu mibovu na hata watu wanaosema kwamba, unajua mimi sihusiki; kwa nini usihusike wakati bado kuna makampuni unalalamikiwa bwana; tunashindwa kuelewa? Nenda pale *Container Terminal*, watu wanapiga kelele sana kuna mikataba ya ajabu ajabu iko pale, lakini bado unasema unaonewa; unaonewa nini? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilifikiri tusiishie kwenye *Richmond*, twende kwenye sehemu nyingine ambazo wengine wamejificha. Jimboni kwangu kule Njombe Magharibi, wanapoona nimesimama halafu bado ninachekelea uozo, hawanielewi. Kwa hiyo ni vizuri tubadilike, sasa hivi tuache kusema kwamba, unajua nitakosa Ubunge; Ubunge huu analeta Mwenyezi Mungu; hatukuingia Ubunge kwa sababu tuna pesa nyingi, watu walituamini wakasema huyu anaweza kutusaidia. Kwa hiyo, ninafikiria kwamba, tusiishie kwenye *Richmond*, tuangalie na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi ya kipekee, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyoshughulikia

mikataba mibovu na kuirekebisha kupitia Tume, hasa ile tume ya kupitia mikataba mibovu ya madini na jinsi anavyowawajibisha akina Balali na kuteua Magavana ambao ni waaminifu. Kwa hiyo, ninampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia Wabunge wenzangu wote, ambao wanajitoa muhanga na wale ambao wanakaa kimya, lakini moyoni wanasema hapana, ningesimama ningesema haya na haya. Kwa hiyo, ninawapongeza sana, wapo kwa ajili ya kutetea maslahi ya wazalendo. Sio siri, sisi Wabunge ndio masikio ya wananchi na ndio sauti zao, tukikaa kimya tutakuwa tunatenda kosa kubwa sana ni lazima tutetee maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kwamba, kitaaluma mimi ni mtaalamu wa ugavi. Wengine wanasema mimi ni dalali, sijui Yono nini? Siyo kweli, mimi ni mtaalamu wa ugavi. Nimefanya kazi kwenye mabenki; nilikuwa *CRDB* na nimesajiliwa kwenye Bodi ya *Material Management (NBMM).* Sasa ninapozungumza hivi, ninataka niwapongeze sana wenzangu wa *TANESCO*, ambao walishughulikia mambo ya zabuni. Wameonyesha ujasiri mkubwa sana, lakini sasa ujasiri wao ulifika kipindi wakaogopa kwamba, wanaweza wakapoteza vibarua. Nimeona wamekataa mara tatu kwamba, hii *Richmond* haifai kabisa, mara tatu bado kidogo jogoo awike. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa wale Wakristo, ninadhani wanafahamu maana yake kwamba, hiki kitu wanapokataa mara tatu baadaye walipozidiwa, wakaona hapana hapa tutapoteza kazi. Yupo ndugu yangu pale Suke, Mkurugenzi wa Ugavi ni Mtaalamu, tulikuwa wote *MB*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akawa ananieleza udhaifu wa pale *Richmond*, lakini sitaki kumnukuu asije kupata matatizo. *(Kicheko)*

Ninavyofahamu mimi ni kwamba, kulikuwa kuna kampuni ambayo ina-*qualify* kabisa, sijui walitumia *International Shopping?* Ilikuwa pale India ambayo, ilikuwa ina mitambo mizuri, ingeweza kufanya kazi vizuri lakini sio hawa akina *Richmond*, ambao ni matapeli; lakini sasa wafanye nini? Hata yale mambo ya *short listing*, unasema kwamba ni siku kumi, wakati sheria zinasema siku 45! Mimi ni mtaalamu; kukiwa kuna chochote unasema siku kumi! Ninashindwa kuelewa; kukiwa na chochote siku kumi au hata siku mbili! *(Kicheko/Makofi)*

Sasa hiyo haraka ilikuwa kwa ajili ya nini, kama hawakula chochote? Kwa hiyo, nilikuwa ninajaribu kuangalia hata ile *GNT;* ile timu ya Wataalamu, ambayo iliwashirikisha, ilishirikisha sehemu mbalimbali; yaani Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha; sasa sielewi wale Wataalamu sijui kulikuwa kuna nini? Pale hata ningefanya mimi peke yangu, ningeweza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna mawingu fulani fulani ni lazima useme kwamba, lazima tuweke Wataalamu, tufanye hivi na hivi na mimi niwatetea wenzangu hawa. Nitakuwa tofauti kidogo, nitawatetea wenzangu hawa ambao walikuwa chini wanaagizwa; kama Waziri muhusika anaagizwa, hawa wa chini watafanya nini? *(Kicheko)*

Hawa *TAKUKURU,* ninadhani watakuwa *TAKUKURU* au sijui Mwana Sheria; kama wanaagizwa wafanye nini jamani? Lazima tuwe wakweli, lakini sasa inatakiwa tuwe mashujaa kama Dokta Idrisa alivyosema anajiuzulu, ule ndiyo uzalendo. Sasa wewe unang'ang'ania mkate, badala ya kung'ang'ania maslahi ya wananchi? Tufike mahali tuseme kwamba haiwezekani, tuwe na msimamo. Tusiwe tunaogopa ogopa, kwa sababu woga ndiyo uliotufanya tuwe katika hali kama hii. Mimi hapa kama Bwana Yono, ningekuwa mwoga kwamba, unajua nitakosa Ubunge; nisingesimama hapa. Mimi niko radhi kwa yoyote; kama tunatetea maslahi ya wananchi, lazima tutetee kabisa tusiogope, hivi vyeo vinapita. Ninawapongeza sana wenzangu waliopita, wamezungumza vizuri na mimi ninakuwa kama ninarudia rudia. Bado dakika tano?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli leo lazima tuzungumze. Wananchi wanalalamika kuhusu suala la kupanda kwa bidhaa, hata mafuta ya taa na viberiti sasa hivi zimekuwa bei juu, yaani hali ni mbaya, watu wanateseka sana. Tatizo ni hawa akina mdudu *Richmond.* Mafuta na umeme kupanda, ndio sababu inayosababisha vitu vipande haraka haraka. Kwa wachumi wanafahamu hilo, sasa ni vizuri tufikie hatua kwamba, ili kupunguza gharama za bidhaa ni lazima tudhibiti ufisadi, rushwa na mambo mengi machafu ambayo yapo. Bahati mbaya, kuna watu wengine ni waadilifu sana katika hii Serikali yetu, lakini hawa wanaopatikana na hali mbaya ni vizuri kama wanavyosema kwamba wajiuzulu kama kawaida, mimi siwaonei huruma hata kidogo. Ikiwa wanaona wameonewa si waende Mahakamani au waje kujitetea hapa Bungeni kwamba, mimi iko hivi na hivi, lakini tusiseme kwamba, unajua! Lazima utoe sababu kwamba, umeonewa wapi, lakini jinsi ripoti zilivyoonekana, siwezi nikawahukumu sana kwamba wameonewa au vipi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, amejitahidi sana tana sana. Lingine nizungumze kuhusu suala la magerezani. Wenzangu wanasema hawa wanaopatikana, wakibainika wana matatizo haya wapelekwe magerezani, lakini ninavyojaribu kuangalia; mimi nilitembelea magereza pale Ukonga, niliona ni watu wa chini sana (maskini), sio wale wenye vitambi, wenye uwezo au matajiri, sasa kuna nini? Inavyoonekana ufisadi mwingine uko hata sehemu kama hizo; ni vizuri katika haki tuangalie hawa watu wadogo, lakini hawa watu wakubwa wenye vitambi, hatuwapeleki magerezani. Sasa ifikie hatua kwamba, kama Mungu atatujalia tutende haki, kama tukigundua kwamba kuna matatizo haya, mbali ya kufilisiwa, wapelekwe magerezani kama kawaida. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba unilinde kidogo. Kwa sababu kule magerezani ufisadi upo, kama kweli tukiwapeleka kule itakuwa safi zaidi. Kwa hiyo, niseme kwamba ni vizuri tuangalie kwa nini hali iko hivyo na sisi wenye ngozi nyeusi kama tumelaanika. Mimi nilipokwenda Ujerumani na Japani, sikuona ngozi nyeusi kama uko chini sana ni ngozi ambayo ina thamani kubwa sana. Tunapokuwa kwenye nchi yetu, tunaonekana kama hatuna thamani, ukiwa mweusi hata mikopo unaonekana kama una matatizo, lakini hawa watu ambao ni rangi nyeupe, ninaona wanatuingiza kwenye matatizo sana. Sisemi wote, ninaomba nieleweke. Wakienda kwenye vyombo vya fedha wanatetemekewa, wakitaka ubia *free way,* kwa hiyo, nilifikiri tuwe waangalifu. Sasa hivi tuelewe kwamba, ngozi yetu nyeusi ina thamani na inaweza ikafanya kitu fulani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninadhani wenzangu watamalizia, nisije nikamaliza uhondo. Hapa hapa kuna kipindi fulani nilisema, jamani mimi nina uwezo wa kushughulikia dawa za kulevya, lakini wenzangu wakasema hapana hii miradi ya wakubwa. Nilijaribu kupeleka ujumbe haukujibiwa, sasa sikuelewa kama tungegusa mikono ya mafisadi au vipi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, niwashukuru sana kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu ambayo nimeifunga ilikuwa na waliotaka kuchangia 59. Sasa kwa wastani kuanzia saa 11.00 hadi saa 01.45, kwa dakika 15, 15, wanaweza wakachangia Waheshimiwa Wabunge 23. Kwa hiyo ni dhahiri sasa, kwa hawa 50 waliosalia, tutamalizia kesho na 23 watachangia Jumatatu; sasa ninadhani ningetoa rai, wale ambao yale waliyokusudia kuyasema, kuna wenzao wamekwisha yasema, basi watuletee taarifa hapa ili tuweze kupunguza majina. *(Makofi)*

Ninajua jambo hili lina hisia kali, lakini pia tunazo Kanuni kuhusu kurudia rudia, nimekuwa rahimu tu kama Spika, nimejaribu kuwavumilia. Wengine wanarudia yale yale yaliyosemwa na wengine, lakini ninaelewa ni muhimu sana Mbunge kusikika. Nitoe mfano wangu tu, leo kuna mwananchi mmoja wa Dodoma, alikuwa analalamika akamwuliza *taxi driver;* "Huyu Spika, hivi hana hisa kwenye *Richmond*; mbona yeye halalamiki?" Kwa hiyo, jambo hili inaonekana usiposema tu; hawajui kwamba kwa Kanuni siruhusiwi kutoa hotuba humu. Ninadhani pamoja na yote hayo, nitawaomba wale ambao wanaona si lazima waseme sasa, basi waturejeshee majina ili tubaki na orodha ambayo itatuwezesha kumaliza siku ya Jumatatu ili Jumanne tuingie katika shughuli nyingine. *(Kicheko)*

Samahani, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, itabidi nianze na Kiongozi wa Upinzani ile saa 04.30, halafu nitakupatia nafasi hapo kadiri tutakavyoendelea. Hii yote tumejifunza kwa *Westminster*, anapotaka kuchangia Kiongozi wa Upinzani, anapewa kipaumbele. Kwa hiyo, atakuwa yeye halafu Mheshimiwa Mgana Msindai, simwoni hapa, halafu ndiyo Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya. Baada ya hapo, tutaendelea sasa na wengine. *(Makofi)*

Wahesimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kwa sababu muda uliosalia, hautuwezeshi hata Mbunge mmoja kuweza kuchangia haki yake ya dakika 15, basi ninaliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.41 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 08 Februari, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*